# SIFA ZA

# MWENYEZI MUNGU MTUKUFU

# KATIKA

# AGANO LA KALE NA QURAN TUKUFU



MTAYARISHAJI:

RAAJII RIDHWAA ALLAH

MTAFITI KATIKA MLINGANISHO WA DINI MBALIMBALI

*Kimefasiriwa na Omari J. Mangilile*

*Kimepitiwa na Shaibu Swalehe Saidi*

www.islamic-invitation.com

# UTANGULIZI

Mpendwa msomaji:

Je, unaamini kuwa Mwenyezi Mungu ana sifa za ukamilifu?

Kama jibu lako ni ndio… Hapana budi kitabu chake kilichoteremshwa kwa wanadamu nacho kiwe kikamilifu.

Je, unaamini kuwa Manabii na Mitume, amani iwe juu yao, wamelindwa na wapo safi hawafanyi maasi, uzinzi na machafu?

Je, hapo kabla, umeshawahi kufanya mlinganisho baina ya sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Agano la Kale na Quran Tukufu?

Mimi ninakuomba kwa mapenzi yote na moyo safi, tafuta uhakika katika kitabu hiki ambacho huenda kikafungua – Mungu akipenda – nyoyo za wale wenye shauku ya kuokoka na kuongoka.

Samahani ewe mpendwa msomaji, kwa kutaja baadhi ya maandiko ya kimapenzi yenye kutia aibu. Kwani mimi nimenukuu kwa ajili ya kutolea ushahidi tu.

## Sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Quran Tukufu

Kila utakavyofikiri kwa kina katika ulimwengu huu na vile vilivyomo miongoni mwa mambo ya ajabu, na namna madhubuti, mahusiano bora na ufundi wa hali ya juu wa vitu vya ulimwengu. Kwa hakika utazidisha yakini kuwa ulimwengu huu una Muumba aliyevifanya viumbe viwepo . . . Na kwa hakika, Muumba huyu, Mwenye kufanya viumbe viwepo, hapana budi atakuwa ni: Mtukufu kuliko vile zinavyopata taswira akili dhaifu za wanadamu. Ni mwenye uwezo zaidi ya vile wanavyofahamu watu kuhusu maana za uwezo. Na ni mjuzi kwa mipaka mipana zaidi ya ujuzi… Na kwa ujumla, hakika Mtengezaji wa ulimwengu huu ni mwenye kusifika na kila sifa ya ukamilifu. … Na ameepukana na kila sifa ya upungufu… Na kwa hakika Quran Tukufu imejaza, imegeuza mitazamo na kuhimiza watu wadumishe tafakuri kuhusiana na neema na vipawa vya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa hakika majina na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Quran Tukufu ni nyingi mno hazitambuliwi zote zote na akili za kibinadamu. Kwa hiyo hatuwezi kudhibiti kuhesabu sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka. Yeye kama alivyojisifia mwenyewe ni Mtukufu Aliyetukuka. Mwenyezi Mungu Mtukufu amekusanya katika Quran Tukufu mema ya kabla yake miongoni mwa vitabu vya waliotangulia, na kuzidisha mambo ya ukamilifu yale yasiyokuwepo katika vitabu vingine. Na akaifanya kuwa ndio kitabu cha mwisho, chenye kukusanya yote, kikuu kuliko vyote na madhubuti kuliko vyote. Na Mwenyezi Mungu akasimamia kukilinda yeye mwenyewe Mtukufu. Kwa andiko lake lililoshuka katika ufunuo wa kuaminika kwa Nabii na Mtume wa Mwisho bwana wetu Muhammad, Rehema na amani ziwe juu yake. **(Hakika Sisi Tumeteremsha mauidha na hakika Sisi ndio Tuyalindao).** Al-Hijr 9.

Wanazuoni wa Kisunni wameyathibitisha majina na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu kama zilivyokuja katika ufunuo wa kuaminika pamoja na kuamini maana zake na kinachojulishwa nazo; bila kuzuia kazi zake, wala kuzifananisha, wala kuzipotosha wala kuziwekea unamna na wala kuzipinga. Wanazipitia kama zilivyokuja pamoja na kuamini maana zake ni kile kinachojulishwa kwazo. Pia wanathibitisha kuwa Mwenyezi Mungu ana sifa za ukamilifu, na wanamtakasa na upungufu na dosari. Wanathibitisha bila kufananisha. Na kumtakasa bila kuzuia kazi zake kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **(Hakuna chochote mfano wake; naye ni mwenye kusikia, mwenye kuona.)** As-shuura 11.

Kwa hakika utafiti juu ya majina na sifa za Mwenyezi Mungu ni muhimu sana. Kwa sababu kumjua Mwenyezi Mungu ni msingi wa imani. Na kwa kuwa jambo hilo ndio tiba yenye nguvu zaidi katika kutibu maradhi ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu. Pia hiyo ni kinga kuu dhidi ya ushirikina. Kwa sababu watu wakizijua sifa za Mola wao, Mtukufu Aliyetukuka na wakajua kiwango cha ukubwa wake, utukufu wa uweza wake, utajiri wake wa kipekee, na upana wa rehema zake, na ukubwa wa adhabu zake, na elimu yake ya kina, na uono wake wa mbali, na ukubwa wa wema wake, na utukufu wa kibri chake, na ukali wa kisasi chake, na upeo wa hekima zake, na kuenea kwa uadilifu wake, hawatoitukuza miungu ya batili, na watajiepusha na miungu hiyo ya bandia. Na muumini atakaposoma sifa za Mwenyezi Mungu katika Quran Tukufu anaziamini. Na imani yake inakuwa matendo mema na kuzidisha imani. Ama mnafiki, yeye anaziona sifa hizo ni za uongo na kuleta kibri. Kwa hiyo anazidisha ukafiri. Atakayezijua sifa za Mola wake atampenda kwa ukubwa wake na rehema zake. Na akimpenda, hilo litamsukuma kutii. Na kama atampenda, basi pendo lake litamkinga na madhambi na kumkataza maasi, na litamsaidia kuvumilia mabalaa. Pia litamsaidia kutii na litamsukuma kujitoa kwa ajili yake.

Na muumini ni mwenye dhana nzuri kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka. Anamjua Mola wake kupitia majina na sifa nzuri za Mola wake. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **(Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye majina mazuri; basi Mwombeni kwayo…).** Al-Aaraf 180. Huyo muumini atakapokuwa na dhana nzuri kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atatenda matendo mazuri. Kwa sababu yeye anataraji kwa matendo hayo radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka. Huku akijua kuwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka ndiye; Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Kwa hiyo anatarajia rehema na pepo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka. Na kama muumini atatumbukia katika maasi hatokata tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu ambaye ni Mpokea toba, Msamehevu, kwa hiyo ataweka dhana nzuri kwa Mwenyezi Mungu, na kutarajia kutoka kwa Mwenyezi Mungu apate toba na kusamehewa.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameifanya dhana mbaya kwa majina na sifa zake kuwa ni sababu miongoni mwa sababu kupata hasara: **(Na hii dhana yenu mliyomdhania Mola wenu imewaangamizeni; na mmekuwa miongoni mwa wenye hasara)**. Ha-Mym-Sajdah (Fuswilat) 23.

Wayahudi na Wakristo wameshughulika (wapo bize) wameacha kumpwekesha Mwenyezi Mungu (kuwa na Mungu mmoja kikweli kweli) kikamilifu, na hayo ni kwa kile walichokizua cha kusema eti Mwenyezi Mungu Mtukufu amejifanyiaa mtoto. **(Na Mayahudi wanasema: Uzeir ni mwana wa Mwenyezi Mungu; na Wakristo wanasema, Masihi ni mwana wa Mwenyezi Mungu; hayo ni maneno ya vinywa vyao tu, wanayaiga maneno ya wale waliokufuru zamani. Mwenyezi Mungu Awaangamize! Wanageuzwa namna gani!)** At-tawba 30. Ameepukana Mwenyezi Mungu Mtukufu na hayo. Kwani anayehitaji mtoto ni mdhaifu anayekufa na kubakisha mwanawe baada yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu yu hai hafi. Kwa hiyo haihitaji yeyote. Anayehitaji mtoto ni Yule anayedhoofika uzeeni na kujiwa na ukongwe. Kwa hiyo anahitaji atakayemsaidia. Kwani kiumbe ni dhaifu kwa maumbile yake, ni fukara kwa muumba wake, anahitaji mali, watoto na wasaidizi wa kumsaidia katika shida zake. Ama Mwenyezi Mungu Mtukufu yeye ni tajiri, mwenye sifa njema, Mtukufu Aliyetukuka amesema: **(Enyi watu wa Kitabu! Msiruke mipaka ya dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo kweli; Masihi Isa bin Mariamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno Lake tu Alilompelekea Mariamu, na ni roho iliyotoka Kwake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake; wala msiseme watatu, jizuieni, itakuwa bora kwenu; bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mungu Mmoja tu. Ni mbali na utakatifu Wake ya kwamba Awe na mwana. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mlinzi.)** Annisaa 171. **(Wanasema: Mwenyezi Mungu Amepanga mwana! Ameepukana na hayo, Yeye Anajitosheleza. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Ninyi hamna dalili kwa hayo. Je, mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua?)** Yunus 68. **(Na sema: Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu Ambaye Hakupanga mwana wala Hana mshirika katika ufalme, wala Hana rafiki kwa sababu ya udhaifu; na umtukuze kwa matukuzo makuu.)** Bani Israili 111.

Uislamu una msimamo gani kuhusiana na Agano la Kale? Uislamu haukubali vitabu vilivyomo katika Agano la Kale. Kwa hakika Uislamu umeikubali waziwazi Taurati iliyoteremshwa kwa msemeshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mussa, amani iwe juu yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliyeiteremsha na kuifunua kwa Nabii wake pale aliposema**: (Amekuteremshia Kitabu chenye haki ndani yake kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake; na Aliteremsha Taurati na Injili kabla (ya hiki) kuwa mwongozo kwa watu; na Ameteremsha Kipambanuzi.)** Aali-Imran 3. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ameisifu hiyo Taurati safi na ya haki kwa sifa nzuri nzuri pale aliposema: **(Hakika Tuliteremsha Taurati yenye mwongozo na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia, kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu, nao walikuwa mashahidi juu yake...)** Al-Maidah 44. Na akasema: **(Na kwa yakini Tuliwapa Musa na Harun Kipambanuzi na mwanga na mawaidha kwa wacha-Mungu.)** Al-Anbiyaa 48.

Baada ya Uislamu kuikubali Taurati iliyoteremshwa kutoka kwa Mungu wa Haki Mtukufu Aliyetukuka, Quran Tukufu imethibitisha kuwa Wayahudi kwa sasa wana Taurati nyingine, lakini sio ile Taurati ya kweli ya Mussa, amani iwe juu yake. Wamechukua jina lake na kubadilisha yaliyomo na kupotosha maneno kwa kuyatoa katika maeneo yake na wakavunja ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu alipowatuhumu na kuwapa changamoto walete ile Taurati sahihi ili waisambaze duniani leo hii au katika muda wowote na sehemu yeyote, pale Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema: **(... Sema: Leteni Taurati na mwisome ikiwa mnasema kweli.)** Aali-Imran 93. Allah ameonesha hoja za kuonesha kuwepo kwa upotoshaji ndani ya Taurati yao pale Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema: **(... Sema: Ni nani Aliyekiteremsha Kitabu alicholeta Musa, chenye nuru na mwongozo kwa watu, mlichokifanya nyaraka-nyaraka, mkadhihirisha sehemu yake na yaliyo mengi mkayaficha?...)** Al-An-am 91. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: **(Enyi watu wa Kitabu! Hakika amekwisha wafikieni Mtume Wetu, huwadhihirishieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na husamehe mengi. Bila shaka imekwisha wafikieni Nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Kitabu kinachobainisha.)** Al-Maidah 15.

Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ameifanya Quran Tukufu kuwa ndio kitabu cha kukihifadhi kwa vitabu vyote vya waliotangulia. Kwa maana chenyewe ndio shahidi, hakimu, rejea, msimamizi, kipimo na msahihishaji wa vitabu hivyo: **(Na Tumekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikidha yaliyokuwa kabla yake katika Kitabu, na kukihifadhi, basi uwahukumu baina yao kwa yale Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki iliyokufikia; kila mmoja wenu Tumemjaalia desturi na njia maalumu; na kama Mwenyezi Mungu Angalipenda Angewafanyeni kundi moja, lakini Anataka kuwajaribuni kwa hayo aliyowapeni. Basi shindaneni katika mambo ya heri. Ninyi nyote marudio yenu ni kwa Mwenyezi Mungu; naye Atawaambieni yale mliyokuwa mkihitilafiana.)** Al-Maidah 48.

❊ ❊ ❊


**Sifa za Mwenyezi Mungu kama zilivotufikia kutoka katika maandiko ya Agano la Kale la kisasa**

1- Mungu Mmoja: Wayahudi walikuwa wanafuata dini ya kuwa na Mungu mmoja kwa baadhi ya nyakati na hili linajulishwa na: ''Sikiza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja. Nawe mpende BWANA, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.'' Kumbukumbu la Torati 6:4-5: ''Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine; zaidi yangu mimi hapana Mungu; nitakufunga mshipi ijapokuwa hukunijua; ili wapate kujua toka mawio ya jua, na toka magharibi, ya kuwa hapana mwingine zaidi ya mimi; Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine.'' Isaya 45:5-6. Lakini, je, Wayahudi walishirikisha miungu mingi katika Ulezi na Uumbaji wa Mungu na Uungu wa kuabudiwa?

Ndio, Wayahudi walishirikisha katika Ulezi na Uumbaji wa Mungu na wakaamini kuwa mwezi unadhuru na kuathiri watu, kwani huo mwezi unachochea magonjwa ya kiakili kama vile Uwendawazimu na kupagawa. (Kamusi ya Biblia ukrasa 743). Kama Wayahudi walivyodhani kuwa sayari zinawatabiria wao yajayo na kutambua mambo yaliyofichikana. Pia waliona eti sayari zina mamlaka ya kuuongoza ulimwengu na maisha ya wanadamu wenyewe pale walipogundua kuwa katika sayari kuna matukio ya ajabu yanayostahiki kuabudiwa kwa mtazamo wao, badala ya kumwabudi Muumba wa hiyo sayari. (Kamusi ya Biblia ukrasa 958 – 959). Pia tazama: Mwanzo wa Uyahudi kitabu cha Zakkii Shinudah (ukurasa: 487). ''Nao wataitawanya mbele ya jua, na mwezi, na jeshi lote la mbinguni, walivyovipenda, na kuvitumikia, na kuandamana navyo, na kuvitafuta, na kuviabudu...'' Yeremia 8:2: ''Akawaondosha wale makuhani walioabudu sanamu, ambao wafalme wa Yuda waliwaweka ili kufukiza uvumba katika mahali pa juu, ndani ya miji ya Yuda, na katika kila mahali, pande zote za Yerusalemu; na hao pia waliomfukizia uvumba Baali, na jua, na mwezi, na sayari, na jeshi lote la mbinguni.'' 2 Wafalme 23:5

Pia Wayahudi walimshirikisha Mungu na vitu vingine katika Uungu wake wa kuabudiwa. Imekuja katika vitabu vyao: ''Wana wa Israeli walifanya yaliyokuwa ni maovu mbele za macho ya BWANA, nao wakawatumikia Mabaali. Wakamwacha BWANA Mungu wa baba zao, aliyewaleta kutoka katika nchi ya Misri, wakafuata miungu mingine, baadhi ya miungu ya watu wale waliokaa karibu nao pande zote, wakajiinamisha mbele yao; wakamkasirisha BWANA, akaghadhibika. Wakamwacha BWANA wakamtumikia Baali na Maashtorethi.'' Waamuzi 2:11-13 ''Basi wana wa Israeli wakaketi kati ya Wakanaani; hao Wahiti, na hao Waamori, na hao Waperizi, na hao Wahivi na hao Wayebusi; wakawaoa binti zao, na binti zao wenyewe wakawaoza wana wao waume, na kuitumikia miungu yao. Wana wa Israeli walifanya yaliyo maovu mbele za macho ya BWANA, nao wakamsahau BWANA, Mungu wao, nao wakawatumikia Mabaali na Maashtorethi. Kwa hiyo hasira za BWANA ziliwaka juu ya Israeli, naye akawauza na kuwatia mikononi mwa Kushan-rishathaimu mfalme wa Mesopotamia; na wana wa Israeli wakamtumikia huyo Kushan-rishathaimu muda wa miaka minane.'' Waamuzi 3:4-8 (Wote walitenda dhambi isipokuwa Daudi, Ezekiel na Josiah; kwa kuwa waliiacha sheria ya Yule Aliye juu kabisa, kwa hiyo ufalme wao ukaenda kwa wengine na utukufu wao ukaenda kwa taifa lingine…). Sira 49:4-6. Vilevile Aahabu (Mfalme wa Wana wa Israeli) aliamwabudu 'Baali', na kufuatwa na Wana wa Israeli wa zama za Nabii Eliyasa (amani iwe juu yake) katika kumwabudu huyo Baali. Licha ya kuwa Nabii Eliyasa aliwakataza wasifanye hivyo, Quran 37:125: **''Je mnamwomba Ba'ali na mnamwacha aliye Mbora wa waumbaji.''** (Tazama Tafsiri ya Twabary ya Quran 37:126). Kwa hakika kuasi na kumshirikisha Mungu kulijirudiarudia sana kwa Wana wa Israeli. Hasa hasa katika Kitabu cha

Waamuzi. Pia hilo likajirudia rudia tena katika Kitabu cha Wafalme. Imeandikwa katika 1 Wafalme 12:28-33: ''Kwa hiyo mfalme akafanya shauri, akafanyiza ng`ombe wawili wa dhahabu, akawaambia watu, Ni vigumu kwenu kupanda kwenda Yerusalemu; tazama, hii ndiyo miungu yenu, enyi Israeli, iliyowapandisha kutoka nchi ya Misri. Akaweka mmoja katika Betheli, na wa pili akamweka katika Dani. Jambo hili likawa dhambi, maana watu walikwenda kuabudu mbele ya kila mmoja, hata huko Dani…). Hiki tulichokitaja kinamfanya kila mwenye akili kuwa na shaka juu ya usahihi wa Agano la Kale la Kisasa na juu ya usalama wake na kutopotoshwa.

|  |  |  |
|---|---|---|
| Wana wa Israeli waliabudu: Ndama | Baali | Ashtaaruthi |

Je, itikadi ya watu hawa ni salama? Mungu amewapelekea Wana wa Israeli Mitume na Manabii wengi ili kuwarudisha tena katika itikadi sahihi, nayo ni kumwabudu Mungu mmoja peke yake, na washuhudie ya kwamba Mungu wa kweli ni mmoja asiye na mshirika na kuwa Masihi Yesu si mwingine ila ni Mtume wa Mungu. ''Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.'' Yohana 17:3 Lakini wafuasi wa Masihi Yesu wamebadilika kidogo kidogo, kutoka katika itikadi (imani) ya Mungu mmoja kwenda katika itikadi ya Utatu Mtakatifu. Nafsi tatu (Baba, Mwana 'Yesu' na Roho Mtakatifu) eti na hao watatu kimsingi ni mmoja. Je, imani ya Mungu Muumba mmoja pekee ndio hiyo hiyo imani ya Utatu wa Mungu mmoja, ''Utatu Mtakatifu''? Au kuna tofauti kubwa baina ya imani mbili hizo?

2- Hazibadiliki wala hazigeuki: Miongoni mwa sifa za Mungu katika Agano la Kale: ''Kwa kuwa mimi, BWANA, sina kigeugeu;...'' Malaki 3:6. Na miongoni mwa sifa za Mungu katika Agano la Jipya: ''Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika,...'' Yakobo 1:17. Ikiwa Mungu habadiliki kutoka Agano la Kale kwenda Agano Jipya. Sasa inakuwaje Mungu Muumba Muabudiwa abadilike kwa Wana wa Israeli, kutoka kuwa Mungu mmoja 'ALUHIIM' na kuwa Mungu mmoja mwenye ''nafsi tatu''? Je, Mungu anabadilika na kufa kisha baadaye anafufuka na kuwa hai?

3- Upole, huruma, kusamehe na wokovu: ''Hakika BWANA mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, anasamehe uovu na anaokoa katika siku ya shida'' Sira 2:11-13 '…akatangaza, BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi...'' Kutoka 34:6-7: ''Lakini mtu mbaya akighairi, na kuacha dhambi zake zote alizozitenda, na kuzishika

amri zangu zote, na kutenda yaliyo halali na haki, hakika ataishi, hatakufa. Dhambi zake zote alizozitenda hazitakumbukwa juu yake hata mojawapo; katika haki yake aliyoitenda ataishi.'' Ezekieli 18:21-22: Kwa hakika mwanadamu akitenda kosa, dhambi au kufanya uhalifu dhidi ya amri za Mungu anapaswa atubu na kuomba msamaha kwa moyo wote. Akifanya hiyo, Mungu anamsamehe; kwa kuwa Mola ni mpole na ni mwingi wa huruma, anasamehe madhambi na kutakasa. Sasa kwa nini hajamhurumia na kumsamehe Adam, (amani iwe juu yake) kwa dhambi zake wakati uleule, badala ya kuleta kisa kinachodaiwa eti kwamba Mungu amemleta mwanawe (Yesu) baada ya kupita maelfu ya miaka ili aje kuuvaa mwili wa mwanadamu, awe fidia, asulubiwe na kuwaokoa wanadamu na dhambi ya mwanzo (dhambi ya kurithi). Ikiwa Mungu ni mpole mwingi wa huruma na anasamehe madhambi, kwa hiyo Adamu, amani iwe juu yake, atakuwa alipokea neno la kutubu kutoka kwa Mola wake, kisha kwa wakati huohuo, yeye na mkewe wakaomba msamaha na kusamehewa dhambi zao?

4- Kuweza na Uwezo: Ayubu, amani iwe juu yake, amethibitisha kuwa, Mungu anaweza kufanya kila kitu na kuwa kwake hakuna lililogumu. ''Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote, Na ya kuwa makusudi yako hayawezi kuzuilika.'' Ayubu 42:2. Je, Mungu anaweza kumpa ufunuo Adam, amani iwe juu yake, wa maneno ya kuomba msamaha ili amsamehe makosa yake? Je, jambo hili ni gumu kwa Mungu?

5- Uadilifu: Dhambi hairithiwi, na mkosaji ndiye anayepaswa kuadhibiwa. Na hapaswi kuadhibiwa mtu mwingine badala ya yule aliyetenda kosa. ''Roho itendayo dhambi, ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe...'' Ezekieli 18:20. ''Mtu awaye yote asitwae jiwe la kusagia, la juu wala la chini, kuwa rehani; kwani hivi ni kutwaa maisha ya mtu kuwa rehani.'' Kumbukumbu la Torati 24:6. '..., Baba za watu wamekula zabibu kali, na meno ya watoto wao yametiwa ganzi. Bali kila mtu atakufa kwa sababu ya uovu wake mwenyewe; kila mtu alaye zabibu kali, meno yake yatatiwa ganzi.'' Yeremia 31:29-30 ''…Je! Nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa kosa langu, mzao wa mwili wangu kwa dhambi ya roho yangu?'' Mika 6:7. Ikiwa Mungu ni mwadilifu na haui watoto kwa makosa na dhambi za mababa. Na kama ikiwa mwana habebi dhambi za baba. Na kila mtu atauawa kwa dhambi zake. Je, ni uadilifu kumwadhibu Yesu Kristo, amani iwe juu yake, kwa makosa ya Adamu, amani iwe juu yake. Makosa ambayo Yesu hakuyatenda,hata hivyo ameadhibiwa ili awakomboe wanadamu kwa dhambi ambayo hairithiwi?

6- Hafanani: ''Basi, mtamlinganisha Mungu na nani? Au mtamfananisha na mfano wa namna gani?'' Isaya 40:18 ''Mtanifananisha na nani, basi, nipate kuwa sawa naye? Asema yeye aliye Mtakatifu.'' Isaya 40:25 ''Mtanifananisha na nani, na kunisawazisha naye, na kunilinganisha naye, ili tuwe sawasawa?'' Isaya 46:5 Ikiwa Mungu amekana kufananishwa na chochote, kwa nini katika Agano la Kale, Mungu amefananishwa na vitu vibaya na machukizo kama vile simba jike na dubu jike? Vilevile, kwa nini Mungu amefananishwa na kupewa sifa za mambo machafu na ugaidi? Je, aliyefananishwa na kusifika kwa sifa hizi anafaa kuwa Mungu wa kuabudiwa?

7- Yu hai na ni Mfalme wa milele: ''Bali BWANA ndiye Mungu wa kweli; Ndiye Mungu aliye hai, Mfalme wa milele;…'' Yeremia 10:10. Ikiwa Mungu ''Ndiye Mungu aliye hai na Mfalme wa milele''. Inakuwaje Mungu huyo amekufa msalabani? Na ni nani aliyeusimamia ulimwengu Mungu huyo alipokufa?

8- Haiwezekani kumwona Mungu: ''Hakika wewe u Mungu uhifichaye nafsi yako, Ee Mungu wa Israeli, Mwokozi.'' Isaya 45:15. ''Kisha akasema, Huwezi kuniona uso wangu, maana mwanadamu hataniona akaishi.'' Kutoka 33:20. Sasa inakuwaje Mungu akadhihiri kwa Mitume na Manabii akiwa katika mwili wa mwanadamu? Vipi Mungu aliingia kwa mwili wake katika tumbo la bikira Maria? Kisha baadaye atokeze na kuwa hai akitokea katika tumbo la kiumbe wake, huku akiwa anawezekana kuonekana akiwa ananyonya, kukojoa na kujisaidia haja kubwa?! Je, Mungu Muumba huzaliwa kutokana na kiumbe chake ili baadaye aonekane?

9- Hajuti: ''Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute;…'' Hesabu 23:19 ''BWANA ameapa wala hataghairi, …'' Zaburi 110:4. Kwa hiyo sifa ya ''kudhihirihikiwa'' (Mungu kubadili rai yake kwa jambo linalomdhihirihikia ambalo hapo kabla halikumdhihirihikia) si sifa ya Mungu. Ni jambo lisilowezekana kwa haki ya Mungu Mtukufu kuwa na sifa za mwanadamu na kujuta kwa matendo yake? Na kupatwa na majuto kutokana na sheria alizozitunga hapo kabla? Sasa kwa nini Mungu alijuta kwa matendo yake, kama tutakavyoona katika kurasa za kitabu hiki?!

10- Hachoki wala hataabiki: ''Je! Wewe hukujua? Hukusikia? Yeye Mungu wa milele, BWANA, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki; akili zake hazichunguziki.'' Isaya 40:28. Kwa hiyo ni jambo lisilowezekana kwa haki ya Mungu mtukufu kuwa na sifa za kibinadamu na kuchoka na kuhitaji mapumziko siku ya saba!

Je, kuna upotoshaji katika maandiko ya Maagano mawili na ushahidi upo wapi? Miongoni mwa mambo yanayokubaliwa na viongozi wa dini wa Kiyahudi na Kikristo ni kuwa miswada (maandiko) ya asili imepotea. Na kwa sasa hakuna hata nakala moja iliyoandikwa kwa maandiko asilia. Na nakala zilizopo hivi sasa ni tarjuma (tafsiri ya kutoka lugha moja kwenda nyingine). Na mswada wa vitabu vyao wa kale zaidi kwao wao ni ule wa karne ya nne AD. Mtunzi wa kitabu ''Kamusi ya Biblia Takatifu'' anasema: ''kwa sasa, sisi hatuna miswada asilia ya (maagano mawili la Kale na Jipya) iliyoandikwa na waandishi asilia wa vitabu vitakatifu.'' Wayahudi na Wakristo wanaeleza sababu za kukosekana kwa miswada ya vitabu vyao vitakatifu na kutojulikana wapokezi wake. Ni kuwepo kwa matukio mengi ya kuwakandamiza na kuwatesa Wayahudi na Wakristo katika kipindi kirefu cha historia yao. Miongoni mwa matukio hayo ni vita vya Waashori dhidi yao mwaka 722 BC. Kisha vita mashuhuri vya Wababeli vya mwaka 586 BC. Vilivyopelekea kuangamizwa kwa hekalu la Wana wa Israeli na wao wenyewe kuchukuliwa mateka na kupelekwa Babeli. Kisha ukandamizaji wa Wayunani uliofuatiwa na ukandamizaji wa Warumi ulioendelea kwa karne nyingi. Ukandamizaji wote huo umepelekea kuchomwa na kuharibiwa kwa vitabu vyao, kuzuiwa kuvisoma na kuuawa kwa viongozi na wanazuoni (wasomi) wao. Na zaidi ya hayo yote, kama Biblia ni ufunuo wa Mungu, inakuwaje inaruhusiwa kufutwa na kuongezwa kitu katika Biblia, na kuyafanyia mapitio maandiko yake baina ya muda na muda mwingine pamoja na kuyatazama na kuyarekebisha tena maandiko yake?''

Ushahidi wa kuwepo upotoshaji wa Biblia[1]: Agano la Kale la sasa hivi bado lina maandiko ya kuthibitisha hilo, miongoni mwayo ni: ''Na mzigo wa BWANA hamtautaja tena; maana neno la kila mtu ndilo litakalokuwa mzigo wake; maana ninyi mmeyapotosha maneno ya Mungu aliye hai, ya BWANA wa majeshi, Mungu wetu.'' Yeremia 23:36. ''Mwasemaje, Sisi tuna akili, na torati ya

[1] Tazama maelezo katika kitabu (IDHIHARILHAKI – kudhihirisha haki) cha Sheikh Mwanachuoni: Rahmatullah Llahi Khalilul Rahmaani Al-Kayraanawiyyu Alhindiyyu.

BWANA tunayo pamoja nasi? Lakini, tazama, kalamu yenye uongo ya waandishi imeifanya kuwa uongo.'' Yeremia 8:8.

**Je, manabii wa Mungu katika Agano la Kale wamekingwa hawafanyi dhambi?**

Manabii wa Mungu katika Agano la Kale wamepachikwa mengi, mfano: Kuabudu masanamu, kufanya mauaji ya kinyama kwa watoto na wanawake, uzinzi, ukuwadi, kunywa pombe, kuchochea wizi, kuwahubiria watu dini wakiwa uchi, kukata viuno…. Na jambo linalojulikana kuwa anayetaka kuyachafua mahubiri ya dini, anapaswa akusudie kuichafua taswira ya huyo anayehubiri hiyo dini. Na upande mwingine ambao ni wa hatari sana, ni kuwa yale wanayowapachika Manabii licha ya kwamba yanatengua kukingwa kwao na maasi lakini pia yanatawanya machafu na kueneza ufisadi na kuhamasisha kufuru…. Au yanahamasisha kuitafuta dini ya kweli… Na hayo ndio yaliyotokea katika jamii za kimagharibi tangu mamia ya miaka.

| Maswali | Je, Mungu wa Agano la Kale ananasibishwa na maandiko yanayohamasisha kuwakebehi na kuondolewa kinga ya kutofanya dhambi kwa manabii wa Mungu (amani iwe juu yao) na kufuru au yanayohamasisha kuitafuta dini ya kweli? | Majibu kwa maandiko ya Agano la Kale kutoka katika Quran na Hadithi Tukufu za Mtume. |
|---|---|---|
| **Sura ya kwanza: Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa na ukahaba, uzinzi na uasherati wa kingono?** | | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni mtunzi wa hadithi zinazoamsha matamanio na hisia za kimapenzi?<br><br>Je, Maandiko yote haya ya kimapenzi na kufunua tupu (uchi), uzinzi na uasherati na machukizo yanamhamasisha | ''useme, Bwana MUNGU auambia Yerusalemu hivi;… ukaongezeka, na kuzidi kuwa mkubwa, ukapata kuwa na uzuri mno; matiti yako yakaumbwa, nywele zako zikawa zimeota; lakini ulikuwa uchi, huna nguo. Basi, nilipopita karibu nawe, nikakutazama; tazama, wakati wako ulikuwa wakati wa upendo; nikatandika upindo wa vazi langu juu yako, nikakufunika uchi wako; naam, nalikuapia, nikafanya agano nawe, asema Bwana MUNGU, … nikakufunga nguo ya kitani safi kiunoni mwako, nikakufunika kwa hariri. Nikakupamba kwa mapambo pia, nikatia vikuku mikononi mwako, na mkufu shingoni mwako… nawe ulikuwa mzuri mno… asema Bwana MUNGU. Lakini uliutumainia uzuri wako, ukafanya mambo ya kikahaba kwa sababu ya sifa zako, ukamwaga mambo yako ya kikahaba juu ya kila mtu aliyepita; …., ukajifanyia sanamu za wanaume, ukafanya mambo ya kikahaba pamoja nazo; …. Je! Mambo yako ya kikahaba ni kitu kidogo tu, hata ukawaua watoto wangu… na mambo yako | Kuwa na ''haya'' na ''stara'' ni sifa mbili za Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka. Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka ni mwenye kustahi na kustiri anapenda staha na stara…) Imepokewa na Abu Daudi na Annasaaiyyu.<br><br>Hadithi ya Salmani, Mwenyezi Mungu amuwie radhi amesema, Mtume, rehema na amani ziwe juu yake amesema: (Hakika Mola wenu ni mwenye kustahi na mkarimu, anastahi kwa mja wake, pindi anaponyanyua mikono yake kwake kumrejesha |

| | | |
|---|---|---|
| mtu awe safi na mwema?<br><br>Je, vifungu vyote hivi, (vya Kahaba wa mji wa Yerusalemu) ni vitakatifu na vinakubaliwa na mwenye akili salama kwa wake zake, watoto wake na dada zake? Je, Mungu wa Agano la Kale anamlaumu mkewe ''Yerusalemu'' kwa kuwa amemsaliti na kufanya uzinzi?! | ya kikahaba, hukuzikumbuka siku za ujana wako, ulipokuwa uchi, huna nguo, ukawa ukigaagaa katika damu yako… ukatanua miguu yako kwa kila mtu aliyepita karibu, ukaongeza mambo yako ya kikahaba. Tena umezini na Wamisri, jirani zako, wakuu wa mwili; ... haya mambo yako ya uasherati. Pia umefanya mambo ya kikahaba pamoja na Waashuri, kwa sababu ulikuwa huwezi kushibishwa; ... Jinsi moyo wako ulivyokuwa dhaifu, asema Bwana MUNGU, ikiwa unafanya mambo hayo yote, kazi ya mwanamke mzinzi, apendaye kutawala watu; ...Mke wa mtu, aziniye! Akaribishaye wageni badala ya mumewe! Watu huwapa makahaba wote zawadi, bali wewe unawapa wapenzi wako wote zawadi zako, na kuwapa rushwa ili waje kwako pande zote, kwa ajili ya mambo yako ya kikahaba. Tena, katika mambo yako ya kikahaba, wewe na wanawake wengine ni mbalimbali, …. tena kwa kuwa unatoa ujira, wala hupewi ujira; ... naam, nitawakusanya juu yako pande zote, na kuwafunulia uchi wako, wapate kuuona uchi wako wote… nao watakuvua nguo zako, na kutwaa vyombo vyako vya uzuri, nao watakuacha uchi, huna nguo." Ezekieli 16:3-39. | mikono mitupu yenye hasara). Imepokewa na Attirmidhiyyu na hili ni tamko lake, na Abu Daudi, Ahmad na Alhaakim.<br><br>32. (Na waambie wanawake waaminio kwamba wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, na wasidhihirishe uzuri wa sura zao wala mapambo yao isipokuwa yale yaliyo bayana katika hayo, na kwamba washushe shungi zao mpaka vifuani mwao, na wasionyeshe uzuri wa sura zao wala mapambo yao isipokuwa kwa waume zao, au kwa baba zao au kwa baba za waume zao, au kaka zao au wana wa kaka zao au wana wa dada zao au wanawake wenzao au wale waliomilikiwa na mikono yao ya kuume ...) An-nuur 31<br><br>(Na wanapofanya mambo ya aibu husema: Tuliwakuta baba zetu juu ya hayo na (pia) Mwenyezi Mungu Ametuamuru hayo. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu haamuru mambo mabaya. Je, mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua?) Al-A`raaf: 28<br><br>(Na kwa hakika utukufu wa Mola wetu umeinuka, Hakuchukua (hana) mke wala mwana:) Aljinn: 3 |

| | | |
|---|---|---|
| Ni akina nani hawa Ohola, na Oholiba?<br><br>Je, kisa hiki kinahamasisha wavulana na wasichana wajiheshimu?<br><br>Upo wapi utakatifu katika maandiko haya yanayoamsha hisia za kimapenzi?<br><br>Je, vifungu hivi ni vitakatifu? Je, inawezekana kwa watoto wa kiume na wakike kufanya ibada ya sala kwa kuyasoma maandiko haya? | "2 Mwanadamu, palikuwa na wanawake wawili, binti za mama mmoja; 3 nao walizini huko Misri; walizini wakati wa ujana wao; huko vifua vyao vililemewa, na huko waliyabana matiti ya ubikira wao. 4 Na majina yao, mkubwa aliitwa Ohola, na umbu lake Oholiba; wakawa wangu, wakazaa wana na binti. Na katika hayo majina yao, Samaria ni Ohola, na Yerusalemu ni Oholiba. 5 Na Ohola alifanya mambo ya kikahaba alipokuwa wangu; naye alipenda mno wapenzi wake, Waashuri, jirani zake, …Akawagawia mambo yake ya kikahaba, watu wateule wa Ashuru, wote pia; 7 … akajitia unajisi kwa vinyago vyote vya kila mmoja wa hao aliowapenda. 8 Wala hakuyaacha mambo yake ya kikahaba tangu siku za Misri, kwa maana wakati wa ujana wake walilala naye, wakayabana matiti ya ubikira wake wakamwaga uzinzi wao juu yake. 9 Kwa sababu hiyo nalimtia katika mikono ya wapenzi wake, katika mikono ya Waashuri, aliowapendelea. 10 Na hawa wakaufunua uchi wake, wakatwaa wanawe na binti zake, wakamwua yeye kwa upanga; akawa jina la aibu kati ya wanawake; kwa maana walitoa hukumu juu yake. 11 Na umbu lake, Oholiba, akayaona hayo walakini alizidi kuharibika kuliko yeye, kwa kupendelea kwake, na kwa uzinzi wake, uliokuwa mwingi kuliko uzinzi wa umbu lake… 13 Naye akaongeza uzinzi wake; 14 kwa maana aliona watu waume, ambao sura zao zimeandikwa ukutani, sura za Wakaldayo zilizoandikwa kwa rangi nyekundu; waliofungiwa mikumbuu viunoni mwao, na vilemba vilivyotiwa rangi vichwani mwao; mara alipowaona aliwapendelea, akatuma wajumbe kwao hata Ukaldayo…. 17 Na watu wa Babeli wakamwendea katika kitanda cha mapenzi, wakamtia unajisi kwa uzinzi wao, akatiwa unajisi nao, kisha roho yake ikafarakana nao. 18 Basi alifunua uzinzi wake, na kufunua uchi wake; ndipo roho yangu ikafarakana naye, kama ilivyofarakana na umbu lake. 19 Lakini aliongeza uzinzi wake, akikumbuka siku za ujana wake, alipofanya mambo ya kikahaba katika nchi ya Misri. 20 Akawapendelea wapenzi wao, ambao nyama ya mwili wao ni kama nyama ya mwili wa punda, nacho kiwatokacho ni kama kiwatokacho | {Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu, na kufanya hisani, na kuwapa jamaa (na wengineo); na anakataza uchafu na uovu, na dhulma…) Annahl 90<br><br>(Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, basi mpigeni kila mmoja wao mijeledi mia. Wala isiwashikeni kwa ajili yao huruma katika hukumu ya Mwenyezi Mungu, ikiwa ninyi mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho; na lishuhudie adhabu yao kundi la waaminio. ) An-nuur 2<br><br>Msomi wa Quran ataona kuwa, Quran imetumia maneno mazuri yaliyo mbali na uovu na uasherati, na kwamba maneno haya yanaendana na ufunuo wa dhati ya Mungu na heshima ya mwanadamu kuisikiliza na kuisoma.<br><br>Mtume, rehema na amani ziwe juu yake amesema katika hadithi iliyopokelewa na Albayhakiyu na wenginiwe: (Jiepusheni na haya mauchafu uchafu yaliyokatazwa na Allah mtukufu, atakayejua kitu chochote katika hayo, na akistiri na Allah atamstiri pia atubie kwa Allah. Hakika mambo yalivyo, atakayetudhihirishia kurasa zake, tutamsimamishia kitabu cha Allah). |

| | | |
|---|---|---|
| Au maandiko haya ni kwa wakubwa tu? | farasi. 21 ulivyokumbuka uasherati wa ujana wako, yalipobanwa matiti yako na Wamisri, kwa maziwa ya ujana wako. 22 Kwa sababu hiyo, Ewe Oholiba, Bwana MUNGU asema hivi, … 26 Pia watakuvua nguo zako na kukuondolea vyombo vyako vya uzuri. 27 Hivyo ndivyo nitakavyokomesha uasherati wako, na uzinzi wako, ulioletwa toka nchi ya Misri; usije ukawainulia macho yako, na kukumbuka Misri tena. 28 Maana BWANA Mungu asema hivi, Tazama nitakutia katika mikono yao unaowachukia… 29 nao watakutenda mambo kwa chuki, watakuondolea kazi zako zote, watakuacha uchi, huna nguo na aibu ya mambo yako ya kikahaba itafunuliwa, uasherati wako na uzinzi wako. Utatendwa mambo hayo kwa sababu umezini na hao wasioamini, na kwa sababu umetiwa unajisi kwa vinyago vyao… 35 Basi Bwana MUNGU asema hivi; kwa kuwa umenisahau, na kunitupa nyuma yako, basi kwa hiyo, uchukue uasherati wako na uzinzi wako.) Ezekieli 23:2-35 | Uzinzi ni haramu. Nao ni katika madhambi makubwa baada ya kumshirikisha Mungu. Mwenyezi Mungu mtukufu amesema: (Na wale wasiomuomba mungu mwingine pamoja na Allah, wala hawaui nafsi aliyoiharamisha Mwenyezi Mungu isipokuwa kwa haki, wala hawazini; na atakayefanya hayo atapata madhara (papa hapa ulimwenguni kabla ya akhera). Na atazidishiwa adhabu siku ya Kiama na atakaa humo kwa kufedheheka (muda mrefu kabisa) milele. Ila Yule atakayetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri; basi hao ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema; na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) mwingi wa kurehemu.) Al-Furqan 68 – 70 |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni mfuska kiasi cha kuleta ufunuo wa maandiko unaoeleza mwili wa mwanamke kimapenzi ya ngono? | "1 Siti msharifu, jinsi zilivyo nzuri Hatua zako katika mitalawanda. Mapaja yako ya mviringo ni kama johari, Kazi ya mikono ya fundi mstadi; 2 Kitovu chako ni kama bilauri iliyoviringana, Na isikose divai iliyochanganyika; Tumbo lako ni mfano wa chungu ya ngano, Iliyozungukwa na ugo wa nyinyoro; 3 Maziwa yako mawili ni kama wana-paa wawili, Ambao ni mapacha ya paa; 4 Shingo yako ni kama huo mnara wa pembe; Macho yako kama viziwa vya Heshboni, Karibu na mlango wa Beth-rabi; Pua yako ni kama mnara wa Lebanoni, Unaoelekea Dameski; 5 Kichwa chako juu yako ni kama Karmeli, Na nywele za kichwa chako kama urujuani, Mfalme amenaswa na mashungu yake. 6 Jinsi yalivyo mazuri, yalivyo matamu, Mapenzi katikati ya anasa! 7 Kimo chako | {Kwa hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu, na kufanya hisani, na kuwapa jamaa (na wengineo); na anakataza uchafu na uovu, na dhulma…) Annahl 90<br><br>Na katika Swahihi mbili, kutoka kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kwa hakika amesema: Atakayekuwa anamwamini Allah na siku ya |

| | | |
|---|---|---|
| Je, maandiko haya ni ya Kiroho au ya kimatatamanio? | kimefanana na mtende, Na maziwa yako na vichala. 8 Nilisema, Nitapanda huo mtende, Na kuyashika makuti yake. Maziwa yako na yawe kama vichala vya mzabibu, Na harufu ya pumzi yako kama mapera; 9 Na kinywa chako kama divai iliyo bora, Kwa mpendwa wangu inashuka taratibu, Ikitiririka midomoni mwao walalao. 10 Mimi ni wake mpendwa wangu, Na shauku yake ni juu yangu.'' Wimbo Ulio Bora 7:1-10 | mwisho; na aseme ya heri au anyamaze.<br><br>Kuongelea mapenzi ya kingono ni njia ya shari na muislamu anaulinda ulimi wake na kile anachokiogopea kitamletea shari. Na tiba ya matamanio ni kuoa, kama sivyo kwa kufunga na kuushughulisha moyo na yale yanayoliwaza ukiwa watu wa heri na kujiepusha na marafiki wabaya. |
| Utakatifu upo wapi katika uzinzi wa mwanamke na asiyekuwa mumewe?<br><br>Je, maandiko ya kimapenzi kuhusu | ''17 Nimetia kitanda changu manukato, Manemane na udi na mdalasini. 18 Haya, na tushibe upendo hata asubuhi, Tujifurahishe nafsi zetu kwa mahaba. 19 <u>Maana mume wangu hayumo nyumbani,</u> Amekwenda safari ya mbali; 21 Amechukua mfuko wa fedha mkononi; Atarudi wakati wa mwezi mpevu. Kwa maneno yake mengi na ulaini akamshawishi, Kwa ubembelezi wa midomo yake akamshinda.'' Mithali 7:17-21.<br><br>''Kwa sababu ya <u>wingi wa ukahaba wa yule kahaba</u> mzuri, yule bibi wa mambo ya uchawi, auzaye mataifa kwa ukahaba wake… Nami nitafunua marinda yako mbele ya uso wako; nami nitawaonyesha mataifa <u>uchi wako, na falme aibu yako.</u>'' Nahumu 3:4-5<br>''… Nawe ukisema moyoni mwako, Mbona mambo haya yamenipata mimi? Ni kwa sababu ya wingi wa <u>uovu wako</u>, marinda yako yamefunuliwa, na visigino vya miguu yako vimeumia.'' Yeremia 13: 22,<br>''Mpendwa wangu ni kama mfuko wa manemane. Ukilazwa usiku maziwani mwangu. Wimbo Ulio Bora 1:13. ''Maziwa yako mawili ni kama wana-paa wawili…) Wimbo Ulio Bora 1:13. Nyuma ya barakoa yako. Ambao ni mapacha ya paa; Wakilisha penye nyinyoro. Wimbo Ulio Bora 4:5.<br>''Ni ayala apendaye na paa apendezaye;<br><br>Maziwa yake yakutoshe sikuzote; Na kwa upendo wake ushangilie daima.'' Mithali 5:19. | (Mwanamume mzinifu hafungamani ila na mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina, na mwanamke mzinifu hafungamani naye mwanamume mzinifu au mshirikina, na hayo yameharamishwa kwa Waislamu) An-nur 3<br><br>(… wala msifuate nyayo za shetani (yale anayokuamrisheni). Bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri.) Al Baqarah 168.<br><br>(Yeye anakuamrisheni (kufanya) mambo mabaya na machafu, na mumsingizie Mwenyezi Mungu msiyoyajua (yakini yake kuwa kweli kasema hayo au hakusema). Al Baqarah 168. |

| | | |
|---|---|---|
| wanawake wazinzi ni maneno ya Mungu?<br><br>Utakatifu upo wapi katika kuelezea matiti ya wanawake na kuamsha hisia za wanaume? | ''Kwetu sisi tuna umbu mdogo, Wala hana maziwa; Tumfanyieje umbu letu, Siku atakapoposwa? Wimbo Ulio Bora 8:8<br>''Mimi nalikuwa ukuta, Na maziwa yangu kama minara...'' Wimbo Ulio Bora 8:10,<br><br>(… Nao wamejikinga kwa kujipangusa chini ya matiti yao…) 2 Maccabees 3:19 | |
| Utakatifu upo wapi katika zinaa ya Wana wa Israeli wana wa Mungu wa Agano la Kale? | ''… binti zao wakaenda kufanya uzinzi na miungu yao, wakawavuta wana wenu wafanye uzinzi na miungu yao.'' Kutoka 34:16,<br><br>''… Mke wako atakuwa kahaba mjini, ...'' Amosi 7:17<br><br>''… nao Israeli wote wakaenda na kuiandama kwa ukahaba huko...'' Waamuzi 8:27 | (Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (ulimwenguni) mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu… ) Al-Imran: 110 |
| Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa matamanio kwa vimwana…?<br><br>Utakatifu na maadili yapo wapi katika zinaa iliyohalalishwa na kula njama? | Zaburi 45:8-12, ''Mavazi yako yote hunukia manemane<br><br>Na udi na mdalasini… Sikia, binti, utazame, utege sikio lako, Uwasahau watu wako na nyumba ya baba yako. Naye mfalme atautamani uzuri wako…''<br>2 Samweli 11:2-27, ''Ikawa wakati wa jioni, Daudi akaondoka kitandani, akatembea juu ya dari ya jumba la mfalme; na alipokuwa juu ya dari aliona mwanamke anaoga; naye huyo mwanamke alikuwa mzuri sana, wa kupendeza macho. Naye Daudi akapeleka, akauliza habari za yule mwanamke. Mtu mmoja akasema, Je! Huyu siye Bath-sheba, binti Eliamu, mkewe Uria, Mhiti? Basi Daudi akapeleka | (Sema: ''Wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo hawatafaulu). Yunus: 69.<br><br>Nabii wa Mungu, Daudi amani iwe juu yake amesifika kuwa ni mwelekevu sana na mwenye hekima na elimu.<br><br>(Subiri juu ya hayo wanayoyasema, na umkumbuke Mja wetu Daudi |

| | | |
|---|---|---|
| Je, ni miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale kuhamasisha uzinzi (Huyo mzinzi jina lake ni Bath-sheba bibi yake ''Yesu'' ambaye ni nafsi ya pili ya Mungu? | wajumbe, akamtwaa; naye akaingia kwake; naye akalala naye; (maana yule mwanamke amekwisha kutakasika unajisi wake); kisha akarudi nyumbani kwake. Yule mwanamke akachukua mimba; basi akapeleka na kumwambia Daudi, akasema, Ni mja-mzito… Daudi Apanga Uria Auliwe. Hata ikawa asubuhi, Daudi akamwandikia Yoabu waraka, akaupeleka kwa mkono wa Uria. Akaandika katika waraka huo, kusema, Mwekeni Uria mbele ya watu penye vita vikali, kisha ondokeni, mmwache, ili apigwe akafe… Uria Mhiti naye akafa. Ndipo Yoabu akapeleka na kumwarifu Daudi habari zote za vita… Daudi akatuma mtu, akamtwaa, akamtia nyumbani mwake; naye akawa mkewe, akamzalia mwana.<br><br>Swali la kutafakari: Je, mzinzi Bath-sheba alibeba mimba ya Daudi mara tu baada ya kulala naye kimapenzi (kuzini naye) kwa mara ya kwanza?! | mwenye nguvu (katika kuendesha Utume na ufalme); Kwa yakini yeye alikuwa mwingi wa kutubia.) (Sad: 17)<br><br>(Na kwa hakika, Tulimpa Daudi fadhila kubwa kutoka Kwetu. (Tuliyaamrisha majabali yawe yanaitikia dua za Ibadaye. Tukayaambia): - ''Enyi milima! Rejezeni sautiye, na (nyie) ndege (pia).''… Saba: 10<br><br>(Basi (hao watu wa Taluti) wakawaendesha mbio (hao maadui zao) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu: na Daudi akamwua Jaluti, na Mwenyezi Mungu akampa (huyo Daudi) ufalme na hikima (utume) na kumfundisha aliyoyapenda…) Al-Baqarah: 251. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale amekifanya kizazi cha Daudi ni kirusi/mzizi, ijulikane kuwa nafsi ya pili ya Mungu yaani ''Yesu'' anatokana na kizazi cha Daudi? | ''lakini BWANA haachi rehema zake… amempa Yakobo mabaki na kwa Daudi kirusi/mzizi...'' Sira 47:22-24<br><br><u>Andiko hili linafunua kwamba hakuna toba kwa Daudi kwa sababu kitabu cha Yoshua bin Siirakh kiliandikwa mwaka 180 kabla ya kuzaliwa Kristo, yaani baada ya kuandikwa Zaburi.</u><br><br>Daudi aliwalaani wana wa Israeli hivyo mji wa Yerusalemu ukaharibiwa kwa mara ya kwanza na wana wa Israeli wakatekwa na kupelekwa Babeli. Je, wana wa Israeli walitaka kulipa kisasi kwa Daudi kwa kumpora Unabii wake na kuichafua historia yake kwa kumpachika visa vya mapenzi? | (Daudi amani iwe juu yake amewalaani wana wa Israeli. (Wamelaaniwa wale waliokufuru miongoni mwa wana wa Israeli kwa ulimi wa Daudi na wa Isa bin Mariam. Hayo ni kwa sababu waliasi nao walikuwa wakiruka mipaka.) Almaaidah 78 |
| Utakatifu upo wapi kwa Daudi | ''Mfalme Daudi alikuwa mzee, mkongwe katika siku zake, nao wakamfunika nguo, lakini asipate joto. | Nabii wa Mungu, Daudi amani iwe juu yake alikuwa |

| | | |
|---|---|---|
| kujipa joto kwa vibikra na kulala na vibikra viwili ili ajipatie joto? | Kwa hiyo watumishi wake wakamwambia, Bwana wangu mfalme na atafutiwe kijana mwanamwali; naye asimame mbele ya mfalme, amtunze; alale kifuani mwako, ili bwana wangu mfalme apate moto...'' 1 Wafalme 1:1-3<br><br>''Tena, wawili wakilala pamoja, hapo watapata moto; lakini mmoja aliye peke yake tu awezaje kuona moto?'' Muhubiri 4:11. | anadumisha kumtukuza Mwenyezi Mungu<br><br>(… na Tukatiisha pamoja na Daudi milima, ikitukuza na ndege pia..) Al-Anbiyaa: 79.<br><br>(Hakika sisi Tuliitiisha milima kwake. Wakasherehekea kumtukuza Mwenyezi Mungu pamoja naye jioni na asubuhi.) Saad: 18. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kukiadhibu kizazi cha Kanaani (bila ya kutenda dhambi) ila kwa sababu ya kulewa na kukaa uchi kwa Nuhu? | ''Akanywa divai, akalewa; akawa uchi katika hema yake. Hamu, baba wa Kanaani, akauona uchi wa baba yake...'' Mwanzo 9:21-22.<br><br>''Nuhu akalevuka katika ulevi wake... Akasema, Na alaaniwe Kanaani; Atakuwa mtumwa kabisa kwa ndugu zake.'' Mwanzo 9:24-25. | (Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adam na Nuhu...) Aali Imran 33<br><br>(Na pia akawaambia) ''Enyi kizazi cha wale tuliowapandisha (katika jahazi) Nuhu! (kuweni wenye shukrani kama mzee wenu huyo). Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani.) Bani Israil 3 |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwafunulia manabii "wanaokaa uchi" kwa muda wa miaka mitatu?<br><br>Je, manabii wanatumikia unabii wao wakiwa uchi mbele za watu?! | [2] '... Haya, uvue nguo ya magunia viunoni mwako, na viatu vyako miguuni mwako.'' [3]Naye akafanya hivyo akaenda uchi, miguu yake haina viatu. BWANA akasema, Kama vile mtumishi wangu Isaya anavyokwenda uchi, hana viatu, awe ishara na ajabu kwa muda wa miaka mitatu...'' Isaya 20:2-4.<br><br>''[24]Naye akavua nguo zake, akatabiri mbele ya Samweli, akalala uchi mchana kutwa na usiku kucha siku ile. Kwa hiyo watu husema, Je! Sauli pia yumo miongoni mwa manabii?'' 1 Samweli 19:24<br><br>''[8]... Nitakwenda nimevua nguo, ni uchi...'' Mika 1:8 | (Waambie Waislamu wanaume wainamishe macho yao (wasitazame yaliyokatazwa), na wazilinde tupu zao, hili ni takaso kwao, bila shaka Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) wanayoyafanya.) Annur 30 |
| Utakatifu upo wapi katika kukisema vibaya kisa cha Lutu na | **<u>Walikuwa mabikra wawili:</u>** ''[8]Tazama, ninao binti wawili ambao hawajajua mtu mume, nawasihi nitawatolea kwenu mkawafanyie vilivyo vyema machoni penu, ila watu hawa msiwatende neno, | Nabii wa Mungu Lutu amani iwe juu yake amesema: ''Hawa ni mabinti zangu'' na hakusema ''hawa wawili ni mabinti zangu |

| | | |
|---|---|---|
| kumuonesha yeye kama mtu ''hanithi'' na ''kuwadi'' kwa mabinti zake wawili? | kwa kuwa wamekuja chini ya dari yangu.'' Mwanzo 19:8<br><br>**<u>Walikuwa wakweze walioposwa:</u>** ''[14]Lutu akatoka akasema na wakweze, waliowaposa binti zake, akasema, Ondokeni mtoke katika mahali hapa kwa sababu BWANA atauharibu mji huu. Lakini akawa kama achezaye machoni pa wakweze.'' Mwanzo 19:14<br><br>Je, mabinti wawili wa Lutu walikuwa mabikra au washaolewa (Lutu aliongea na wakweze)? | wa kuwazaa''. Yeye Lutu anakusudia kuwa wanawake wa kaumu yake ni watoto zake'' huku akiwaongoza watu wake waende kwa wanawake wao. (… akasema (Lut) Enyi kaumu yangu! Hao binti zangu (binti za umma wangu walioolewa katika nyumba zenu) ndio wametakasika kwenu …) Hud 78 |
| Utukufu upo wapi katika uzinzi wa ndugu kwa ndugu, Lutu na binti zake wawili wa kuwazaa?<br><br>Je, maandiko haya yanahamasisha wasichana wajistiri?<br><br>Je, pombe inaondoa akili hadi kufikia kutotambua kitu? | ''[33]Wakamnywesha baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka huyo <u>mkubwa akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka</u>… [35]Wakamnywesha tena baba yao mvinyo usiku ule, <u>akaondoka mdogo akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka</u>. [36]Basi hao binti wote wawili wa Lutu wakapata mimba kwa baba yao. [37]Yule mkubwa akazaa mwana, akamwita jina lake Moabu; huyo ndiye baba wa Wamoabi, hata leo. [38]Na yule mdogo naye akazaa mwana akamwita jina lake Benami; huyo ndiye baba wa Waamoni hata leo.'' Mwanzo 19:33-38<br><br>Swali la kutafakuri: Je, mabinti wawili wa Lutu wali beba mimba mubashara kutoka kwa baba yao mara t u baada ya kulala naye kingono kwa mara ya kwanza (uzinzi wa ndugu kwa ndugu)?! | Nabii Luti amani iwe juu yake alikuwa mwenye hikima na mjuzi (Na Luti tukampa hukumu na ilimu na tukamuokoa na (watu wa) ule mji uliokuwa ukifanya maovu. Bila shaka wao walikuwa watu wabaya wavunja amri) Al-Anbiyaa 74.<br><br>Kutoka kwa Abu Hurayra Mungu amuwie radhi. Mtume wa Allah, rehema na amani ziwe juu yake amesema: ''Rehema za Allah ziwe kwa Luti. Kama ingewezekana Angelikuwa ni mwenye kutegemea katika nguzo imara…'' Jaamiu Attirmidhiy. |
| Utukufu upo wapi katika hadaa ya Yakubu ili azini na Lea kisha kuzaa naye badala ya kumuoa Raheli ambaye | ''[20]Yakobo akatumika miaka saba… [21]Yakobo akamwambia Labani, Nipe mke wangu, maana siku zangu zimetimia; niingie kwake… [23]Ikawa wakati wa jioni akamtwaa Lea, binti yake, akamletea Yakobo, naye akaingia kwake… [25]Ikawa, kulipokuwa asubuhi, kumbe! Ni Lea. Akamwambia Labani, Nini hii uliyonitenda? [26] Sikukutumikia kwa | Kutoka kwa Abdallah bin Omar Mungu amuwie radhi yeye na baba yake, kutoka kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Mtukufu mtoto wa Mtukufu mtoto wa Mtukufu mtoto wa Mtukufu Yusufu mtoto wa Yakubu mtoto wa Is- |

| | | |
|---|---|---|
| amemtumikia ili amuoe? | Raheli? Mbona umenidanganya?...'' Mwanzo 29:20-26 | haka mtoto wa Ibrahimu) Sahihi Bukhariyu 4688. |
| Utukufu upo wapi katika kuelezea mahusiano ya kimapenzi baina ya (Onani na Thaamar) (bibi yake ''Yesu'' ambaye ni Nafsi ya pili ya Mungu)? | ''[8]Yuda akamwambia Onani, Uingie kwa mke wa nduguyo, ukamwoe, ukamwinulie nduguyo uzao. [9]Onani alijua ya kwamba huo uzao hautakuwa wake, ikawa, alipoingia kwa mke wa nduguye, akamwagia chini asimpe nduguye uzao.'' Mwanzo 38:8-9.<br><br>Swali: ni nini maoni yako kwa binti yako mdogo akakuuliza kwa nia njema ... ee baba ... nini maana ya akamwagia chini asimpe nduguye uzao? | Kutoka kwa Abuu Dhari Mungu amuwie radhi, hakika Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: [''... na katika uke wa mmoja wenu kuna kutoa sadaka'' wakamuuliza: Ewe Mtume wa Allah. Je, mmoja wetu atayaendea matamanio yake kisha anapata malipo katika hilo? Akajibu: ''Mwaonaje lau kama angeyapeleka katika haramu, je, angepata dhambi kwa hilo? Basi hivyo hivyo kama atayapeleka katika halali atapata malipo.} Sahihi Muslim 1748. |
| Utukufu upo wapi katika kuhamasisha wajane wafanya zinaa? Kwa nini Yuda hakutekeleza (sheria ya Ibrahimu) ya adhabu ya zinaa ni ''kujichoma'' yeye mwenyewe? Badala ya kuitekeleza adhabu ya zinaa kwa (Tamari) tu (bibi yake ''Yesu'' Nafsi ya pili ya Mungu)?<br><br>''Mtoeni tumchome'' | ''[14]Basi akavua nguo za ujane wake, akajivika utaji, akajifunika uso, akakaa mlangoni pa Enaimu, karibu na njia ya kuendea Timna... [15]Yuda alipomwona alimdhania kuwa ni kahaba, maana amejifunika uso. [16]Akamgeukia kando ya njia, akasema, Niruhusu niingie kwako. Maana hakujua ya kuwa ni mkwewe. Akamwuliza, Utanipa nini, ukiingia kwangu? [17]Akasema, Nitakuletea... Basi akampa, akaingia kwake, naye akapata mimba. [19]Akaondoka, akaenda zake, akavua utaji wake, na kuvaa mavazi ya ujane wake... [24]Ikawa baada ya miezi mitatu Yuda akapewa habari kwamba, Mkweo, Tamari, amefanya uzinifu, naye ana mimba ya haramu. Yuda akasema, Mtoeni ateketezwe. [26]Yuda akafikiri, akasema, Yeye ni mwenye haki kuliko mimi, kwa kuwa sikumpa Shela, mwanangu...) Mwanzo 38:14-26<br><br>Swali la tafakuri: je, Tamari mzinifu alipata mimba palepale alipolala kingono (alipozini) kwa mara ya kwanza na Yuda!!!? | (... wala hawazini; na atakayefanya, atapata madhara (papa hapa ulimwenguni kabla ya akhera). Al-Furaqan 68.<br><br>Uzinzi ni haramu, nao ni katika madhambi makubwa baada ya kushirikisha Mungu.<br><br>Kutoka kwa Abdallah bin Masuud Mungu amuwie radhi amesema: Nilimuuliza Mtume wa Allah, rehema na amani ziwe juu yake: Ni dhambi ipi kubwa zaidi kwa Allah? Akasema: ni kumfanya Mwenyezi Mungu ana mshirika na hali ya kuwa amekuumba. Akamuuliza kisha ipi? Akasema: ni kumuua mtoto wako kwa kuogopea atakula na wewe. Nakamuuliza kisha ipi? Akasema: kuzini ni mke wa jirani yako. Bukhariyu na Muslim. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Daudi alitekeleza adhabu ya kumpiga mawe mzinzi kwa mtoto wake Absalomu? | ''Basi wakamtandikia Absalomu hema juu ya nyumba darini; naye Absalomu akaingia kwa Masuria ya babaye machoni pa Israeli wote.'' 2 Samweli 16:22<br><br>Swali: Je, kuzini na mtu ambaye haruhusiwi kumwoa ni halali kwa wana wa Daudi? | Wala msiwaoe wake waliowaoa baba zenu; isipokuwa yale yaliyokwishapita (yaliyopita yamepita yasirejeshwe tena). Bila shaka jambo hili ni uovu na uchukizo na ni njia mbaya…) Annisaa 22-23 |
| Je, Yakobo alitekeleza adhabu ya kumpiga mawe mzinzi kwa mtoto wake Reubeni? | ''… kwa sababu ulikipanda kitanda cha baba yako, ukakitia unajisi; alikipandia kitanda changu.'' Mwanzo 49:4<br><br>Swali: Je, kuzini na mtu wa haramu kwa kumuoa ni halali kwa wana wa Yakubu? | Na katika Sunani Abuu Daudi na Ibnu Maajah katika hadithi ya Ibnu Abbas amesema: Mtume wa Allah, rehema na amani ziwe juu yake amesema: (Atakayemwingilia ndugu ambaye ni haramu kumuoa mueni). |
| Je, Daudi alitekeleza adhabu ya kumpiga mawe mzinzi (zinaa ya ndugu wa haramu kuoana) kwa mtoto wake Amnoni? Zi wapi haki za mwanamke? | ''[9]… Naye Amnoni akasema, Toeni watu wote kwangu. Wakatoka kila mtu kwake. [10]Amnoni akamwambia Tamari, Kilete chakula chumbani, nipate kula mkononi mwako. Basi Tamari akaitwaa mikate aliyoifanyiza, akamletea Amnoni nduguye mle chumbani. [11]Naye alipokwisha kuileta karibu naye, ili ale, Amnoni akamkamata, akamwambia, Njoo ulale nami, ndugu yangu. [12]Naye akamjibu, La, sivyo, ndugu yangu, usinitenze nguvu; kwani haifai kutendeka hivi katika Israeli; usitende upumbavu huu… [14]Walakini yeye hakukubali kusikiliza sauti yake; naye akiwa na nguvu kuliko yeye, akamtenza nguvu, akalala naye.'' 2 Samweli 13:9-14<br><br>Swali: je, kumbaka dada ni halali kwa watoto wa Daudi? | Kuhusu adhabu ya uzinzi kwa ndugu wanaofaa kuoana, imekuja hadithi kutoka kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake ikieleza kuuawa kwa mtu anayezini na nduguye wa haramu kumuoa miongoni mwa ndugu zake. Na hilo ni kwa sababu lenyewe ni uchafu mkubwa. Katika riwaya iliyopokewa na Ahmad, na hadithi hii ni sahihi. Hakika (Atakayezini na ndugu wa haramu kuwaoa atauawa hata kama atakuwa hajawahi kuoa au kuolewa). |
| Je, Ibrahimu amevunja sheria na kuoa ndugu yake? | ''Naye kweli ni ndugu yangu, binti wa baba yangu ila siye mwana wa mama yangu, ndipo akawa mke wangu.'' Mwanzo 20:12 | Sara hakuwa ndugu wa Ibrahimu, amani iwe juu yake. (Tazama sahihi Muslim hadithi namba 2371). (Na nani atajitenga na mila ya Ibrahimu (kaichukia dini hii ya kati na kati, isipokuwa ni yule mpumbavu? Na kwa yakini sisi tulimchagua |

| | | |
|---|---|---|
| | Sheria, maamrisho na mambo ya lazima kwa Nabii wa Mungu Ibrahimu, amani iwejuu yake tazama: (Mwanzo 26:5) na (Mwanzo 18:19) | (Ibrahimu) katika dunia; na kwa hakika yeye katika akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (kabisa). Al-Baqarah 130 |
| Utakatifu upo wapi katika kumbaka Dina? Zi wapi haki za mwanamke? | ''Basi Dina binti, Lea, ambaye Lea alimzalia Yakobo, akatoka kuwaona binti za nchi. 2 Shekemu, mwana wa Hamori, Mhivi, mkuu wa nchi, akamwona akamtwaa, akalala naye, akambikiri.'' Mwanzo 34:1-2 | (Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kiabisa). Bani Israil 32 |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anatoa ufunuo wa kuwa Suleiman alikuwa ni mtu ''mpenda kuoaoa'' kwa kuwa alioa wake elfu moja! Na kuwa Suleiman alikuwa mshirikina uzeeni kwake? | ''[1]Mfalme Sulemani akawapenda wanawake wengi wageni, pamoja na binti yake Farao, wanawake wa Wamoabi, na wa Waamoni, na wa Waedomi, na wa Wasidoni, na wa Wahiti, [2]na wa mataifa BWANA aliyowaambia wana wa Israeli, Msiingie kwao, wala wasiingie kwenu; kwa kuwa hakika wataigeuza mioyo yenu kuifuata miungu yao. Sulemani akaambatana nao kwa kuwapenda. [3] Akawa na wake mia saba binti za kifalme, na masuria mia tatu; nao wakeze wakamgeuza moyo. [4]Maana ikawa, Sulemani alipokuwa mzee, wake zake wakamgeuza moyo wake, afuate miungu mingine, wala moyo wake haukuwa mkamilifu kwa BWANA, Mungu wake, kama moyo wa Daudi baba yake.'' 1 Wafalme 11:1-4 | (Wakafuata yale yaliyoyafuata mashetani, (wakadai kuwa yalikuwa) yalikuwa katika ufalme wa (Nabii) Suleiman; na Suleiman hakukufuru, bali mashetani ndio yaliyokufuru, wakiwafundisha watu uchawi…) Al-Baqarah 102 |
| Utakatifu upo wapi katika suala la Suleiman kuinamisha paja lake kwa wanawake? | ''Umeinamisha mapaja yako kwa wanawake, wakautawala mwili wako...'' Sira 47:19-21<br><br>Swali: Je, kuna andiko la waziwazi katika Agano Jipya linaloharamisha kuoa mitala (wake zaidi ya mmoja)? | (Na bila shaka tuliwapa Daudi na Suleimani ilimu (kubwa kabisa na wakamshukuru Mwenyezi Mungu) wakasema: "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu. (Tanamshukuru Mwenyezi Mungu aliyetufadhilisha kuliko wengine katika waja wake waliomuamini). Annaml 15 |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kufunua tupu za wanawake na kuwatumbukiza | ''[2] … wala mimi si mume wake; na ayawekee mbali mambo ya uasherati wake yasiwe mbele ya uso wake, na mambo ya uzinzi wake yasiwe kati ya maziwa yake; [3]nisije nikamvua nguo zake akawa uchi, … [4]naam, sitawaonea rehema watoto wake; kwa maana ni watoto wa uzinzi. [5]Maana mama yao | Binadamu ameumbwa kuwa na tabia ya kujistiri, kama ilivyokuja katika kisa cha Adam na mkewe: (Basi akawateka (wote wawili) kwa khadaa (yake). Na walipouonja mti ule, aibu zao ziliwadhihirika na wakaingia |

| | | |
|---|---|---|
| watu katika uzinzi? | amezini; yeye aliyewachukua mimba ametenda mambo ya aibu;...'' Hosea 2:2-5<br><br>''[10]Na sasa nitaifunua aibu yake ....'' Hosea 2:10<br><br>''[17]Basi, kwa hiyo, Bwana atawapiga binti za Sayuni kwa pele za utosini, na BWANA ataifunua aibu yao.'' Isaya 3:17<br><br>''[2]… Vua utaji wako, ondoa mavazi yako, Funua mguu wako, pita katika mito ya maji. [3]Uchi wako utafunuliwa, Naam, aibu yako itaonekana. Nitalipa kisasi; simkubali mtu ye yote.'' Isaya 47:2-3 | kujibandika majani ya (miti ya huko) Peponi. Na Mola wao akawaita (akawaambia) "Je, sikukukatazeni mti huu na kukwambieni ya kwamba shetani ni adui yenu aliyedhahiri?'' Al-Aarafu 22.<br><br>(Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kiabisa). Bani Israil 32<br><br>Muslim amepokea kutoka kwa mtume wa Allah rehema na amani ziwe juu yake amesema: "Mwanamume asitazame uchi wa mwanamume mwingine, na mwanamke asitazame uchi wa mwanamke mwingine'' |
| Utakatifu upo wapi kwa Hosea kuwaoa wazinifu? | ''[2]… BWANA alimwambia Hosea, Enenda ukatwae mke wa uzinzi, na watoto wa uzinzi; kwa maana nchi hii inafanya uzinzi mwingi, ...'' Hosea 1:2<br><br>''[1]… Enenda tena, mpende mwanamke apendwaye na rafiki yake, naye ni mzinzi; kama vile BWANA awapendavyo wana wa Israeli...'' Hosea 3:1 | (Enyi wake wa Mtume! Atakayefanya maovu dhahiri miongoni mwenu, atazidishiwa adhabu mara mbili...) Al-Ahzab 30. |
| Utakatifu upo wapi katika kutowaadhibu wanawake wazinifu? | ''[14]Sitawaadhibu binti zenu wazinipo, wala bibi arusi zenu wafanyapo uasherati; maana wao wenyewe huenda kando pamoja na wanawake wazinzi, hutoa dhabihu pamoja na makahaba; na watu hawa wasiofahamu wataangamia.'' Hosea 4:14 | (Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kiabisa). Bani Israil 32 |
| Utakatifu upo wapi katika kisa cha Ruthu kulala na (bibi wa ''Yesu'' Nafsi ya pili ya Mungu)? | ''[1]Kisha Naomi akamwambia mkwewe… [3]Basi wewe oga, ujipake mafuta ujivike mavazi yako… [4]Nayo itakuwa wakati atakapolala, utapaangalia mahali alalapo, nawe uingie, uifunue miguu yake ujilaze hapo; na yeye atakuambia utakalofanya. [5]Akamwambia, Hayo yote unenayo mimi nitayafanya.'' Ruthu 3:1-5 | (Sema (umwambie): ''Mola wangu ameharamisha (Haya: Ameharamisha) mambo machafu, yaliyodhihirika na yaliyofichika, na dhambi na kutoka katika taa (ya wakubwa) pasipo haki…) Al-Aaraf 33 |
| Je, miongoni mwa sifa za | ''[11]BWANA asema hivi, Angalia, nitakuondokeshea uovu katika nyumba yako, nami nitawatwaa wake | (Na (makafiri) wanapofanya mambo machafu husema: |

| | | |
|---|---|---|
| Mungu wa Agano la Kale ni kutoa adhabu kwa mkosa na adhabu yake iwe ni kufanya uzinzi? | zako mbele ya macho yako, na kumpa jirani yako, naye atalala na wake zako mbele ya jua hili.,.'' 2 Samweli 12:11-12<br><br>''[15]Lakini itakuwa usipotaka kuisikiza sauti ya BWANA, Mungu wako… [30]Utaposa mke na mume mwingine atalala naye; ….'' Kumbukumbu la Torati 28:15-30 | "Tumewakuta nayo baba zetu (na) pia Mwenyezi Mungu ametuamrisha hayo." Sema: Mwenyezi Mungu haamrishi mambo mabaya. Mnasema juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua?) Al-Aaraf 28. |
| Utakatifu upo wapi katika kulala na mjakazi je, huu sio uzinzi? | ''[20]Tena mtu ye yote alalaye na mwanamke aliye mjakazi, naye ameposwa na mume, wala hakukombolewa kwa lo lote, wala hakupewa uhuru; wataadhibiwa; hawatauawa, kwa sababu huyo mwanamke hakuwa huru.'' Mambo ya Walawi 19:20 | (Shetani anakuogopesheni ufukara na anakuamrisheni ubakhili; na Mwenyezi Mungu anakuahidini msamaha utokao kwake na ihsani (kubwa pindi mkitoa); na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa mkubwa na mwenye kujua.) Al-Baqarah 268. |
| Utakatifu upo wapi katika kufunua tando za bikra za wasichana mia nne, na mabikira thelathini na mbili elfu? | ''[12]Nao wakapata katika wenyeji wa Yabesh-gileadi wanawali mia nne, ambao hawajamjua mtu mume kwa kulala naye; ...'' Waamuzi 21:12-14<br><br>''[18]Lakini hao watoto wote wa kike ambao hawakumjua mume kwa kulala pamoja naye, mtawaweka hai kwa ajili yenu.'' Hesabu 31:18<br><br>''[35]tena wanadamu jumla yao ilikuwa thelathini na mbili elfu, katika hao wanawake ambao hawakumjua mume kwa kulala pamoja naye.'' Hesabu 31:35 | (Je, tuwajaalie wale walioamini na kutenda mema kuwa sawa na wafanyao uharibifu katika ardhi? Au tuwajalie watawa (wacha Mungu) kuwa sawa na waovu? (Hatufanyi sisi hivyo). Sad 28<br><br>Kutoka kwa Abuu Huraira, kutoka kwa Mtume Rehema na amani ziwe juu yake amesema: (Allah hatomstiri mja duniani isipokuwa pia atamstiri siku ya kiama). Muslim 2590. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu ni kutoa ufunuo wa kueleza hatua za kuoa mateka na kuwadhalilisha kwa kuwanyoa vichwa? | ''[11]ukaona kati ya mateka mwanamke mzuri, ukafanya tamaa kwake, ukawaza kumtwaa kuwa mkeo; [12]ndipo umchukue kwenu nyumbani kwako, naye atanyoa kichwa, akate na kucha; [13]avue na mavazi ya uteka wake akae nyumbani mwako, awakalie matanga babaye na mamaye mwezi mzima, kisha uingie kwake uwe mumewe, naye awe mkeo. [14]Tena utakapokuwa huna furaha naye, mpe ruhusa aende atakako; lakini usimwuze | (Na ambao wanahifadhi tupu zao. Isipokuwa kwa wake zao au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, basi hao hawalaumiwi). Al-Maarij 29-30 |

| | | |
|---|---|---|
| | kabisa kwa fedha, usimfanye kama mtumwa, kwa kuwa ulimtweza.'' Kumbukumbu la Torati 21:11-14 | |
| Utakatifu upo wapi katika kuwatongoza na kulala na mabinti? Zipo wapi haki za mwanamke? | ''[28]Mtu mume akimwona kijana aliye mwanamwali ambaye hajaposwa, akamshika na kulala naye, wakaonekana; [29]yule mtu mume aliyelala naye na ampe baba yake yule kijana shekeli hamsini za fedha, kisha na awe mkewe, kwa kuwa amemtweza; hana ruhusa ya kumwacha siku zake zote.'' Kumbukumbu la Torati 22:28-29<br><br>''[16]Mtu akimshawishi mwanamwali, aliyeposwa na mume, na kulala naye, lazima atatoa mahari kwa ajili yake ili awe mkewe. [17]Ikiwa baba yake huyo mwanamwali akataa kabisa kumpa, atalipa fedha kama hesabu ya mahari ya mwanamwali ilivyo.'' Kutoka 22:16-17 | Mbakaji akimuoa muhanga wake aliyembaka! Hilo linajulisha uvunjifu wa maumbile ya utu na kasoro za kiakili upungufu wa kufuata taratibu za dini au kukosekana kwa dini. Hasahasa maumivu ya kubakwa hayaondoshwi kwa masiku wala hayafutwi na zama. |
| Je, kutekanyara wanawake ni ufunuo?<br><br>Utakatifu upo wapi katika kuutusi uchi wa mama? | ''[21]… nanyi kila mtu na amshike mkewe katika hao binti za Shilo...'' Waamuzi 21:21<br><br>---<br><br>''[30]… akamwambia, Wewe, mwana wa mke mkaidi, asi, je! Mimi sijui ya kuwa umemchagua huyo mwana wa Yese, kwa aibu yako mwenyewe, na kwa aibu ya uchi wa mama yako.'' 1 Samweli 20:30<br><br>''[5] … nami nitamwangamiza mama yako.'' Hosea 4:5 | (Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao; huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane kwa majina mabaya (ya kejeli): Jina baya kabisa kuambiwa mtu ni asi baada ya kuwa ni muislamu. (Na kufanya hayo ni uasi) na wasiotubu, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao). Al**h**ujurat : 11 |
| Utakatifu upo wapi katika kisa cha mwanamume asiye na wivu miongoni mwa WALAWI alieilinda nafsi yake dhidi ya Waisraeli kwa | ''[22]Hapo walipokuwa wakifurahisha mioyo yao, tazama, watu wa mji huo, watu mabaradhuli wakaizingira hiyo nyumba pande zote, wakagonga mlango; wakasema na huyo mwenye nyumba, huyo mzee, na kumwambia, Mlete nje mtu yule aliyefika nyumbani kwako, ili tupate kumjua. [23]Naye mtu mwenye nyumba akawatokea hapo nje, na kuwaambia, La, sivyo, ndugu zangu nawasihi msifanye uovu jinsi hii; kwa kuwa mtu huyu ameingia ndani ya nyumba yangu, msifanye | Dayuthi ni mtu ambaye hana wivu kwa mkewe. Kwa hiyo wivu wa mwanamume kwa mkewe na wanawake wa familia yake ni jambo zuri. Na ni alama ya ukamilifu wa urijali (uanaume) na heshima. Na kuacha wivu ni udayuthi (uhanithi) unaolaaniwa kisheria na kimaumbile. Na hili ndilo |

| | | |
|---|---|---|
| kumtoa mkewe adhalilishwe na kuziniwa usiku kucha kisha asubuhi akamchinja huyo mkewe vipande 12? | upumbavu huu. [24]Tazama, binti yangu yupo hapa, ni mwanamwali, na suria wake huyo mtu; nitawaleta hapa nje sasa nanyi watwezeni, na kuwatenda hayo myaonayo kuwa ni mema; lakini mtu huyu msimtende jambo la upumbavu namna hii. [25]… akamshika suria wake, na kumleta nje kwao; nao wakamjua, na kumtenda uovu usiku kucha hata asubuhi... [26]Ndipo huyo mwanamke akaja alfajiri, akaanguka chini mlangoni pa nyumba ya mtu yule alimokuwamo bwana wake…. [29]Naye alipokwisha kuingia nyumbani mwake, akatwaa kisu, kisha akamshika huyo suria yake, akampasua kiungo kwa kiungo, vipande kumi na viwili...'' Waamuzi 19:22-29<br><br>Swali kwa nia njema: Je, yale aliyoyasema Lutu kuwaambia watu wake: ''nawasihi nitawatolea kwenu mkawafanyie vilivyo vyema machoni penu,'' (Mwanzo 19:8). Sio yale yale aliyoyasema mtu Mlawi 'asiye na wivu ''watwezeni, na kuwatenda hayo myaonayo kuwa ni mema''? | lililofanya kulinda heshima na mke na ndugu wa kike ni jambo la kisheria. Na atakayekufa akitetea haya anahesabiwa ni shahidi (shujaa). Kwa kauli ya Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake: (Atakayeuawa wakati anawatetea watu wake huyo ni shahidi) Imepokewa na Ahmad. |
| Utakatifu upo wapi kwa mwanamume kumuomba mwanamume mwingine aweke mkono wake chini ya paja la mwanamume wa kwanza? | ''[2]Ibrahimu akamwambia mtumishi wake, mzee wa nyumba yake… Tafadhali uutie mkono wako chini ya paja langu…'' Mwanzo 24:2<br><br>''[29]Siku za kufa kwake Israeli zikakaribia; akamwita mwanawe Yusufu, akamwambia, Kama nimeona kibali machoni pako, weka mkono wako chini ya paja langu, ukanifanyie rehema na kweli; nakusihi usinizike katika Misri.'' Mwanzo 47:29 | (Na Ibrahimu akawahusia haya wanawe; na Yakubu pia akawausia wanawe); "Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuchagulieni dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa waislamu (wanyenyekevu). Al-Baqarah 132 |
| Je, katika sharti za miujiza ni kufunga mlango na kuweka mdomo kwenye mdomo mwingine na kulala juu ya mtoto ili kumuhuisha maiti? | ''[32]Basi Elisha alipofika nyumbani, tazama, mtoto amekwisha kufa… [33]Basi akaingia ndani, akajifungia mlango, yeye na yule mtoto wote wawili, akamwomba BWANA. [34]Akapanda juu ya kitanda, akajilaza juu ya mtoto, akaweka kinywa chake juu ya kinywa chake, na macho yake juu ya macho yake, na mikono yake juu ya mikono yake; akajinyosha juu yake; mwili wake yule mtoto ukaanza kupata moto. [35]… akapanda, akajinyosha juu yake; na yule mtoto akapiga chafya mara saba, na mtoto akafumbua macho yake.'' 2 Wafalme 4:32-35 | Elisha au Eliasa alikuwa ni Nabii miongoni mwa manabii wa wana wa Israeli. (Na mkumbuke Ismaili na Alyasaa na Dhulkifli; na hao wote walikuwa miongoni mwa watu bora). Sad 48.<br><br>(Na (tukamwongoa) Ismaili na Al-Yasaa (Elisha) na Yunusi na Luti. Na wote tukawafadhilisha |

| | | |
|---|---|---|
| | Swali la kutafakuri: Elisha alikuwa anafufua wafu kwa idhini ya Mungu, Wayahudi wala hawakumfanya Mungu… Kwa nini Wakristo wamemfanya Yesu ni Mungu wakati Yesu naye pia alikuwa anafufua wafu kwa idhini ya Mungu? | juu ya walimwengu (wote katika zama zo). Al-An-am 86. |
| Utakatifu upo wapi katika mapenzi ya ajabu kabisa baina ya wanaume wawili Yonathani/Daud?<br><br>Je, maandiko ya kuoneshana mapenzi ya kingono baina ya wanaume wawili ni matakatifu? | ''[26]Nimesikitika kwa ajili yako, Yonathani, ndugu yangu, Ulikuwa ukinipendeza sana; Upendo wako kwangu ulikuwa wa ajabu, Kupita upendo wa wanawake.'' 2 Samweli 1:26.<br><br>''[1]Ikawa Daudi alipokwisha kusema na Sauli, roho ya Yonathani, ikaambatana na roho ya Daudi, Yonathani akampenda kama roho yake mwenyewe.'' 1 Samweli 18:1<br><br>''[4]Ndipo Yonathani akamwambia Daudi, Kadiri roho yako itakavyo, nitakutendea.'' 1 Samweli 20:4<br><br>''[23]Sauli na Yonathani walipendwa na kupendeza Maishani wala mautini hawakutengwa; Walikuwa wepesi kuliko tai, Walikuwa hodari kuliko simba.'' 2 Samweli 1:23 | Miongoni mwa aina za ushoga (mapenzi ya jinsia moja), ni stori za mapenzi na kupendezana baina ya wanaume wawili. Na hili linawakilisha tukio miongoni mwa matukio ya kuporomoka kwa maadili ya wanadamu na kuacha maumbile yake ya kiutu.<br><br>Kutoka kwa Jaabiri, Mungu amuwie radhi, amesema: Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, amesema: "Hakika hofu kuu ninayoihofia kwa uma wangu ni matendo ya watu wa Lutu." Mpokezi amesema, hadithi hii ina daraja la hasani na ni gharib. |
| Utakatifu upo wapi katika kutokuwa na haya kwa Daudi na kujifunua mbele za watu wa Mungu? | ''[20]Ndipo Daudi akarudi ili awabarikie watu wa nyumbani mwake. Na Mikali, binti Sauli, akatoka nje aende kumlaki Daudi, naye akasema, Mfalme wa Israeli alikuwa mtukufu leo namna gani, akijifunua mwili wake mbele ya vijakazi vya watumishi wake, mfano wa watu baradhuli mmojawapo, ajifunuavyo mwili wake mbele ya watu, asipokuwa na haya!'' 2 Samweli 6:20 | (Na bila shaka tuliwapa Daudi na Suleimani ilimu (kubwa kabisa na wakamshukuru Mwenyezi Mungu) wakasema: "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu. (Tunamshukuru Mwenyezi Mungu) aliyetufadhilisha kuliko wengi katika waja wake waliomuamini!" An-naml 15 |
| Je, mwanamume akimbaka msichana aliyechumbiwa akiwa kondeni adhabu yake ni kuuawa? | ''[25]Lakini yule mtu mume kama akimkuta kondeni kijana aliyeposwa, naye mume akamtenza nguvu, akalala naye; yule mtu mume aliyelala naye na afe pekee; [26]lakini yule kijana usimfanye neno; hana dhambi yule kijana ipasayo kuuawa, kwa kuwa ni mfano wa mtu kumwondokea mwenzake akamwua, ni vivyo lilivyo jambo hili; [27]kwani alimkuta | (Wala usikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kabisa). Bani Israil 32 |

| | | |
|---|---|---|
| | kondeni; yule kijana aliyeposwa akalia, pasiwe na mtu wa kumwokoa.'' Kumbukumbu la Torati 22:25-27 | |
| Je, haya maandiko ya kingono yanahamasisha jamii itenda mema? | ''[10]Mimi ni wake mpendwa wangu, Na shauku yake ni juu yangu. [11]Njoo, mpendwa wangu, twende mashambani, Tufanye maskani katika vijiji. [12]Twende mapema hata mashamba ya mizabibu, Tuone kama mzabibu umechanua, Na maua yake yamefunuka; Kama mikomamanga imetoa maua; Huko nitakupa pambaja zangu.'' Wimbo Ulio Bora 7:10-12<br><br>Swali: Chukulia.. Suleimani anaongea mapenzi na mkewe… Je, andiko hili ni ufunuo mtakatifu? | Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Uma wangu wote utasamehewa isipokuwa wale wanaodhihirisha dhambi zao. Na kwa hakika miongoni mwa wadhihirishao dhambi ni mtu atende jambo baya usiku kisha ikifika asubuhi amesitiriwa na Allah, mtu huyo anasema: ewe Fulani jana nilifanya hili na hili. Kwa hakika alilala usiku akiwa amestiriwa na Mola wake na anaamka asubuhi anafunua yale aliyositiriwa na Allah). Bukhariyu na Muslim. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la kale ni kutumia miili ya wanawake ili kuwaulia maadui? | **Judith ameimba wimbo uliomfedhehesha pale aliposema:**<br><br>''Judith mwana wa… amemwangamiza kwa uzuri wake. Alivua nguo za ujane wake na kuvaa za harusi ili kuwafurahisha wana wa Israeli. Uliupaka manukato uso wake, na kusuka nywele zake… akavalia vidani vya fakhari ili amfitinishe. Kupendeza kwa viatu vya Judith vilinyakua macho yake, na uzuri wake uliiteka nafsi yake kwa hiyo Judith akamkata shingo kwa jambia.'' Tazama kitabu cha Judith kipo kwa Wakatoriki na Waothodox | Uislamu unapinga kutumia mwili wa mwanamke kwa lengo lolote lile. (Kwa yakini wale wanaopenda uenee uovu kwa wale walioamini, watapata adhabu iumizayo katika dunia na akhera; …) Annur 19. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la kale ni kumpigia debe Rahabu (bibi wa nafsi ya pili ya Mungu) ambaye ni mzinifu katika | ''[1]Yoshua, mwana wa Nuni, akawatuma watu wawili kutoka Shitimu kwa siri, ili kupeleleza, akawaambia, Enendeni mkaitazame nchi hii, na Yeriko. Wakaenda wakafika nyumbani kwa kahaba mmoja jina lake aliitwa Rahabu, wakalala huko… [3]Mfalme wa Yeriko akatuma watu kwa Rahabu, akasema, Watoe watu wale waliokuja kwako, walioingia ndani ya nyumba yako, maana wamekuja ili kuipeleleza nchi. [4]Yule mwanamke akawatwaa wale watu wawili, akawaficha, akasema, Naam, wale | Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Hatozini mzinifu, wakati anazini awe bado ni muumini) Ameipokea Albukhariyu (2475) na Muslim (57).<br><br>Na Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, ameeleza kuhusu adhabu ya wazinifu kaburini. |

| | | |
|---|---|---|
| uzinifu wake na hadaa zake? | watu walikuja kwangu, lakini sikujua walikotoka; [5]… wala sijui walikokwenda; wafuateni upesi, maana mtawapata.'' Yoshua 2:1-5 | Kuwa wao wataadhibiwa kwa moto. Imepokewa na Al-Bukhariyu (1320). |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwahamasisha wanadamu kuutumia uzuri na miili ya wanawake, kama ilivyo katika kisa cha Esta mzinifu wa kike na Ami yake Mordekai ambaye ni kuwadi? | ''[5]Basi palikuwa na Myahudi mmoja huko Shushani ngomeni; jina lake Mordekai… [7]Naye alikuwa amemlea Hadasa, yaani, Esta, binti wa mjomba wake, kwa kuwa hana baba wala mama. Naye msichana huyu alikuwa wa umbo, mzuri na uso mwema… Esta naye aliingizwa katika nyumba ya mfalme… [10]Walakini Esta hakudhihirisha kabila yake wala jamaa yake, kwa maana ndivyo alivyomwagiza Mordekai asiwadhihirishe… [16]Basi Esta alipelekwa kwa mfalme… [17]Mfalme akampenda Esta kuliko wanawake wote, naye akapata neema na kibali machoni pake kuliko mabikira wote; basi akamtia taji ya kifalme kichwani pake… [20]Esta alikuwa hajadhihirisha jamaa yake wala kabila yake, kama vile Mordekai alivyomwagiza; kwa maana Esta alikuwa akiyashika maagizo ya Mordekai, vile vile kama wakati alipolelewa naye…'' Esta 2:5-20. | Usilamu unakataza mwanamke asifanye kazi za madanguro na kuutumia mwili wake au uzuri wake kwa malengo ya kivita na kingono. (Kwa yakini wale wanaopenda uenee uovu kwa wale walioamini, watapata adhabu iumizayo katika dunia na akhera; …) Annur 19. |
| Mpendwa msomaji:<br><br>Baada ya kusoma sura ya kwanza katika kitabu hiki.<br><br>Je, unaamini kwamba uasherati na uzinzi na kujiweka uchi na ngono zembe ni miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale? | | |
| **Sura ya pili: Je, Roho Mtakatifu (nafsi ya tatu) wakati anapokuwa kwa mwanadamu anafanya maovu?** | | |
| Utakatifu upo wapi katika Roho Mtakatifu (nafsi ya tatu ya Mungu) ambaye anamtokea Sauli kisha anatukana kwa maneno mabaya na kutabiri akiwa uchi? | ''… na roho ya Mungu ikamjilia yeye, akaendelea mbele, huku anatabiri… [24] Naye akavua nguo zake, akatabiri mbele ya Samweli, akalala uchi mchana kutwa na usiku kucha… '' 1 Samweli 19:23-24.<br><br>''Basi hasira yake Sauli ikawaka juu ya Yonathani, akamwambia, Wewe, mwana wa mke mkaidi, asi je! Mimi sijui ya kuwa umechagua huyo mwana wa Yese, kwa aibu yako mwenyewe, na kwa aibu ya uchi wa mama yako.'' 1 Samweli 20:30.<br><br>______________________________________ | Roho sio miongoni mwa sifa za Mungu Mtukufu. Bali yeye ni miongoni mwa viumbe vya Mungu. (Na wanakuuliza habari za Roho. Sema: "Roho ni jambo lililohusika na Mola wangu (Mwenyezi Mungu)…" Bani Israil 85.<br><br>Na kulihusisha neno Roho na neno tukufu Mwenyezi Mungu ni kulihusisha kwa kulipatia ujiko (utukufu) na kulikirimu. |

| | | |
|---|---|---|
| Utakatifu upo wapi kwa Roho Mtakatifu (nafsi ya tatu ya Mungu) ambaye anamtokea Daudi wakati akizini?<br><br>Utakatifu upo wapi kwa Roho Mtakatifu (nafsi ya tatu ya Mungu) ambaye anamtokea Samsoni ili amuue mtoto wa simba na kuwakamata mbweha mia tatu na kuwaua mfupa wa punda elfu moja. Na kuzini huko "Gaza" na anatengana na Roho Mtakatifu baada ya kunyoa nywele? | ''… roho ya BWANA ikamjia Daudi kwa nguvu tangu siku ile… '' 1 Samweli 16:13.<br><br>''… alipokuwa juu ya dari aliona mwanamke anaoga; nayo huyo mwanamke alikuwa mzuri sana… [4] Basi Daudi akapeleka wajumbe, akamtwaa; naye akaingia kwake; naye akalala naye; (maana Yule mwanamke amekwisha kutakasika unajisi wake)…) 2 Samweli 11:2-4.<br><br>''Ndipo Samsoni… na tazama, mwana-simba akamngurumia. [6] Roho ya BWANA ikamjilia kwa nguvu, naye akampasua kana kwamba anampasua mwana-mbuzi…) Waamuzi 14:5-6.<br><br>''… Ndipo roho wa BWANA ikamjia kwa nguvu, … akapiga watu elfu kwa mfupa huo.'' Waamuzi 15:14-15<br><br>''Roho ya BWANA ikamjilia juu yake … akapiga watu waume thelathini katika watu hao, na kuzitwaa nyara zao, na kuwapa hao waliokitambua kitendawili mavao hayo..'' Waamuzi 14:19<br><br>''Samsoni akaenda Gaza, akaona huko mwanamke kahaba, akaingia kwake.'' Waamuzi 16:1<br><br>'' [4]Samsoni akaenda akakamata mbweha mia tatu; kisha akatwaa vienge vya moto akawafunga mbweha mkia kwa mkia, akatia kienge kati ya kila mikia miwili. [5]Alipokwisha kuviwasha moto vile vienge, akawaachia mbweha kati ya ngano ya Wafilisti, akayateketeza matita, na ngano, hata na mashamba ya mizeituni.'' Waamuzi 15:4-5<br><br>"[17]Ndipo alipomwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake, akamwambia, Wembe haukupita juu ya kichwa changu kamwe; maana mimi nimekuwa Mnadhiri wa Mungu, tangu tumboni mwa mama yangu; nikinyolewa, ndipo nguvu zangu zitanitoka, nami nitakuwa dhaifu, nitakuwa kama wanadamu wenzangu… Kisha akamwita mtu akavinyoa vile vishungi saba vya nywele za kichwa chake; akaanza | Kwani, Mwenyezi Mungu ndiye aliyeiumba na kuimiliki. Anaifisha muda wowote atakao. Na anaituma muda wowote atakao. (Kisha akamtengeneza na akampulizia roho Yake….). Sajdah 9. (Basi nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na mimi, …) Al-Hijr 29.<br><br>Ama kuhusu Roho Mtakatifu, yeye ni mja wa Mungu na mjumbe wake Jibrilu, amani iwe juu yake, aliyetumwa na Mungu kwa Mitume na manabii, na kwa Maryam, rehema na amani ziwe juu yao.<br><br>Mwenyezi Mungu amemuhusisha kwake huyo Roho Mtakatifu, katika kauli yake (Roho wetu) kwa maana ya Jibrilu, amani iwe juu yake. Uhusisho wa hapa ni wa kumkirimu na kumtukuza. Huu ni uhusisho wa kiumbe, Jibrilu, amani iwe juu yake, kwa Muumba wake Mtukufu. (Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Muhuisha Sharia yetu (Jibrili) akajimithilisha kwake (kwa sura ya) binadamu aliyekamili. (Mariamu) akasema: "Hakika mimi najikinga kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema (Aniepushe) nawe. Ikiwa unamuogopa Mungu (basi ondoka nenda zako)." (Malaika) akesema: "Hakika mimi ni mjumbe wa Mola wako; ili |

| | | |
|---|---|---|
| Utakatifu upo wapi kwa roho wa Mungu (nafsi ya tatu ya Mungu) aliyevaa Gideoni na kaua na huyo Roho wa Mungu hakumzuia kuzini na Israeli huko nyuma yake?<br><br>Utakatifu upo wapi kwa roho wa Mungu (nafsi ya tatu ya Mungu) amabaye anamshukia Yeftha wakati anamchinja binti yake bikra katika sadaka ya kuteketezwa? Dhambi yake ni nini? | kumsumbua, nguvu zake zikamtoka… Lakini hakujua ya kuwa BWANA amemwacha.'' Waamuzi 16:17-20<br><br>''[34] Lakini roho ya BWANA ikaja juu yake Gideoni; naye akapiga tarumbeta; na Abiezeri walikutanika na kumfuata.'' Waamuzi 6:34<br><br>''[4]Basi Gideoni akafika Yordani, akauvuka, yeye na hao watu mia tatu waliokuwa pamoja naye… [10]… kwa sababu walianguka watu mia na ishirini elfu waliokuwa wenye kutumia upanga.'' Waamuzi 8:4-10<br><br>''Basi Gideoni akafanya naivera kwa vitu vile, akaiweka katika mji wake, mji huo wa Ofra; nao Israeli wote wakaenda na kuiandama kwa ukahaba huko; nayo ilikuwa ni tanzi kwa Gideoni na kwa nyumba yake'' Waamuzi 8:27<br><br>''[29]Ndipo roho ya BWANA ikamjilia juu yake Yeftha, … [30]Naye Yeftha akamwekea BWANA nadhiri, akasema, Kwamba wewe utawatia wana wa Amoni mkononi mwangu kweli, [31]ndipo itakuwa ya kwamba, kile kitakachotoka katika milango ya nyumba yangu kunilaki, hapo nitakaporudi na amani kutoka kwa hao wana wa Amoni, kitu hicho kitakuwa ni cha BWANA, nami nitakisogeza kiwe sadaka ya kuteketezwa. [32]Basi Yeftha akavuka kuwaendea wana wa Amoni ili kupigana nao; naye BWANA akawaua mkononi mwake… [34]Kisha Yeftha akafika Mispa nyumbani kwake, na tazama, binti yake akamtokea kumlaki, na matari na machezo; naye alikuwa ni mwanawe pekee; hakuwa na mwingine, mwana wala binti, ila yeye.,[35]Ikawa alipomwona akayararua mavazi yake, akasema, Ole wangu! Mwanangu, umenitweza sana, nawe u mmoja miongoni mwa hao wanisumbuao … [39]… aliyemtenda sawasawa na ile nadhiri yake aliyokuwa ameiweka..'' Waamuzi 11:29-39<br><br>''[19]BWANA akasema, Ni nani atakayemdanganya Ahabu …? Basi huyu akasema hivi; na huyu hivi. [20]Akatoka pepo, akasimama mbele za BWANA, akasema, Mimi nitamdanganya. BWANA | nikupe mwana mtakatifu." Maryam 17 – 19<br><br>Hapo zamani walikuwa wanapotaka kukielezea kitu kwa upeo wa usafi wanasema: hakika hiki ni roho. Na alipokuwa Issa amani iwe juu yake ametokana na "kupuliziwa roho" na sio kwa "mbegu za uzazi" ndipo Issa bin Mariam akahusishwa na tamko "Roho wa Mungu" na kufanya hivi ni katika mlango wa kumtukuza na kumkirimu. Kwani sote ni waja wa Mungu. Na hakika si vinginevyo, kuhusishwa huko ni kwa lengo la kubainisha cheo cha muhusishwa amani iwe juu yake. (Enyi watu wa Kitabu! Msipindukie mipaka katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo kweli. Masihi Isa bin Maryamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na (ni kiumbe aliyeumbwa kwa) tamko lake (tu Mwenyezi Mungu) alilompelekea Maryamu. Na ni roho iliyotoka kwake (Mwenyezi Mungu kama roho nyingine). Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume yake; wala msisema "watatu …" Jizuieni (na itikadi hiyo); itakuwa bora kwenu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mungu Mmoja tu. Ni mbali na utakatifu wake kuwa ana mwana. Ni vyake (vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa kutosha.) An-Nisaa 171. |

<table>
<tr><td>Je, Mungu anampeleka Roho wa uongo ili ampotoshe Ahabu?<br><br>Je, Roho anawapotosha manabii na kumuweka roho wa uongo katika midomo ya manabii?<br><br>Je, roho muovu na mbaya haiondoki isipokuwa kwa kuipigia ala za muziki kinubi?<br><br></td><td>akamwambia, Jinsi gani? [21]Akasema, Nitaondoka, na kuwa pepo wa uongo vinywani mwa manabii wake wote. Akasema, Utamdanganya, na kudiriki pia; ondoka, ukafanye hivyo. [22]Basi sasa, angalia, BWANA ametia pepo wa uongo vinywani mwa manabii wako hawa; naye BWANA amenena mabaya juu yako.'' 1 Wafalme 22:20-23, 2 Mambo ya Nyakati 18:19-22<br><br>''Ikawa, ile roho mbaya kutoka kwa Mungu ilipomjilia Sauli, ndipo Daudi akakishika kinubi, akakipiga kwa mkono wake, naye Sauli akaburudishwa, na ile roho mbaya ikamwacha.'' 1 Samweli 16:23<br><br>''Ikawa, ile roho mbaya kutoka kwa Mungu ilipomjilia Sauli, ndipo Daudi akakishika kinubi, akakipiga kwa mkono wake...'' 1 Samweli 16:23<br><br>''Ikawa siku ya pili yake, roho mbaya kutoka kwa Mungu ikamjilia Sauli kwa nguvu, naye akatabiri ndani ya nyumba. Basi Daudi alikuwa akipiga kinubi kwa mkono wake...'' 1 Samweli 18:10<br><br>1 Samweli 19:9<br><br>''Tena ikawa, roho mbaya kutoka kwa BWANA ilimjilia Sauli, hapo alipoketi ndani ya nyumba yake... naye Daudi alikuwa akipiga kinubi kwa mkono wake.'' 1 Samweli 19:9</td><td>Mtume wa Allah, Isa amani iwe juu yake, yeye ni roho miongoni mwa roho zilizoumbwa na Allah.<br><br>Pia Isa amani iwe juu yake ni "neno la Mungu" kwa kumkirimu na kumtukuza. Hakika Mwenyezi Mungu mtukufu alimuamrisha Jibril Mwaminifu, apulizie kwa Maryamu, upulizo ukateremka kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na ukaingia katika fuko la uzazi la Maryamu na ukawa roho iliyoumbwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na Isa amani iwe juu yake akawa "aliyeumbwa" kwa neno kutoka kwa Mwenyezi Mungu nalo ni (*Kuwa*) bila baba. Na kwa neno (*Kuwa*) ndipo akawa Isa ni kiumbe. Yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni neno lake aliloliweka kwa Maryamu, na ni roho kutoka kwake. Hivyo basi, Isa amani iwe juu yake, yeye sio hilo NENO wala yeye si Mwana wa Mungu. Kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetukuka anapotaka jambo huliambia: kuwa nalo linakuwa.</td></tr>
<tr><td colspan="3">Mpendwa msomaji: Baada ya kusoma sura ya pili katika kitabu hiki.<br><br>Je, unaamini kwamba Roho wa Mungu (nafsi ya tatu ya Mungu) wakati anapomshukia mtu anafanya maovu?</td></tr>
<tr><td colspan="3">Sura ya tatu: Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kumfanyia uadui mwanamke?</td></tr>
<tr><td>Ni zipi hizo laana kumi kwa</td><td>Kuhani wa Taurati (Assanhadrim) amedai kuwa Mungu ameandika laana kumi kwa Eva.</td><td>Hakuna hata aya moja ndani ya Quran Tukufu inayoeleza kuwa Hawa (Eva)</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| mwanamke zilizoandikwa na Mungu wa Agano la Kale? | Na haya ni maelezo ya yale waliyoyaona miongoni mwa shida katika maisha ya wanawake: (1 – Hedhi 2 – Damu ya bikra 3 – Tabu za mimba 4 – Maumivu ya kuzaa 5 – kulea watoto 6 – kufunika kichwa kana kwamba yupo msibani 7 – kutobolewa masikio kana kwamba ni mjakazi 8 – kumsiburi mume kana kwamba ni mtumishi 9 – kutokubaliwa ushahidi wake 10 – baada ya laana zote hizi ni ''umauti''. | ndiye aliyemshawishi Adamu ale ule mti au inayoeleza kuwa Hawa ndiye aliyekula kwanza kabla ya Adamu. Na uchungu wa kujifungua sio adhabu kutoka kwa Allah. Kwani Allah kama alivyotaja katika Quran Tukufu haiadhibu nafsi yeyote kwa dhambi ya nafsi nyingine. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: (… Wala mbebaji (mizigo yake ya dhambi) hatabeba mizigo ya mwingine...) (Al-An-am 164, Bani Israil 15, Fatir 18, A-zumar 7, An-Najm 38) |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anamtuhumu Eva (Hawa) ya kwamba yeye ndiye asili ya kuanza dhambi. Na kwa sababu hii wanaadhibiwa wanawake wote? | ''Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako;'' Mwanzo 3:17<br><br>''Dhambi zilianza kutoka kwa mwanamke, na k wa sababu yake sote tutakufa…'' Sira 25:24 | Adamu na Hawa walifanya dhambi na kisha wakaomba msamaha na kusamehewa na Allah. (Kisha Adam akapokea maneno (ya maombi) kwa Mola wake, (akaomba), na Mola wake akapokea toba yake; hakika yeye ndiye mwingi wa kupokea toba (kwa wenye kutubia) na mwingi wa kurehemu (kwa wanaostahiki kurehemewa…) Al-Baqarah 37 |
| Je, anayezaliwa na mwanamke si msafi na hafai?<br><br>Je, mwanamke ni chanzo cha machafu? | ''Akamwambia mwanamke, Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala.'' Mwanzo 3:16<br><br>Swali: Ikiwa Masihi amekuja ili kuwakomboa na kubeba adhabu ya mauti kwa niaba ya wanadamu. Sasa kwa nini mwanamke aendelee kuadhibiwa kwa maumivu ya mimba na kuzaa hadi sasa? Kwa nini kikawepo kisa cha kusulubiwa, kuokoa, kufufuka na utakaso? | Bibi Maryam amani iwe juu yake, mama wa nabii Isa Masihi, yeye ni mwanamke mtukufu, anayejiheshimu, msafi, alivumilia maudhi ya watu wake. Pia alikuwa mcha Mungu, anayemjua Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa hakika alikirimiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa karama za waziwazi. Na Mwenyezi Mungu amemchagua baina ya wanawake wote ili awe mama wa Nabii Isa Masihi rehema na amani ziwe juu yake. Bila ya kuwa na mume |

| | | |
|---|---|---|
| Je, mwanamke ni mjinga na msaliti?<br><br>Je, hakuna mwanamke mwema?<br><br>Je, mwanamke mzuri hana akili?<br><br>Je, mwanamke ni jambo katika mauti? | ''Basi mtu awezaje kuwa na haki mbele ya Mungu?<br><br>Au awezaje kuwa safi aliyezaliwa na mwanamke?'' Ayubu 25:4<br><br>''Je! Mwanadamu ni kitu gani, hata akawa safi?<br><br>Huyo aliyezaliwa na mwanamke, hata awe na haki?'' Ayubu 15:14<br><br>Swali: Je, Maryam mama yake Yesu amerithi dhambi kutoka kwa mababu zake? Je, yeye ni safi na ana haki?<br><br>''… kutokana na nguo amekuja nondo, na kuto ka kwa mwanamke umekuja uovu''Sira 42:13<br><br>''Mwanamke mpumbavu hupiga kelele,<br><br>Ni mjinga, hajui kitu.'' Mithali 9:13<br><br>''Hakika kama vile mke amwachavyo mumewe kwa hiana...'' Yeremia 3:20<br><br>''… mwanamume mmoja katika elfu nimemw ona; bali mwanamke mmoja miongoni mwa w ote mimi sikumwona.'' Mhubiri 7:28<br><br>''Kama pete ya dhahabu katika pua ya nguruwe, | au kuguswa na mwanamume. Na bibi Maryam amani iwe juu yake, ni mwanamke bora kabisa duniani kwa andiko la Quran Tukufu na hadithi ya Mtume Mtukufu. Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema katika uteremsho wake madhubuti: (Na (kumbuka) Malaika waliposema: "Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amekuchagua na kukutakasa na kukutukuza kuliko wanawake wa ulimwengu (wote). Aali Imran 42.<br><br>Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, amesema: "Mwanamke mbora kabisa ni Maryamu binti Imraan kisha Fatuma binti Muhammad kisha Khadija binti Khuwaylidi Kisha Asia binti Muzaahimu" Imepokewa na Alhaafidh Ibni Abdilbarri.<br><br>(Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo (zinaa) ni uchafu (mkubwa) na ni njia mbaya (kiabisa). Bani Israil 32.<br><br>Sheria ya Kiislamu imekuja kuharamisha maswala ya kumtundika mwanamke. Na ikaweka misingi: kama hakutakuwa na maafikiano iwepo talaka. (Talaka (anazoweza kumrejea mwanamke) ni (zile zilizotolewa) mara mbili (za kwanza). Kisha ni kumweka/kukaa naye kwa wema au kumwacha kwa ihsani…) Al-Baqarah 229 |

| | | |
|---|---|---|
| Je, mwanamke ni kuoza ndani ya mfupa?<br><br>Je, mjane ambaye hajazaa hana haki ya kutoa maoni yake katika ndoa yake mpya?<br><br>Je, ndugu wa mume anamwagia mbegu zake ardhini kama alivyofanya Onani? | Kadhalika mwanamke mzuri asiye na akili.'' Mithali 11:22<br><br>''Nami nimeona lililo na uchungu kupita mauti; yaani, mwanamke ambaye moyo wake ni mitego na tanzi, na mikono yake ni kama vifungo...'' Mhubiri 7:26<br><br>''Mwanamke mwema ni taji ya mumewe;<br>Bali aaibishaye ni kama kuoza mifupani mwake.'' Mithali 12:4<br><br>''[5]Watakapoketi pamoja mtu na nduguye, mmojawapo akafa, wala hana mwana wa kiume, mke wa yule aliyekufa asiolewe nje na mgeni; nduguye yule mumewe amwingilie amweke kwake awe mkewe, kumfanyia yampasayo nduguye mumewe. [6]Na iwe, yule mzaliwa wa kwanza atakayemzaa, amfuate nduguye aliyekufa kwa jina lake, lisije likafutwa jina lake katika Israeli.'' Kumbukumbu la Torati 25:5-6<br><br>''Onani alijua ya kwamba huo uzao hautakuwa wake, ikawa, alipoingia kwa mke wa nduguye, akamwagia chini asimpe nduguye uzao.'' Mwanzo 38:9<br><br>''[7]Na yule mtu kwamba hapendi kumtwaa mke wa nduguye, aende huyo mke wa nduguye langoni kwa wazee, akawaambie, Nduguye mume wangu yuakataa kumsimamishia nduguye jina katika Israeli, hataki kunitimizia yampasayo nduguye mume | Maumivu ya hedhi si adhabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Katika Sahihu Muslim kutoka kwa Anasi: Kwa hakika Mayahudi walikuwa pindi wanawake miongoni mwao wanapopata hedhi hawali nao na hawachanganyiki nao katika majumba. Maswahaba wa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, wakamuuliza. Ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha: (Na wanakuuliza juu ya hedhi; waambie huo ni uchafu. Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi (zao). Wala msiwakaribie mpaka watwaharike. Wakishakutwaharika basi waendeeni katika pale alipokuamrisheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanaojitakasa.) Al –Baqarah 222.<br><br>Na Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, akasema: "Fanyeni naye kila kitu isipokuwa tendo la ndoa tu." Maneno haya yakawafikia Wayahudi nao wakasema: Mtu huyu hataki kuacha jambo letu lolote isipokuwa lazima aende kinyume nalo.<br><br>Hedhi ina hukumu nyingi zaidi ya ishirini. Tutataja katika hizo: swala na funga.<br><br>Hukumu ya swala: Ni haramu kwa mwenye hedhi kuswali swala ya fardhi wala ya suna. Pia hapaswi kuswali isipokuwa kama atauwahi wakati wa swala kiasi cha rakaa moja kamili, hapo ndipo atalazimika kuswali. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, mjane anatemea mate usoni na kuvua viatu vya ndugu wa mumewe anapokataa kuolewa naye? | wangu. [8]Ndipo wamwite wazee wa mji wake waseme naye; naye akisimama na kusema, Sitaki mimi kumtwaa mwanamke huyu, [9]ndipo mke wa nduguye amkaribie mbele ya hao wazee, amvue kiatu chake mguuni mwake, na kumtemea mate ya uso; kisha atajibu yule mwanamke, aseme, Mume akataaye kumjengea nduguye nyumba yake na afanywe hivi. [10]Na jina lake katika Israeli liitwe, Nyumba ya mvuliwa kiatu.'' Kumbukumbu la Torati 25:7-10 | Sawasawa ameuwahi wakati huo mwanzoni mwake au mwishoni mwake. Ama adhkaari (dua) na Takbira, Tasbihi, Tahmiidi, kusema bismillah wakati wa kula na mengineo, kusoma hadithi, fiqihi, na dua, kuitikia amiin katika dua, na kusikiliza Quran hayo si haramu kwa mwenye hedhi. |
| Heshima ya mwanamke ipo wapi? | ''[14]Basi akavua nguo za ujane wake, akajivika utaji, akajifunika uso, akakaa mlangoni pa Enaimu, karibu na njia ya kuendea Timna. Maana aliona ya kwamba Shela amekuwa mtu mzima, wala hakuozwa awe mkewe. [15]Yuda alipomwona alimdhania kuwa ni kahaba, maana amejifunika uso. [16]Akamgeukia kando ya njia, akasema, Niruhusu niingie kwako. Maana hakujua ya kuwa ni mkwewe. Akamwuliza, Utanipa nini, ukiingia kwangu? [17]Akasema, Nitakuletea mwana-mbuzi wa kundini. Naye akamwuliza, Je! Utanipa rehani hata utakapomleta?'' Mwanzo 38:14-17 | Hukumu ya funga: Kwa mwenye hedhi ni haramu kufunga faradhi au sunna, na anapaswa alipe funga za faradhi. Kwa mujibu wa hadithi ya Aisha, Allah amuwie radhi: (Tulikuwa tunapatwa na hilo – yaani hedhi – tuliamrishwa kulipa funga wala hatukuamrishwa kulipa swala). Al-Bukhariyu na Muslimu. |
| Je, mjane, pindipo hajaolewa na ndugu wa mume na akawa huyo mjane anatamani kuzaa azini kama alivyofanya Tamara? | '' [13]Naye atamwoa mwanamke katika ubikira wake. [14]Asitwae mjane, wala mwanamke aliyeachwa na mumewe, wala mwanamke mwenye unajisi, wala kahaba; lakini atamwoa mwanamwali katika watu wake mwenyewe. [15]Naye asiwatie unajisi kizazi chake ....'' Mambo ya Walawi 21:13-15 | Baba hana haki ya kumuuza binti yake. Mtu huru hauzwi. Kutoka kwa Abuu huraira, Mungu amuwie radhi. Kutoka kwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, amesema: Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: Watu watatu nitagombana nao siku ya kiama; Mtua aliyenipa (kitu) kisha akanisaliti. Na mtu aliyemuuza mtu huru na kula thamani yake. Na mtu aliyemwajiri mfanyakazi aliyetekeleza wajibu wake na hakumlipa ujira wake. Al-Bukhariyu. |
| Je, mwanamke aliyeachwa hana vigezo vya kuwa mke wa Kuhani? | ''Wala hawataoa wanawake wajane, wala mwanamke aliyeachwa na mume wake; lakini watatwaa mabikira wa wazao wa nyumba ya | Mwanamume atakapo- mtuhumu mkewe kwa uzinzi. Na mke akakataa katakata tuhuma hizo. Au mume akidai kuwa mtoto wa mkewe si wake. Na mke akapinga na kusema mtoto ni |

| | | |
|---|---|---|
| Je, mwanamke ataendelea kuwa kama aliyening`inia hadi aachwe? | Israeli, au mjane aliyefiwa na mumewe kuhani.'' Ezekieli 44:22<br><br>Mwanamke hana haki ya kuomba talaka na hivyo ataendelea kama aliyetundikwa (aliyefungwa). Na mwanamume ndiye pekee mwenye haki ya kumpa talaka mkewe na kumaliza ndoa. Kumbukumbu la Torati 24:1, Isaya 50:1 | wa mumewe, na hakuna ushahidi. Wawili hao wataenda katika, kuapizana (kulaaniana) kwa muundo uliobainishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na wale wanaowasingizia wake zao (kuwa wamezini) na hawana mashahidi ila nafsi zao, basi ushahidi wa mmoja wao utakuwa kushuhudilia mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu: ya kwamba bila shaka yeye ni mmoja wa wanaosema kweli. Na mara ya tano (aape) kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa ni miongoni mwa waongo. Na (mke) itamuondokea adhabu kwa kutoa shahada mara nne kwa kiapo cha Mwenyezi Mungu ya kwamba (huyu mume) ni miongoni mwa waongo. Na mara ya tano (aape) ya kwamba hasira ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake kama (mumewe) yu miongoni mwa wasema kweli, (na yeye mke ndiye muongo). Annur 6 – 9. |
| Je, mwanamke hukatwa mkono wake akishika uchi wa mwanamume? | '' [11]Washindanapo waume wao kwa wao, akakaribia mke wa mmojawapo, ili kumwokoa mumewe katika mkono wa ampigaye, yule mke akatoa mkono wake, na kumkamata tupu yake; [12]umkate ule mkono wake, lisiwe na huruma jicho lako.'' Kumbukumbu la Torati 25:11-12 | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anamuadhibu mwanamke mwenye hedhi na huyo mwanamke ataendelea kunyanyapaliwa na kukinajisi kila kitu kinachomzunguka hadi hedhi iishe? | '' [19]Mwanamke ye yote, kama anatokwa na kitu, na kitu chake alichokuwa nacho mwilini mwake ni damu, ataketi katika kutengwa kwake muda wa siku saba; na mtu ye yote atakayemgusa atakuwa najisi hata jioni. [20]Na kitu cho chote akilaliacho katika kutengwa kwake kitakuwa najisi; na kila kitu ambacho akiketia kitakuwa najisi. [21]Mtu ye yote atakayekigusa kitanda chake huyo mwanamke atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni. [22]Mtu ye yote atakayekigusa cho chote ambacho huyo mwanamke amekiketia atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni. [23]Kwamba ni katika kitanda, au cho chote alichokikalia huyo mwanamke, atakapokigusa kitu hicho, atakuwa najisi hata jioni. [24]Na mtu ye yote atakayelala na mwanamke na unajisi ukawa juu yake, atakuwa najisi muda wa siku saba; na kila kitanda alichokilalia kitakuwa najisi. [25]Na mwanamke kama akitokwa na damu yake siku | Quran Tukufu haijaondoa uaminifu wake kwa bibie Sara na haijamtuhumu kwa chochote. (Na mkewe (Ibrahimu – Bibi Sara) alikuwa kasimama wima (anawatumikia); akacheka (aliposikia hivyo). Basi tukampa habari njema ya (kuwa watazaa mtoto wamwite) Is-haqa...) Hud 71.<br><br>Ushahidi wa mwanamume mmoja kwa wanawake wawili katika mikataba ni kwa ajili ya kuthibitisha hukumu na si kwa ajili ya upungufu wa mwanamke. Ushahidi wa mwanamume haukubaliki katika mambo yanayomuhusu mwanamke. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, mwanamke anajihesabia nafsi yake siku saba baada ya kuisha hedhi ili awe msafi tena?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale anamuadhibu mwanamke kwa kutokewa na hedhi yake na hana budi huyo mwanamke atoe kafara ya vifaranga viwili vya njiwa?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale anamwadhibu mwanamke mwenye damu ya uzazi, na hana budi huyo mwanamke atoe kafara ya kondoo au njiwa au njiwa pori? | nyingi, nayo si katika majira ya kutengwa kwake, au kama anatoka damu kuzidi majira ya kutengwa kwake; siku hizo zote za kutoka damu ya unajisi wake, atakuwa kama alivyokuwa katika siku za kutengwa kwake; yeye yu najisi. [26]Kila kitanda akilaliacho katika siku zote za kutoka damu kitakuwa kama kitanda cha kutengwa kwake; na kila kitu atakachokilalia kitakuwa najisi, kama unajisi wa kutengwa kwake. [27]Na mtu ye yote atakayevigusa vitu vile atakuwa najisi, naye atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni. [28]Lakini huyo mwanamke kwamba ametakaswa na kule kutoka damu kwake, ndipo atakapojihesabia siku saba, na baadaye atakuwa safi. [29]Siku ya nane atajipatia ua wawili, au makinda mawili ya njiwa, na kumletea kuhani, mlangoni pa hema ya kukutania. [30]Kuhani atamsogeza mmoja kuwa sadaka ya dhambi, na wa pili kuwa sadaka ya kuteketezwa; naye kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake mbele za BWANA, kwa ajili ya kutoka damu ya unajisi kwake.'' Mambo ya Walawi 15:19-30<br><br>'' [6]Kisha hizo siku za kutakaswa kwake zitakapotimia, kwa ajili ya mwana, au kwa ajili ya binti, ataleta mwana-kondoo wa mwaka mmoja kuwa sadaka ya kuteketezwa na kinda la njiwa, au ua, kuwa sadaka ya dhambi, awalete mlangoni pa hema ya kukutania, na kumpa kuhani; [7]na yeye atawasogeza mbele za BWANA, na kufanya upatanisho kwa ajili yake; naye atatakasika na jicho la damu yake. Hii ndiyo amri yake huyo azaaye, kwamba ni mtoto mume au mke. [8]Kama mali yake huyo mwanamke haimfikilii mwana-kondoo, hapo ndipo atakapochukua hua wawili, au makinda mawili ya njiwa; mmoja kuwa sadaka ya kuteketezwa, na wa pili kuwa sadaka ya | Lakini ushahidi wa mwanamke katika mambo yake yanayomuhusu hukubaliwa, kwa mfano mambo ya kujifungua, kunyonyesha, hedhi na kubeba mimba.<br><br>Endapo mume ataweka sharti la kuwa mke awe bikra na alipolala naye akamkuta kinyume na hivyo. Basi huyo mume ana haki ya kuvunja ndoa. Na kama suala hilo la kutokuwa bikra lilijulikana kabla ya kumuingilia, basi huyo mke hapati chochote katika mahari, na kama lilijulikana baada ya kumuingilia, basi kama huyo mke ndiye aliyemdanganya mume atapaswa arejeshe mahari kwa mume.<br><br>Na kama mume atakuwa kadanganywa na walii (msimamizi wa ndoa) wa mke au na mtu mwingine yeyote Yule huyo mtu aliyemdanganya mume ndiye atakayemlipa huyo mume mahari aliyoitoa.<br><br>Mwanamke ana haki ya kutumia mali zake. Kutoka kwa Abuu Said Al-Khudriyu, Mungu amuwie radhi, Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, amesema: "… Enyi makundi ya wanawake toeni sadaka …" (Al-Bukhariyu)<br><br>Kutoka kwa Jabir bin Abdillahi, Mungu amuwie radhi, Mtume, Rehema na |

| | | |
|---|---|---|
| Kwa nini mwanamke anakuwa najisi kwa wiki moja pindi anapojifungua mtoto wa kiume na anakuwa najisi kwa wiki mbili anapojifungua mtoto wa kike? | dhambi; naye kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake, naye atakuwa safi.'' Mambo ya Walawi 12:6-8<br><br>''[2]… Mwanamke akitunga mimba na kuzaa mtoto mume, ndipo atakuwa yu najisi siku saba... [3]Siku nane mtoto atatahiriwa govi ya zunga lake. … [5]Lakini kwamba amezaa mtoto mke ndipo atakuwa najisi juma mbili…'' Mambo ya Walawi 12:2-5<br><br>Swali la tafakuri na utafiti wa kisayansi: hivi kwa nini najisi ya mwanamke ni wiki moja akizaa mwanamume na wiki mbili akizaa mtoto wa kike? | amani ziwe juu yake, amesema: (… wakawa wanatoa mapambo yao sadaka na kuyatupia katika nguo ya Bilali (Mungu amuwie radhi) miongoni mwa hereni na pete zao). Muslimu 885.<br><br>Mjane ana haki ya kumrithi mumewe. (… Nao wake zenu watapata robo ya mlivyoacha, ikiwa hamna mtoto (wala mjukuu). Lakini mkiwa mnaye mtoto au mjukuu, basi hao (wanawake) watapata thumuni (sehemu ya nane) ya vile mlivyoacha….) An-nisaa 12. |
| Je, mwanamke huuzwa ili awe mjakazi? | ''[7]Mtu akimwuza binti yake awe kijakazi, hatatoka yeye kama watumwa wa kiume watokavyo. [8]Kwamba bwana wake hakupendezewa naye...'' Kutoka 21:7-8 | |
| Mungu wa Agano la Kale anakusudia nini anaposema kwamba mwanamke anafungua mdomo wake kama msafiri na kufungua ALJAHBA kwa kila mshale? | ''Anafungua mdomo wake kama msafiri mwe nye kiu, na anakunywa kila maji atakayoyakut a … na anafungua podo lake dhidi ya kila msh ale.'' Sira 26:12<br><br>'' [21]hapo ndipo kuhani atamwapisha mwanamke kwa kiapo cha kuapiza… na akufanye wewe uwe laana … [24]kisha atamnywesha mwanamke hayo maji ya uchungu yaletayo laana; nayo maji yaletayo laana yataingia ndani yake, nayo yatageuka kuwa uchungu. .. [27]Kisha hapo atakapokwisha kumnywesha maji, ndipo itakapokuwa, kama amekuwa hali ya unajisi na kumkosa mumewe, hayo maji yaletayo laana | |

| | | |
|---|---|---|
| Je, mke anayetuhumiwa kuzini anakunywa maji machungu yaliyolaaniwa? | yatamwingia ndani yake, nayo yatakuwa uchungu, na tumbo lake litavimba, na paja lake litapooza; na huyo mwanamke atakuwa laana kati ya watu wake.'' Hesabu 5:21-27 | |
| Na kwa nini mume anayetuhumiwa kwa uzinzi naye hayanywi hayo maji machungu yaliyolaaniwa? | Uzinzi ni uhusiano wa kimapenzi usio wa kisheria unaofanyika baina ya mwanamke aliyeolewa na mwanamume asiyekuwa mumewe. Lau mwanamume aliyeoa kama atamwingilia mwanamke asiyeolewa hilo halizingatiwi kuwa ni kosa la uzinzi. Na huyo mwanamume sio mzinzi, na huyo mwanamke pia si mzinzi. Kosa la uzinzi linapatikana pale tu mwanamume (aliyeoa au hajaoa) atakapomwingilia mwanamke aliyeolewa. | |
| Je, mwanamke asiyeolewa akizini yeye si mzinifu? | Je ushahidi wa mwanamke haukubaliwi?<br><br>Sababu ni kutuhumiwa kwa Sara mke wa Ibrahimu kuwa amemuongopea Ibrahimu: ''Akakana Sara, akisema, Sikucheka, maana aliogopa. Naye akasema, Sivyo, umecheka.'' Mwanzo 18:15 | |
| Je, kutoa ushahidi ni haki ya wanaume tu? | ''Mtu akitwaa mke, akamwingilia na kumchukia [14] kisha akamshitaki mambo ya aibu kumzushia jina baya, akasema , nimemtwaa mwanamke huyu, nami nilipomkaribia sikuona kwake alama za ubikira; [15] … [20 lakini ikiwa ni kweli neno hili, la kutoonekana kwake Yule kijana alama za ubikira [21] na wamtoe nje Yule kijana mlangoni pa nyumba ya baba yake, na waume wa mji wake wampige kwa mawe hata afe; kwa vile alivyofanya upumbavu katika Israeli… '' Kumbukumbu la Torati 22:13-21 | |

| | | |
|---|---|---|
| Ni zipi sababu za kutokubaliwa ushahidi wa mwanamke? | Nadhiri ya mwanamke haikubaliwi kwa kuwa mwanamke ni miliki ya baba yake kabla ya kuolewa, na ni miliki ya mumewe baada ya kuolewa. Hesabu 30:2-15 | |
| Je, kama mume, kwa uongo, atamtuhumu mkewe kuwa hana "bikra" Je, mke atapigwa mawe licha ya uongo wa mume? | '' [46]Nanyi mtawafanya kuwa urithi kwa watoto wenu baada yenu, wawe milki yao...'' Mambo ya Walawi 25:46 sheria za mirathi: (Hesabu 27:1-11).<br><br>Swali: Je, mjane hana haki ya mirathi ya mumewe? Je, mume ndiye mrithi wa kwanza wa mwanamke baada ya umauti wake hata kama ana watoto? Je, watoto wa kike wanarithi pale ''tu'' endapo hakutakuwa na watoto wa kiume? Je, mama hana haki ya kurithi? | |
| Mpendwa msomaji: Baada ya kusoma sura ya tatu.<br><br>Je, unaamini kwamba Mungu wa Agano la Kale ni adui wa mwanamke? | | |
| Sura ya nne: Je Mungu wa Agano la Kale ana vitendo, mifananisho, sifa na maamrisho maovu? | | |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuhimiza kuipandisha roho ya Samweli kwa njia ya mapepo? | ''[7]Ndipo Sauli akawaambia watumishi wake, Nitafutieni mwanamke mwenye pepo wa utambuzi, nipate kumwendea na kuuliza kwake... [11]Ndipo yule mwanamke aliposema, Je! Ni nani nitakayekupandishia? Naye akasema, Nipandishie Samweli... [13]... Yule mwanamke akamwambia Sauli, Naona mungu anatoka katika nchi. [14]... Akajibu, Ni mzee anazuka; naye amefunikwa vazi. Basi Sauli akatambua ya kwamba ndiye Samweli mwenyewe, akainama uso wake mpaka nchi, akasujudia.'' 1 Samweli 28:7-14 | Jambo la kuwauliza/kuwaomba mashetani, wapiga ramli, makuhani na watabiri nyota limekatazwa kisheria. Na kuwakubalia yale wanayoyaeleza ni haramu zaidi na ni dhambi kubwa. Pia jambo hilo ni miongoni mwa makundi ya ukafiri. Katika kitabu cha Imamu Ahmad cha Sunani, kutoka kwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, kwa hakika amesema: (Mtu atakayemwendea kuhani na kumkubalia yale anayoyasema, basi mtu huyo ameshayakufuru |

| | | |
|---|---|---|
| | | yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad, Rehema na amani ziwe juu yake). |
| Je, atakayepandisha shetani atauliwa au atatibiwa? | ''Tena mtu mume au mtu mke aliye na pepo, au aliye mchawi, hakika atauawa; watawapiga kwa mawe; damu yao itakuwa juu yao.'' Mambo ya Walawi 20:27 | Adhkaari na Ruqiya (dua) za kisheria hutumika kutibu walopandisha shetani, kijicho na husda…. |
| Utakatifu upo wapi katika kula mavi na kunywa mikojo yao? | ''[12]Lakini yule amiri akawaambia, Je! Bwana wangu amenituma kwa bwana wako, na kwako wewe, niseme maneno haya? Hakunituma kwa watu hawa walio ukutani, ili wale mavi yao wenyewe na kunywa mkojo wao pamoja nanyi?'' Isaya 36:12, 2 Wafalme 18:27 | Muislamu ni safi, anajiepusha na kila najisi na anajisafisha nazo. (… Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanaojitakasa). Al-Baqara 222. |
| Utakatifu upo wapi katika mahari ya magovi 200 ya kutahiriwa wanaume? | ''[27]basi Daudi akainuka, akaenda yeye na watu wake, akaua katika Wafilisti watu mia mbili; na Daudi akazileta govi zao, wakampa mfalme hesabu kamili, ili awe mkwewe mfalme. Naye Sauli akamwoza Mikali, binti yake.'' 1 Samweli 18:27 | Sheria mahari ni katika uzuri wa Uislamu. Nayo ni kumtukuza mwanamke na kumpa heshima yake. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale kuadhibu kwa kutoa uchafu? | ''Nami nitatupa uchafu uchukizao juu yako, kukufanya uwe mchafu, nami nitakufanya kuwa kitu cha kutazamwa kwa dharau.'' Nahumu: 3:6<br><br>''[3] … nami nitapaka nyuso zenu mavi, naam, mavi ya sadaka zenu; nanyi mtaondolewa pamoja nayo'' Malaki 2:3 | (… Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanaojitakasa). Al-Baqara 222. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kutoa maamrisho ya kinajisi: kula mkate wa najisi "uliochafuliwa" (chapa 1885) / "mkate" Juu ya mashonde maalum ya watu?<br><br>Kumwaga damu kama mavumbi | ''[12]Nawe utakila kama mkate wa shayiri, nawe utakioka mbele ya <u>macho yao juu ya mashonde yatokayo katika mwanadamu</u>. [13]BWANA akasema, Hivyo ndivyo wana wa Israeli watakavyokula chakula chao, hali kimetiwa unajisi… [14]Ndipo nikasema, Ee Bwana MUNGU, tazama, roho yangu haikutiwa unajisi; maana tangu ujana wangu hata sasa sijala nyamafu… [15]Ndipo akaniambia, Tazama, nimekupa <u>mashonde ya ng'ombe badala ya mashonde ya mwanadamu,</u> nawe utakipika chakula chako juu ya hayo.'' Ezekieli 4:12-15 kimechapwa mwaka 1865, na kuchapwa tena 1885. | Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake amesema: (Usafi ni nusu ya imani) imepokewa na Muslim. Na muislamu lazima ausafishe mwili wake, nguo zake, na eneo lake na kila najisi. Pia hana budi ausafishe moyo wake na mifundo, husda na bughudha. Pia asafishe viungo vyake kwa kujiepusha na maasi na maovu. Na kwa kufanya hivyo, muislamu anakuwa amekusanya usafi wa nje na ndani. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: (… Hapendi Mwenyezi Mungu kukutieni katika tabu; bali |

| | | |
|---|---|---|
| na nyama kama mavi? | ''Nawe utakila kama mkate wa shayiri, nawe utakioka mbele ya macho yao juu ya mashonde yatokayo katika mwanadamu.'' Ezekieli 4:12<br><br>''… na damu yao itamwagwa kama mavumbi, na nyama yao kama mavi.'' Sefania 1:17 | anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru.) AL-Maidah 6. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ametoa ufunuo wa kuzuia kugusa maiti kwa kuwa atakayewagusa maiti atakuwa najisi kwa siku saba? | ''[11]Mtu agusaye maiti ye yote atakuwa najisi muda wa siku saba; … [14]Hii ndiyo amri, mtu afapo ndani ya hema; kila mtu aingiaye ndani ya hema hiyo, na kila mtu aliye humo hemani, atakuwa najisi muda wa siku saba… [16]Kisha mtu ye yote huko nje shambani atakayemgusa mtu aliyeuawa kwa upanga, au mzoga, au mfupa wa mtu, au kaburi, atakuwa najisi muda wa siku saba.'' Hesabu 19:11-16 | Kumuosha maiti ni lazima kwa kundi maalumu. Kwa kuwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, ameamrisha kuwaosha maiti. Baadhi ya wasomi wanaona kuwa kuosha maiti kunatengua udhu. Kama muosha atatia udhu wa kisheria na kuoga jambo hilo linakuwa ni bora kwake. Imekuja katika hadithi sahihi, kutoka kwa Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, hakika yake alikuwa anaoga kutokana na kumwosha maiti. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni mlevi na anaamrisha watu walewe pombe? Na anakunywa pombe kinguvu?<br><br>Je, katika mkono wa Mungu wa Agano la Kale mna kikombe chenye pombe inayolevya? | ''… Nanywa divai yangu na maziwa. Kaleni, rafiki zangu, kanyweni, Naam, nyweni sana, wapendwa wangu.'' Wimbo Ulio Bora 5:1<br><br>''Mpe kileo yeye aliye karibu na kupotea; Kampe divai yeye aliye na uchungu nafsini. [8] anywe akausahau umasikini wake; Asiikumbuke tena taabu yake. '' Mithali 31:6-7<br><br>''Maana mkononi mwa BWANA mna kikombe, Na mvinyo yake inatoka povu; Kumejaa machanganyiko; Naye huyamimina...'' Zaburi 75:8<br><br>"[27]… asema hivi, Nyweni, na kulewa, na kutapika, na kuanguka... [28]Tena itakuwa, kama wakikataa kukipokea kikombe kile mkononi mwako, wanywe, ndipo utakapowaambia, BWANA wa majeshi asema hivi, Lazima mtakunywa.'' Yeremia 25:27-28 | (Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu; na kutazamia kwa mishale ya kupiga ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (ni) katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu (kutengenekewa). Hakika shetani anataka kukutilieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na (kukuzuilieni) kuswali. Basi je, mtaacha (mabaya hayo)? AL-Maidah 90 – 91. Kutoka kwa Ibnu Omari, Mungu amuwie radhi yeye na baba yake amesema, Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake amesema: "Mwenyezi Mungu imeilani pombe, na anayeinywa, |

<table>
<tr>
<td></td>
<td>''Ndipo Bwana alipoamka kama aliyelala usingizi, Kama shujaa apigaye kelele sababu ya mvinyo;'' Zaburi 78:65<br><br>''Wao hupapasa gizani pasipokuwa na mwanga, N aye huwafanya kupepesuka kama vile mlevi.'' Ayu bu 12:35</td>
<td>na anayewanywesha watu, na anayeiuza, anayeinunua, na anayeikamua (itengeneza), na kinachokamuliwa, na anayeibeba, na anayebebewa". Sunanu Abuu Daudi 3189.</td>
</tr>
<tr>
<td>Je, miongoni mwa kushabihishwa kwa Mungu wa Agano la Kale ni kuwa yeye ni kama: Simba dume, simba jike, chui na dubu?<br><br>Na nondo, ubovu, na mwana-simba?</td>
<td>''Basi nimekuwa kama simba kwao; kama chui nitavizia njiani; [8]nitakutana nao kama dubu aliyenyang'anywa watoto wake; nami nitararua nyama ya mioyo yao; na huko nitawala kama simba; ...'' Hosea 13:7-8<br><br><table><tr><td></td><td></td><td></td></tr><tr><td>Simba</td><td>Chui</td><td>Dubu</td></tr></table><br>''Kwa sababu hiyo mimi nimekuwa kama nondo kwa Efraimu, nimekuwa kama ubovu kwa nyumba ya Yuda.'' Hosea 5:12<br><br>''Maana mimi nitakuwa kama simba kwa Efraimu, na kama mwana-simba kwa nyumba ya Yuda...'' Hosea 5:14</td>
<td>Hakuna katika Quran wala katika hadithi sahihi kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amejifanyia mwili wa mti au moto au mtu (Masihi, Budha, Krishnaa ...) au mnyama (ng`ombe, panya, simba...).<br><br>(Ni nani dhalimu mkubwa kuliko Yule amtungiaye uongo Mwenyezi Mungu...) Al-Anam 93.<br><br>(... Ni neno kubwa hilo litokalo katika vinywa vyao. Hawasemi ila uwongo tu.) Kahf 5.</td>
</tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| |  mwana-simba<br> nondo, ubovu | |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kupumzika (jambo ambalo ni muhimu kwa mwenye kuchoka) kisha anapunga upepo kwa raha kabisa. | ‘’Ni ishara kati ya mimi na wana wa Israeli milele; kwani kwa siku sita BWANA alifanya mbingu na nchi, akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika.’’ Kutoka 31:17<br><br>[2]Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. [3]Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe…’’ Mwanzo 2:2-3<br><br>‘’BWANA asema hivi… Na mahali pangu pa kupumzikia ni mahali gani?’’ Isaya 66:1 | (Na hakika tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yao katika nyakati (siku) sita, wala hayakutugusa machovu. Basi vumilia kwa hayo wasemayo…) Qaf 38 – 39. |
| Utakatifu upo wapi katika kuvunja ahadi? | ‘’… na kulivunja agano langu pamoja nao; kwa kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wao;’’ Mambo ya Walawi 26:44 | (…Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake…) Ar-um 6. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kucheza mieleka?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale ni dhaifu na kutoa Baraka baada ya kucheza mieleka? | ''[24]Yakobo akakaa peke yake; na mtu mmoja akashindana naye mweleka hata alfajiri. [25]Naye alipoona ya kuwa hamshindi, alimgusa panapo uvungu wa paja lake; ukateguka uvungu wa paja la Yakobo alipokuwa akishindana naye. [26]Akasema, Niache, niende, maana kunapambazuka. Akasema, Sikuachi, usiponibariki. [27]Akamwuliza, Jina lako n'nani? Akasema, Yakobo. [28]Akamwambia, Jina lako hutaitwa tena Yakobo, ila Israeli, maana umeshindana na Mungu, na watu, nawe umeshinda. [29]Yakobo akamwuliza, akasema, Niambie, tafadhali, jina lako? Akasema, Kwa nini waniuliza jina langu? Akambariki huko.'' Mwanzo 32:24-29 | Yakubu amani iwe juu yake, alikuwa ni miongoni mwa manabii wa Mwenyezi Mungu, na ni miongoni mwa wenye matendo mema, elimu yenye manufaa, nguvu ya kufanya ibada na muono wa mbali. (Na haikuwa kwa mtu kwamba, Mwenyezi Mungu anasema naye ila kwa ilhamu (anayotiwa moyoni mwake) au kwa nyuma ya pazia (la kumsikilizisha sauti inayotokana na Mwenyezi Mungu) au humtuma Mjumbe, (Jibrili); naye humfunulia (humletea wahyi) kiasi anachotaka kwa idhini Yake; bila shaka Yeye ndiye aliye juu, Mwenye hikima.) Ash-shuura 51 |
| Je, miongoni mwa vitendo vya Mungu wa Agano la Kale ni kuwa anawezekana kuonwa na kuongea naye uso kwa uso?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale anatembea mchana katika nguzo ya mawingu na usiku katika nguzo ya moto?<br><br>Je, kuna kupingana baina ya maandiko: ya | Inawezekana kumuona Mungu: ''Naye BWANA akasema na Musa uso kwa uso...'' Kutoka 33:11<br><br>''... maana alisema, Nimeonana na Mungu uso kwa uso...'' Mwanzo 32:30<br><br>''BWANA akamtokea Ibrahimu karibu na mialoni ya Mamre...'' Mwanzo 18:1<br><br>''... nao wakamwona Mungu, wakala na kunywa.'' Kutoka 24:11<br><br>''BWANA akamtokea, akasema...'' Mwanzo 26:2<br><br>''Mungu akamjia Balaamu usiku, akamwambia...'' Hesabu 22:20 | Haiwezekani kumuona Mungu hapa duniani: (Macho hayamfikii (kumwona), bali Yeye anayafikia macho (kuyaona na kuwaona hao wenye macho). Naye ni mwenye kujua yaliyofichikana na yaliyodhahiri). An-am 103.<br><br>Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, ameeleza: kuwa hakuna atakayemuona Mola wake mpaka afe, imetolewa na Muslim katika sahihi yake. |

| | | |
|---|---|---|
| uwezekano wa kumuona Mungu… na Haiwezekani kumuona Mungu?! | ''Ilikuwa walipokuwa njiani mahali pa kulala, BWANA akakutana naye...'' Kutoka 4:24<br><br>''BWANA akashuka katika nguzo ya wingu…'' Hesabu 12:5<br><br>''BWANA naye akawatangulia mchana ndani ya wingu mfano wa nguzo … na usiku, ndani ya moto mfano wa nguzo…'' Kutoka 13:21<br><br>''Lakini Yona akaondoka akimbilie Tarshishi, apate kujiepusha na uso wa BWANA...'' Yona 1:3<br><br>Haiwezekani kumwona Mungu: Je, kuna kupingana? ''Hakika wewe u Mungu ujifichaye nafsi yako, Ee Mungu wa Israeli, Mwokozi.'' Isaya 45:15<br><br>''Kisha akasema, Huwezi kuniona uso wangu, maana mwanadamu hataniona akaishi.'' Kutoka 33:20 | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni dhalimu, mwovu na sio mwadilifu ndio sababu akamwacha mama kwa sababu ya madhambi ya watoto wake, ili aongeze | ''BWANA asema hivi, Iko wapi hati ya talaka ya mama yenu, ambayo kwa hiyo naliachana naye? Au nimewauza ninyi kwa nani katika watu wanaoniwia? Ninyi mliuzwa kwa sababu ya maovu yenu; tena mama yenu ameachwa kwa sababu ya makosa yenu.'' Isaya 50:1<br><br>''Yeye anipondaye kwa dhoruba, Na kuziongeza jeraha zangu pasipokuwa na sababu.'' Ayubu 9:17 | (Sema: "Je, nishike Mola mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na hali yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye Mola wa kila kitu?" Wala nafsi yo yote haichumi (ubaya) ila ni juu yake; (hatalipwa kiumbe mwingine kwa ubaya wake). Wala mbebaji (mizigo yake ya dhambi) hatabeba mizigo ya mwingine (kumsaidia). Kisha marejeo yenu n yote ni kwa Mola wenu. Naye atakuambieni yale |

| | | |
|---|---|---|
| majeraha bila ya sababu? | " [6]... [7]Tazama, nalia, Udhalimu, lakini sisikiwi; Naulilia msaada, wala hapana hukumu." Ayubu 19:6-7 | mliyokuwa mkihitalifiana.) An-am 164. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni dhalimu ndio sababu anawanyima vilema kuingia katika makutano ya Mungu? | "[1]... Nitanena kwa uchungu wa roho yangu. [2]Nitamwambia Mungu, Usinihukumie makosa; Nionyeshe sababu ya wewe kushindana nami. [3]Je! Ni vema kwako wewe kuonea...?" Ayubu 10:1-3 | (Anayefanya mema anajifanyia (mwenyewe) nafsi yake, na mwenye kutenda ubaya ni juu (ya nafsi) yake (vilevile); na Mola wako si dhalimu (hata kidogo) kwa waja (wake). Ha Mym Sajdah 46. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni dhalimu, ndio sababu haziingizi katika makutano ya mungu koo za Peresi na Boazi mpaka kizazi cha kumi? | "Aliyejeruhika konde, au aliye katika tupu yake, asiingie mtu huyo katika mkutano wa BWANA." Kumbukumbu la Torati 23:1<br><br>" [18]Kwa kuwa mtu awaye yote aliye na kilema hatakaribia; mtu kipofu, au kiwete, au mtu aliye na pua iliyoharibika, au aliye na kitu kilichozidi vimpasavyo mwili, [19]au mtu aliyevunjika mguu, au aliyevunjika mkono, [20]au aliye na kijongo, au aliye kibeti, au aliye na kilema cha jichoni, au aliye na upele, au mwenye buba, au aliyevunjika mapumbu;... [23]... wala asikaribie madhabahu, kwa sababu ana kilema; ili kwamba asipanajisi patakatifu pangu; kwa kuwa mimi ndimi BWANA niwatakasaye." Mambo ya Walawi 21:18-23<br><br>"Mwana wa haramu asiingie katika mkutano wa BWANA; hata kizazi cha kumi asiingie aliye wake katika mkutano wa BWANA." Kumbukumbu la Torati 23:2 Daudi na Bath-sheba walikuwa ni wazinzi. (2 Samweli 11:3-5). Daudi katika kizazi cha kumi anatokana na (mwana wa haramu) Faariswa. Naye katika kizazi cha nne ni (mwana wa zinaa) wa Boazi. Je, Daudi haingii katika mkutano wa Mungu? (Kumbukumbu la Torati 23:2) Kwa nini haikutekelezwa sheria ya Musa kwa Daudi na | (Basi adhabu kali itawathibitikia wanaoandika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: "Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu." (Wanasema uwongo huo) Ili wachukue thamani ndogo ya kilimwengu. Basi ole wao kwa yale waliyoyaandika kwa mikono yao (wakasingizia kuwa ya Mungu). Na ole wao kwa yale wanayoyachuma.) Al Baqara 79.<br><br>Mwenyezi Mungu Mtukufu Aliyetukuka ni mwadilifu na si dhalimu. Naye Mtukufu ndiye mwenye kusema: ("Kauli yangu haibadilishwi kwangu, wala Mimi siwadhulumu waja wangu.") Qaf 29.<br><br>Vilevile, Naye ndiye mwenye kusema: ("(Anayefanya mema anajifanyia (mwenyewe)nafsi yake, na mwenye kutenda ubaya ni juu (ya nafsi) yake (vilevile); na Mola wako si dhalimu (hata |

| | | |
|---|---|---|
| | Bath-sheba? (Kutoka 20:14), (Kumbukumbu la Torati 5:18), (Mambo ya Walawi 18)<br>________________________________<br>''Mwamoni wala Mmoabi wasiingie katika mkutano wa BWANA; wala hata kizazi cha kumi mtu wao asiingie katika mkutano wa BWANA milele;'' Kumbukumbu la Torati 23:3 Ruthu Mmoabi (ni kizazi cha haramu (zinaa) cha Lutu na binti yake mkubwa). Mwanzo 19:30-38, Ruthu 4:17. Na Mwamoni (ni kizazi cha haramu cha Lutu na binti yake mdogo). Mwanzo 19:30-38, 1 Wafalme 14:21. Suleimani katika kizazi cha tano ni (mtoto wa zinaa) wa Boeri. Je, Suleimani haingii katika makutano ya BWANA? Kumbukumbu la Torati 23:3<br>________________________________<br>Ruthu Mmoabi na Neema Mwamoni wao ni mabibi wa Yesu Masihi. Yesu Masihi alikuwa ni kizazi Ruthu Mmoabi na Neema Mwamoni (Mathayo 1:1-16). Je, Yesu Masihi haingii katika makutano ya BWANA (milele)?<br><br>''…, kwa kumpa mafungu mawili katika vyote alivyo navyo; kwa maana ndiye mwanzo wa nguvu zake; haki ya mzaliwa wa kwanza ni yake yeye.'' Kumbukumbu la Torati 21:15-17 | kidogo) kwa waja (wake). Ha Mym Sajdah 46. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni dhalimu na mbaguzi, ndio maana anampa mtoto kifungua mimba mafungu mawili?<br><br>Je, yeye ni dhalimu na | '' [10]Kwa hiyo akamwambia Ibrahimu, Mfukuze mjakazi huyu na mwanawe, maana mwana wa mjakazi hatarithi pamoja na mwanangu, Isaka. [11]Na neno hilo lilikuwa baya sana machoni pa Ibrahimu, kwa ajili ya mwanawe. [12]Mungu akamwambia Ibrahimu, Neno hili lisiwe baya machoni pako, kwa ajili ya huyo mwana, na huyo mjakazi wako. Kila akuambialo Sara, sikiza sauti yake...'' Mwanzo 21:10-12 | Katika hadithi inayosimuliwa na Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kutoka kwa Mola wake Mtukufu aliyetukuka, amesema: (Enyi waja wangu, hakika mimi nimeharamisha dhulma kwa nafsi yangu na nikaifanya hiyo dhulma iwe haramu baina yenu hivyo msidhulumu. Enyi waja wangu, nyote nyinyi mmepotea ila Yule nitakayemwongoa. Hivyo takeni kuongoka kutoka kwangu nami |

| | | |
|---|---|---|
| mbaguzi, ndio maana anakubali dhulma ya Ibrahimu wakati wa kugawa mirathi na kumnyima Ismaili na ndugu zake?!<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale ni dhalimu, na ndio maana anamuadhibu aliyepatwa na ugonjwa wa ngozi nayo ni ukoma na kumwita: (najisi, najisi) na kuziunguza nguo zake na kubomoa nyumba yake kwa sababu mtu huyo ni najisi?! | ‘’ [5]Ibrahimu akampa Isaka yote aliyokuwa nayo. [6]Lakini wana wa masuria aliokuwa nao Ibrahimu, Ibrahimu akawapa zawadi, naye akawaondoa katika mahali alipokaa Isaka mwanawe, wakati wa uhai wake, waende pande za mashariki, mpaka nchi ya Kedemu.’’ Mwanzo 25:5-6<br><br>‘’ [45]Kisha mwenye ukoma aliye na pigo ndani yake, nguo zake zitararuliwa, na nywele za kichwa chake zitaachwa wazi, naye atafunika mdomo wake wa juu, naye atapiga kelele, Ni najisi, ni najisi.’’ Mambo ya Walawi 13:45<br><br>‘’Na atalichoma moto vazi hilo, kwamba ni lililofu mwa au kwamba ni lililosokotwa, kama ni la sufi, au la kitani, au kitu chochote cha ngozi, ambacho kina hilo pigo ndani yake; kwa maana, ni ukoma unaokula; vazi hilo litachomwa moto.’’ Mambo ya Walawi 13:52<br><br>‘’ [44] Ndipo kuhani ataingia ndani na kuangalia, na tazama, likiwa pigo limeenea ndani ya hiyo nyumba, ni ukoma unaokula hiyo nyumba; ni katika unajisi. [45] naye ataibomoa nyumba, mawe yake, na miti yake, na chokaa yote ya hiyo nyumba; naye atavichukua vyote nje ya mji hata mahali palipo na uchafu.’’ Mambo ya Walawi 14:44-45 | nitawaongoa. Enyi waja wangu, nyote nyinyi mna njaa ila nitakayemlisha. Niombeni chakula nami nitawalisha. Enyi waja wangu, nyote nyinyi mpo uchi ila niliyemvisha. Hivyo niombeni nikuvalisheni nami nitawavalisha. Enyi waja wangu, hakika nyinyi mnafanya makosa usiku na mchana, nami nasamehe madhambi yote. Hivyo niombeni msamaha nitawasamehe. Enyi waja wangu, hakika nyinyi hamtofikia kunidhuru na mkanidhuru, na wala hamtofikia kuninufaisha mkaninufaisha. Enyi waja wangu, lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, wanadamu wenu na majini wenu wote wangelikuwa katika moyo mmoja wa mcha Mungu zaidi kati yenu, hilo lisingezidisha chochote katika ufalme wangu. Enyi waja wangu, lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, wanadamu wenu na majini wenu wote wangelikuwa katika moyo wa mwovu zaidi kati yenu, hilo lisingelipunguza chochote katika milki yangu. Enyi waja wangu, lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, wanadamu wenu na majini wenu wote mngelisimama upande mmoja wa juu na kuniomba nami nikampa kila mtu atakachoniomba, hilo lisingepunguza chochote katika kile nilicho nacho ila kama inavyopunguza sindano inapoingizwa baharini. Enyi waja wangu, hakika si vinginevyo, hayo ni matendo yenu, nimeyadhibiti hesabu zake kwa ajili yenu, kisha |

| | | |
|---|---|---|
| | | nakulipeni kikamilifu kwa matendo hayo. Hivyo atakayepata heri na amshukuru Allah. Na atakayepata kisichokuwa hicho asimlaumu yoyote ila nafsi yake.) Imetolewa na Muslimu. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anahukumu katikati ya miungu yote? | ''Mungu asimama katika kusanyiko la Mungu; Katikati ya miungu anahukumu.'' Zaburi 82:1<br><br>''Kwa kuwa BWANA ni Mungu mkuu, Na Mfalme mkuu juu ya miungu yote.'' Zaburi 95:3 | Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (... hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah, ni mmoja tu, hana mshirika, ufalme ni wake, na sifa njema zote ni zake. Naye ni muweza juu ya kila kitu....). Bukhariyu na Muslimu. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ana upande wa "nyuma"? | ''nami nitaondoa mkono wangu, nawe utaniona nyuma yangu, bali uso wangu hautaonekana.'' Kutoka 33:23 | (Hakuna chochote mfano wake; naye ni mwenye kusikia, mwenye kuona.) As-shuura 11. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kunusa ubani? | ''[37]Na uvumba utakaofanya, hamtajifanyia uvumba wenye viungo sawasawa na uvumba huo; utakuwa kwenu mtakatifu kwa ajili ya BWANA. [38]Mtu ye yote atakayefanya mfano wa huo, ili kuunusa, mtu huyo atakatiliwa mbali na watu wake.'' Kutoka 30:37-38 | (Ameepukana Mola wako, Mola mwenye enzi, na yale wanayomsifu (nayo makafiri). As-saaffat 180. |
| Je, Mungu anafurahia kwa kuridhika na harufu ya vinavyoungua? | ''BWANA akasikia harufu ya kumridhisha...'' Mwanzo 8:21<br><br>'' ... kwa njia ya moto, ya harufu ya kupendeza kwa BWANA.'' Mambo ya Walawi 1:9<br><br>''... na kuyateketeza mafuta yao kuwa sadaka iliyosongezwa kwa BWANA kwa moto, iwe harufu ya kupendeza.'' Hesabu 18:17 | (Mwenyezi Mungu yu mbali na sifa wanazompa.) As-saaffat 159. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kutoa ahadi na viapo kwa manabii zake baada ya hao Manabii kutoa madhabahu, sadaka za kuteketezwa madhabahuni na sehemu za kuchomea? | ‘’ [20]Nuhu akamjengea BWANA madhabahu; akatwaa katika kila mnyama aliye safi, na katika kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu. [21]BWANA akasikia harufu ya kumridhisha; BWANA akasema moyoni, Sitailaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu...’’ Mwanzo 8:20-21.<br><br>‘’BWANA akamtokea Abramu, akasema, Uzao wako nitawapa nchi hii. Naye huko akamjengea madhabahu BWANA aliyemtokea.’’ Mwanzo 12:7<br><br>‘Siku ile BWANA akafanya agano na Abramu, akasema, Uzao wako nimewapa nchi hii, kutoka mto wa Misri mpaka huo mto mkubwa, mto Frati.’’ Mwanzo 15:18 | (Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adamu na Nuhu na kizazi cha Ibrahimu na kizazi cha Imrani (Babaake Musa; na Imrani mwingine aliye baba yake Maryamu) juu ya walimwengu wote (wa zama zo). Aali Imran 33.<br><br>Ibrahimu, amani iwe juu yake alibashiriwa kuwa atapata mtoto mpole (Ismaili) naye ndiye mchinjwa. Na Ibrahimu akabashiriwa kupata mtoto mjuzi (Is-haqa). Allah akasema: (Na tukambashiria (kumzaa) Is-haka, (mtoto wake wa pili). Nabii miongoni mwa watu wema (kabisa). As-saaffat 112. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale hajui kwamba Ismaili alikuja kabla ya Is-haqa?<br><br>Je, Mungu amejua “sasa hivi” kuwa Ibrahimu anamuogopa yeye? | ‘’ [9]... kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni... [12]Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee. [13]Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yak ... Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe... [16]... asema BWANA... [17]katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao; [18]na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu.’’ Mwanzo 22:9-18 | (... na wakamtolea habari nzuri za (kuwa atazaa) mtoto mwenye ilimu.) Adh-dhaariyat 28.<br><br>Mtoto wa “pekee” aliyemtangulia Is-haka ni Ismaili amani iwe juu yake. Na ibrahimu amani iwe juu yakeakabashiriwa baada ya hapo kuwa Is-haka atakuwa Mtume yeye na Yakubu. (Na mkewe (Ibrahimu – Bibi Sara) alikuwa kasimama wima (anawatumika); akacheka (aliposikia hivyo). Basi tukampa habari njema ya (kuwa watazaa mtoto wamwite) Is-haqa na baada ya Is-haqa (watapata mjukuu wamwite) Yaakubu.) Hud 71. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale | ‘’ [39]Gideoni akamwambia Mungu, Hasira yako isiwake juu yangu, nami nitasema mara hii tu; nakuomba, nijaribu kwa ngozi hii mara hii tu; sasa | Allah anawatahini waja waje: (Ili Mwenyezi Mungu apate kuwapambanua walio wabaya na |

| | | |
|---|---|---|
| anajaribiwa na Gideoni? | ngozi tu na iwe kavu, na uwe umande juu ya nchi yote. [40]Mungu akafanya hivyo usiku ule; maana ile ngozi tu ilikuwa kavu, napo palikuwa na umande juu ya nchi yote.'' Waamuzi 6:39-40 | walio wazuri na kuwaweka wabaya juu wabaya wengine na kuwarundika wote kuwatupa katika Jahanamu...). Al-Anfal 37. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kutokuzijua nyumba za wana wa Israili ila baada ya kuona damu? | ''Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lo lote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri.'' Kutoka 12:13<br><br>''Kwa kuwa BWANA atapita ili awapige hao Wamisri; na hapo atakapoiona hiyo damu katika kizingiti cha juu, na katika ile miimo miwili, BWANA atapita juu ya mlango, wala hatamwacha mwenye kuharibu aingie nyumbani mwenu kuwapiga ninyi.'' Kutoka 12:23 | (Na miongoni mwao kuna baadhi yao wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) kitabu ili mpate kuyafikiri (maneno) yao hayo kuwa ni ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu); na wanasema: "Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu", na hali hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu; na wanamsingizia Mwenyezi Mungu uwongo na hali wanajua (kuwa huo ni uwongo). Aali Imran 78. |
| Je, miongoni mwa matendo ya Mungu wa Agano la Kale ni kwamba yeye anateremka ili yeye mwenyewe akamuue Musa, kisha anaachana naye baada ya kuona damu ya govi la kutahiriwa? | BWANA alitangaza kuwa yeye mwenyewe atateremka ili kumuua Musa asubuhi na mapema kwa sababu Musa alikataa kumtahiri mwanawe... lakini mkewe bi Sipora alilikata govi la mtoto kwa kisu alichokuwa nacho na kuchukua damu na kuipakaza katika miguu ya Musa, kisha Sipora akapiga kelele '' Hakika wewe u bwana harusi wa damu kwangu mimi. BWANA akamwacha mtoto. Ndipo Sipora akasema: bwana harusi wa damu kwa ajili ya kutahiri.'' ''[24]Ilikuwa walipokuwa njiani mahali pa kulala, BWANA akakutana naye akataka kumwua. [25] Ndipo Sipora akashika jiwe gumu na kuikata govi ya zunga la mwanawe, na kuibwaga miguuni pake akasema. Hakika wewe u bwana harusi wa damu kwangu mimi. [26]Basi akamwacha. Ndipo huyo mkewe akanena, U bwana harusi wa damu wewe, kwa ajili ya kutahiri.'' Kutoka 4:24-26 | Haiwezekani kumuona Mungu: (Macho hayamfikii (kumwona), bali Yeye anayafikia macho (kuyaona na kuwaona hao wenye macho). Naye ni mwenye kujua yaliyofichikana na yaliyodhahiri). An-am 103.<br><br>("Kauli yangu haibadilishwi kwangu, wala Mimi siwadhulumu waja wangu.") Qaf 29. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaitenga nafsi ya mwanamume govi? | ''Na mwanamume mwenye govi asiyetahiriwa nyama ya govi lake, mtu yule atatengwa na watu wake; amelivunja agano langu.'' Mwanzo 17:14 | (Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano. Hakika Mwenyezi Mungu anajua, na nyinyi hamjui (lolote). An nahl 74. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa katika hali na kujifanyia mwili na kuchanganyika na viumbe wake (Ijulikane kuwa viumbe wote wana najisi na uchafu?)<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale ana makazi anayoishi yeye mwenyewe? | ''Mwimbieni BWANA akaaye Sayuni...'' Zaburi 9:11<br><br>''... kwa maana BWANA ndiye akaaye Sayuni.) Yoeli 3:21<br><br>''Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao.'' Kutoka 25:8<br><br>''Ndipo Sulemani akanena, BWANA alisema ya kwamba atakaa katika giza nene.'' 1 Wafalme 8:12<br><br>''Ndipo Sulemani akanena, BWANA alisema ya kwamba atakaa katika giza nene.'' 2 Mambo ya Nyakati 6:1<br><br>''Toka mbinguni BWANA huchungulia... [14]Toka mahali pake aketipo Huwaangalia wote wakaao duniani.'' Zaburi 33:13-14<br><br>''... naam, usikie toka makaoni mwako, toka mbinguni...'' 2 Mambo ya Nyakati 6:21<br><br>''Lakini Mungu je? Atakaa kweli kweli juu ya nchi? Tazama, mbingu hazikutoshi, wala mbingu za mbingu; sembuse nyumba hii niliyoijenga!'' 1 Wafalme 8:27 na 2 Mambo ya Nyakati 6:18 | Mwenyezi Mungu Mtukufu amestawi katika kiti chake cha enzi juu mbingu saba, pia yeye ndiye wa juu kwa viumbe vyake vyote. Mwenyezi Mungu ni mwenye kutofautiana na viumbe vyake, yeye ni mtukufu aliyetukuka. Yeye si hali, wala mwili, wala hajachanganyika katika viumbe vyake. Yeye ndiye mtukufu aliyetukuka. Yupo juu ya viumbe vyake, utakatifu ni wake. Na Mwenyezi Mungu yu si kwa elimu yake na usikivu wake na uoni wake na uwezo wake na nguvu na kukizunguka kwake kila kitu na sio kwa dhati yake.<br><br>(Ametakasika Mwenyezi Mungu na ameepukana, na hayo wayasemayo kwa uepukano mkubwa (kabisa). Bani Israil 43. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anatembea? | '' [3]Kwa maana, angalieni, BWANA anakuja akitoka mahali pake, naye atashuka, na kupakanyaga mahali pa dunia palipoinuka...?'' Mika 1:3-5 | (Na ni nini dhana ya wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo...) Yunus 60. |

| | | |
|---|---|---|
| | ''Kisha wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini…'' Mwanzo 3:8 | |
| Je, miongoni mwa matendo ya Mungu wa Agano la Kale ni kuwaadhibu watu na kuwachafulia lugha zao. (siasa ya wagawe uwatawale)? | '' [4]Wakasema, Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni… [5]BWANA akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu. [6]BWANA akasema, Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya… [7]Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao.'' Mwanzo 11:4-7 | (Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja; Adamu) na (yule Yule) mwanamke (mmoja; Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi; siyo mkejeleane). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni Yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote). Al-Hujurat 13. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa na hofu?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale anahofia magari ya chuma?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale anaogopa Adamu asije akala mti wa uzima? | ''BWANA alikuwa pamoja na Yuda; naye akawafukuza watu waliokaa katika nchi ya milimani; asiweze kuwafukuza hao waliokaa katika hilo bonde, kwa kuwa wao walikuwa na magari ya chuma.'' Waamuzi 1:19<br><br>'' [22]BWANA Mungu akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele; [23]kwa hiyo BWANA Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa.'' Mwanzo 3:22-23 | (… Na hakika wanaomwogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wale wataalamu (wanavyuoni). Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Msamehevu.) Fatir 28.<br><br>Hapa mtenda ni: (Wataalamu) kwani wao ndio watu wa kumcha na kumwogopa Mwenyezi Mungu. Na jina tukufu (Allah): ni mtendwa aliyetangulia.<br><br>(Na Mayahudi na Wakristo wanasema: "Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na wapenzi wake." Sema: "Basi kwa nini anakuadhibuni kwa ajili ya dhambi zenu? Bali nyinyi ni watu (tu) katika aliowaumba. Humghufiria |

| | | |
|---|---|---|
| | | (humsamehe) amtakaye (anapotubia) na humuadhibu amtakaye (asipotubia)…) Al-Maidah 18. |
| Je, miongoni mwa matendo ya Mungu wa Agano la Kale ni kulala, kuzinduka, kuamka na kutanabahi? | ''Ndipo Bwana alipoamka kama aliyelala usingizi, Kama shujaa apigaye kelele sababu ya mvinyo'' Zaburi 78:65<br><br>''Amka, Bwana, mbona umelala? Ondoka, usitutupe kabisa.'' Zaburi 44:23<br><br>''Uamke, uwe macho…'' Zaburi 35:23<br><br>''… kwa maana ameamka ..'' Zakaria 2:13 | (Mwenyezi Mungu hakuna mola ila Yeye, (na) ndiye Mwenye uhai wa maisha, Msimamia kila jambo. Kusinzia hakumshiki wala kulala. Ni vyake (peke yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika…) Al-Baqarah 255. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ana wana?<br><br>Je, wana wa mungu wana cheo cha uungu?<br><br>Ni nani huyo mwana wa kwanza wa mungu, je, ni Israili au Afraymu au Yesu Kristo?<br><br>Na lau kama nafsi ya pili ya mungu ndio Mwana wa pekee wa Mungu, | Yakobo (Israeli): ''… Israeli ni mwanangu mimi…mzaliwa wa kwanza wangu.'' Kutoka 4:22<br><br>Suleimani: ''Mimi nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwanangu…'' 2 Samweli 7:14<br><br>Efraimu: ''… na Efraimu ni mzaliwa wa kwanza wangu.'' Yeremia 31:9<br><br>Daudi: ''… Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa.'' Zaburi 2:7<br><br>Watoto wa BWANA: ''… na wanawe na binti zake.'' Kumbukumbu la Torati 32:19 | (Na (makafiri) husema: "(Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema amejifanyia mtoto." Bila shaka mmeleta jambo lichukizalo kabisa (kwa kusema hivyo). Zinakaribia mbingu kutatuka kwa (tamko) hilo na ardhi kupasuka na milima kuanguka (ikakatika) vipandevipande. Kwa kule kudai kuwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema ana mtoto. Wala haiwi kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema kuwa na mtoto. Hakuna yoyote aliyomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa (Mwenyezi Mungu), Mwingi wa rehema hali ya kuwa ni mtumwa (wake). Maryam 88 – 93.<br><br>(Na kiwaonye wale wanaosema: "Mwenyezi Mungu amejifanyia mtoto." Wao hawana ilimu juu ya |

| | | |
|---|---|---|
| ni nani hasa hao wana wa Mungu? | ''Ninyi mmekuwa wana wa BWANA, Mungu wenu...'' Kumbukumbu la Torati 14:1<br><br>''wana wa Mungu...'' Mwanzo 6:2<br><br>''Mpeni BWANA, enyi wana wa Mungu...'' Zaburi 29:1<br><br>''...Ni nani afananaye na BWANA miongoni mwa malaika?'' Zaburi 89:6<br><br>''... Na wana wote wa Mungu walipopiga kelele...'' Ayubu 38:7<br><br>''... wana wa Mungu walipokwenda...'' Ayubu 2:1 | (jambo) hili ila wanajisemea tu). Ni neno kubwa hilo litokalo katika vinywa vyao. Hawasemi ila uwongo tu.) Kahf 4 – 5. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale amemuumba mtu kwa mfano na sura yake? | '' [26]Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu... [27]Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.'' Mwanzo 1:26-27 | (Hakuna chochote mfano wake; naye ni mwenye kusikia, mwenye kuona.) As-shuura 11. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaamrisha kusulubiwa kwa watu saba wasio na kosa ili kuomba mvua inyeshe? | '' [1]Kulikuwa na njaa siku za Daudi muda wa miaka mitatu... naye Daudi... akawatwaa hao wana wawili wa Rispa, binti Aya, aliomzalia Sauli, Armoni na Mefiboshethi; na wana watano wa Merabu binti Sauli... akawatia mikononi mwa Wagibeoni, nao wakawatundika mlimani mbele za BWANA, nao wakaangamia wote saba pamoja; wakauawa... hata waliponyeshewa mvua toka mbinguni...'' 2 Samweli 21:1-14 | Swala ya kuombea mvua inyeshe ni suna iliyosisitizwa pale watu wanapokuwa na shida ya mvua kwa sababu ya ukame wa ardhi. Kutoka kwa Abdallah bin Zaidi amesema: Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake aliomba mvua akaswali rakaa mbili na kugeuza shuka yake. Bukhariyu na Muslimu. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale “anadhalilishwa/ anadharauliwa”?<br><br><br><br><br>Je, Mungu “anadhalilishwa” ili asulubiwe?<br><br>Je upande wa kiungu umeuacha upande wa kibinadamu usulubiwe peke yake? | ‘’BWANA akamwuliza Musa, Je! Watu hawa watanidharau hata lini? Wasiniamini hata lini? Nijapokuwa nimefanya ishara hizo zote kati yao.’’ Hesabu 14:11<br><br>---<br><br>Swali: Je, Mungu wa Agano la Kale na Jipya ‘’ “anadhalilishwa’’ mpaka yeye mwenyewe anateremka ardhini ili asamehe madhambi yote. Akajivika mwili wa mwanadamu, nafsi ya pili… na hatimaye Mungu akafanyia udhalilishaji (nafsi ya pili) wakamvua nguo, wakamtemea mate, wakampiga kichwani na kumsulubu? Je, nafsi ya pili wakati akiwa msalabani ‘’anaadhibika na kuumia’’ (ijulikane kuwa uungu na ubinadamu havitengani hata kidogo) huku akisema: ‘’Mungu wangu! Mungu wangu! Mbona waniacha’’ Hayo ni kwa kuwa nafsi ya kwanza (Baba) alimwacha mwanawe aadhibike, apate maumivu na kuokoa? Je, wakristo wanakana kifo cha ule upande wa uungu kwa kuwa Mungu hafi kwa maandiko: ‘’… Kama Mimi niishivyo milele.’’ Kumbukumbu la Torati 32:40 ‘’Bali BWANA ndiye Mungu wa kweli; Ndiye Mungu aliye hai, Mfalme wa milele…’’ Yeremia 10:10 ‘’Ee BWANA, Mungu wangu, mtakatifu wangu, wewe si wa milele? Hatutakufa…’’ Habakuki 1:12 | (… hakika Mwenyezi Mungu bila shaka ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda). Al-Hajj 74.<br><br>Na Masihi Isa mwana wa Maryamu, amani iwe juu yake, yeye ni mtume wa Allah. Hajauawa wala hajasulubiwa: (… hali hawakumwua wala hawakumsulubu, bali walibabaishiwa (mtu mwingine wakamdhani nabii Isa…). An-nisaa 157.<br><br>Alinyanyuliwa na Allah kupelekwa mbinguni kwa mwili wake na roho yake. Naye mpaka sasa yu hai huko mbinguni. Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, amesema kuhusiana na kushuka kwa Isa katika zama za mwisho: [Hakika inaogopewa kwamba atakushukieni mwana wa Maryamu akiwa ni imamu mwadilifu na hukumu adilifu. Atavunja msalaba na kumuua nguruwe….} Bukhariyu na Muslimu. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale hawezi kuchagua Mitume wazuri hivyo anamtuma Suleimani ili amkufuru Mungu na kuiabudu miungu mingine? | ‘’ [5]… Sulemani akamfuata Ashtorethi, mungu mke wa Wasidoni na Milkomu, chukizo la Waamoni. [6]Sulemani akafanya yaliyo mabaya machoni pa BWANA, wala hakumfuata BWANA kwa utimilifu, kama Daudi baba yake. [7]Sulemani akamjengea Kemoshi, chukizo la Wamoabi, mahali pa juu, katika mlima uliokabili Yerusalemu, na Moleki, chukizo la wana wa Amoni… [9]Basi BWANA akamghadhibikia Sulemani…’’ 1 Wafalme 11:5-9<br><br>Swali: Sulemani anajua kuwa adhabu ya kuabudu miungu ya uongo ni kupigwa mawe hadi kufa. | Kuamini kuwa manabii, amani iwe juu yao, hawatendi dhambi ni miongoni mwa itikadi thabiti za Kiislamu. Na kutoamini hivyo ni kuwavunjia adabu kwa makusudi katika usafi wa Mitume na ni ukafiri wa wazi unaomtoa mtu katika dini.<br><br>Suleimani, amani iwe juu yake, hajakufuru (… na Suleimani hakukufuru, bali mashetani ndio |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale hachagui vizuri manabii, hivyo anamtuma Haruni ili atengeneze ndama aliyeyeyushwa kwa dhahabu? Na kumtuma Musa atengeneze sanamu ya nyoka wa shaba linaloponya kila anayeumwa na nyoka? | (Kumbukumbu la Torati 13:1-11). Kwa nini alipokuwa mzee aliabudu miungu ya uongo? Je, Mungu anampa ufunuo mtu kafiri anayesujudia miungu ya uongo?<br>---<br>''[2]Haruni akawaambia, Zivunjeni pete za dhahabu zilizo katika masikio ya wake zenu, na wana wenu, na binti zenu, mkaniletee. [3]Watu wote wakazivunja pete za dhahabu zilizo katika masikio yao, wakamletea Haruni. [4]Akaipokea mikononi mwao akaitengeneza kwa patasi, akaifanya iwe sanamu ya ndama kwa kuiyeyusha; nao wakasema, Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyokutoa katika nchi ya Misri. [5]Naye Haruni alipoona jambo hili, akajenga madhabahu mbele yake; Haruni akatangaza akasema, Kesho itakuwa sikukuu kwa BWANA.'' Kutoka 32:2-5<br><br>''[8]Bwana akamwambia Musa, Jifanyie nyoka wa shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi. [9]Musa akafanya nyoka wa shaba, akaiweka juu ya mti, hata ikiwa nyoka amemuuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi.'' Hesabu 21:8-9 | waliokufuru, wakiwafundisha watu uchawi….) Al-Baqarah 102.<br><br>Saamiriyu alitumia nafasi ya kutokuwepo kwa Musa, amani iwe juu yake, akatengeneza ndama wa dhahabu mwenye tundu mbili la kwanza lipo nyuma yake linaloingiza hewa kisha inatoka katika tundu la pili liliopo kichwani mwake kwa namna ya kutoa mlio wa ng`ombe. Kwa hakika Haruna, amani iwe juu yake, alijaribu kuwabainishia watu wake kwa waziwazi na kuwasihi: (Na Haruni aliwaambia zamani (akasema): "Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mumefitinishwa tu kwa (kitu) hiki. Na kwa yakini Mola wenu ni Yule Mungu mwenye kurehemu. Basi nifuateni na tiini amri yangu (muache kuabudu mungu huyu)." Ta- ha 90. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaridhia kwa Haruni atoe sadaka kwa Azazeli (shetani au pepo)? | ''[9]Na Haruni atamleta yule mbuzi aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya BWANA; na kumtoa awe sadaka ya dhambi. [10]Bali Yule mbuzi aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya Azazeli atawekwa hai mbele za ili kumfanyia upatanisho, ili kumpeleka jangwani kwa ajili ya Azazeli.'' Mambo ya Walawi 16:9-10 | Haruni, amani iwe juu yake aliendelea kuwa imara katika haki mpaka anafariki. Alikuwa mwaminifu kwa mahubiri ya Musa, amani iwe juu yake. Musa, amani iwe juu yake akasema katika tukio mojawapo: (Musa) akasema: "Mola wangu! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu…)." Al-MAidah 25. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaridhia mtu akufuru | ''[33]Akaitambua, akasema, Ndiyo kanzu ya mwanangu, mnyama mkali amemla; bila shaka Yusufu ameraruliwa. [34]Yakobo akararua mavazi | Yakubu, amani iwe juu yake, anatufundisha uvumilivu wakati wa balaa: (Na wakaleta juu ya kanzu yake damu ya uwongo. |

| | | |
|---|---|---|
| (maamuzi ya Mungu) kwa kifo cha Yusufu? | yake, akajivika gunia kiunoni, na kumlilia mwanawe siku nyingi.'' Mwanzo 37:33-34 | (Baba yao) akasema: (alipoiona ile kanzu haikuchanika – walisahau kuichanachana): "Bali nafsi zenu zimekuzainishieni (zimekupambieni) jambo (kumfanyia mwenzenu. Basi mmekwisha kufanya. Mmemuua kusudi). Basi (langu mimi ni) subira njema; na Mwenyezi Mungu ndiye aombwaye msaada kwa haya mnayoyasema.") Yusuf 18. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anawafunulia Manabii: Musa na Yoshua wafanye uporaji na wizi? Je, Mungu anapora mifugo?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale anamfunulia Yakobo amuongopee baba yake Isaka ili aibe "Baraka" kutoka kwa ndugu yake Esau?<br><br>Je, Baraka: ni wingi wa pombe na kuwatenga mataifa na kuwatawala ndugu zake? | ''Lakini kila mwanamke ataomba kwa jirani, na kwa huyo akaaye naye nyumbani, vyombo vya fedha, na vyombo vya dhahabu, na mavazi; nanyi mtawavika wana wenu na binti zenu; nanyi mtawateka nyara Wamisri.'' Kutoka 3:22<br><br>'… lakini nyara zake na wanyama wake wa mji mtavitwaa kuwa mateka yenu wenyewe…'' Yoshua 8:2<br><br>"Isipokuwa wanyama wa mji na nyara za mji Israeli wakatwaa wenyewe kuwa ni mapato yao, sawasawa na hilo neno la BWANA..." Yoshua 8:27<br><br>" ... [9]Hivi Mungu akamnyang'anya mali yake baba yenu, na kunipa mimi.'' Mwanzo 31:8-9<br><br>" [19]Yakobo akamwambia babaye, Mimi ni Esau, mzaliwa wako wa kwanza, nimefanya kama ulivyoniambia. Ondoka, tafadhali, ukae kitako, ule mawindo yangu, ili roho yako inibariki… [22]Basi Yakobo akamkaribia Isaka, babaye, naye akampapasa, akasema, Sauti ni sauti ya Yakobo, lakini mikono ni mikono ya Esau... [24]Akamwuliza, Wewe ndiwe kweli mwanangu | Mtume wetu mtukufu, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Kwa hakika wameangamia wale wa kabla yenu. Kwa sababu wao walikuwa, pindi mwenye uwezo akiiba, wanamwacha na pindi mnyonge miongoni mwao akiiba wanamtekelezea adhabu). Imepokewa na Bukhariyu.<br><br>Kwa hakika uongo ndio kichwa na mwanzo wa maovu. Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: "Jiepusheni na uongo, kwa hakika uongo unapeleka katika maovu, na maovu yanapeleka motoni. Na mja hatoacha kuendelea na kuongopa na kujipamba na uongo mpaka anaandikwa kwa Allah kuwa yeye ni mwongo". |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale anamuamrisha Samweli aongope, pale alipompeleka kwa Daudi (ibnu Yese) ili ampake mafuta kwa mgongo wa chupa? | Esau? Akasema, Ndimi... [27]Akakaribia akambusu. Naye akasikia harufu ya mavazi yake, akambariki akasema, Tazama, harufu ya mwanangu Ni kama harufu ya shamba alilolibariki Bwana. [28]Mungu na akupe ya umande wa mbingu, Na ya manono ya nchi, Na wingi wa nafaka na mvinyo. [29]Mataifa na wakutumikie Na makabila wakusujudie, Uwe bwana wa ndugu zako, Na wana wa mama yako na wakusujudie. Atakayekulaani alaaniwe, Na atakayekubariki abarikiwe.'' Mwanzo 27:19-29<br><br>''[1]BWANA akamwambia Samweli, Hata lini utamlilia Sauli, ikiwa mimi nimemkataa asiwamiliki Israeli? Ijaze pembe yako mafuta, uende, nami nitakupeleka kwa Yese, Mbethlehemi; maana nimejipatia mfalme katika wanawe. [2]Samweli akasema, Nawezaje kwenda? Sauli akipata habari, ataniua. Basi BWANA akasema, Chukua ndama pamoja nawe, ukaseme, Nimekuja ili kumtolea BWANA dhabihu.'' 1 Samweli 16:1-2 | Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: (Wanaozua uwongo (wakipita wakitangaza kama hivyo kusema Mtume anafundishwa Qurani na huyo Mrumi) ni wale wasioziamini Aya za Mwenyezi Mungu; na hao ndio waongo). An-Nahl 105.<br><br>Kutoka kwa Abuu Huraira, kutoka kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: {"Alama za mnafiki ni tatu, akiongea anaongopa, na akiahidi anavunja ahadi, na anapoaminiwa anasaliti"} Bukhariyu na Muslimu. |
| Utakatifu upo wapi kwa Ibrahimu kuwa dayuthi (hana wivu) ili apate heri kutoka kwa Firauni wa Misri na Abimeleki, kwa sababu ya mkewe Sara? | " [13]Tafadhali useme, wewe u ndugu yangu, iwe heri kwangu kwa ajili yako, na nafsi yangu iishi kwa ajili yako. [14]Basi ikawa Abramu alipofika Misri, Wamisri wakamwona huyo mwanamke ya kwamba yeye ni mzuri sana. [15]Wakuu wa Farao wakamwona, nao wakamsifu kwa Farao; basi yule mwanamke akachukuliwa nyumbani mwa Farao. [16]Naye akamtendea Abramu mema kwa ajili yake; naye alikuwa na kondoo na ng'ombe, na punda waume, na watumwa, na wajakazi, na punda wake, na ngamia.'' Mwanzo 12:13-16 Vilevile na Abimeleki wa Gerari Mwanzo 20:1, na Mwanzo 20:14-17. | Wivu wa mwanamume kwa mkewe na watu wake ni jambo zuri. Na ni alama ya kukamilika kwa urijali na kuheshimika. Na kuacha wivu ni udayuthi mbaya kisheria na kitabia. Na haya ndio yaliyofanya kulinda heshima kuwa ni jambo la kisheria. Na atakayekufa akilinda heshima yake anahesabiwa ni shahidi (shujaa). Kwa kauli ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: "Atakayeuliwa akitetea familia yake huyo ni shahidi". Imepokewa na Ahmad. |
| Utakatifu upo wapi kwa kuwa Isihaka hana wivu | ''[7]Watu wa mahali hapo wakamwuliza habari za mkewe. Akasema, Ni ndugu yangu huyu maana aliogopa kusema, Ni mke wangu, watu wa nchi | Onyo kali liliokuja kwa Dayuthi ni kauli ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake: "Watu watatu |

| | | |
|---|---|---|
| kwa mkewe "Dayuthi" kwa sababu ya mkewe Rebeka? | wasije wakamwua kwa ajili ya Rebeka; kwa maana alikuwa mzuri wa uso…Abimeleki, mfalme wa Wafilisti, akachungulia dirishani akamwona Isaka anacheza-cheza na Rebeka mkewe.'' Mwanzo 26:7 | hawatotazamwa na Allah Mtukufu aliyetukuka siku ya Kiama: Mwenye kuwaasi wazazi wake wawili, mwanamke mwenye kujifanya mwanaume, na Dayuthi (asiye na wivu na mkewe).'' Imepokewa na Ahmad na Annasaaiyu. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale amemfanya Musa ni Mungu na Mungu kuwa "wa unne" badala ya "utatu"?<br><br>Je, Mungu anautia ugumu moyo wa Farao licha ya kauli ya Farao kwa Musa na Haruni ''haya niombeeni?'' | ''[1]BWANA akamwambia Musa, Angalia, nimekufanya wewe kuwa kama Mungu kwa Farao; na huyo ndugu yako Haruni atakuwa nabii wako… [3]Nami nitaufanya mgumu moyo wa Farao… '' Kutoka 7:1-3<br><br>''… lakini nitaufanya mgumu moyo wake…'' Kutoka 4:21<br><br>''Farao akasema, Mimi nitawapa ruhusa mwende, ili mmchinjie dhabihu BWANA, Mungu wenu, jangwani; lakini hamtakwenda mbali sana; haya niombeeni.'' Kutoka 8:28 | Musa na Haruni, amani iwe juu yao, walienda kwa Firauni na kumfikishia ujumbe. Na Musa, amani iwe juu yake aliendelea kuwalingania Firauni na watu kwa mawaidha mazuri…. Lakini hilo halikuwazidishia wao ila kuendelea na kibri ardhini, kuchupa mipaka na kuwaadhibu waumini… Musa, amani iwe juu yake, akawaombea dua kuangamizwa… Allah akawaadhibu kwa ukame, hali mbaya ya hewa na kupungukiwa na matunda ili wakumbuke… |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anawafunulia Manabii wawalilie watoto waliouwawa miongoni mwa watoto wa mataifa yake? | ''… roho yangu italia … na jicho langu litalia sana na kutoka machozi mengi...'' Yeremia 13:17<br><br>''[9]Basi, naililia mizabibu ya Sibma… alilolisema BWANA juu ya Moabu zamani.'' Isaya 16:9-13<br><br>''Nawe utawaambia neno hili, Macho yangu na yatiririke machozi, usiku na mchana, wala yasikome….'' Yeremia 14:17<br><br>''Laiti ningeweza kujifariji, nisione huzuni! Moyo wangu umezimia ndani yangu.'' Yeremia 8:18<br><br>'… binti ya watu wangu!'' Yeremia 9:1 | (Ameepukana Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi – na hayo wanayomsifia). Az-Zukhruf 82. |

| | | |
|---|---|---|
| | ''Mtima wangu, mtima wangu! Naumwa katika moyo wangu wa ndani; moyo wangu umefadhaika ndani yangu...'' Yeremia 4:19<br><br>''Kwa sababu hiyo mtima wangu unamlilia Moabu kama kinubi, na matumbo yangu kwa ajili ya Kir-Heresi.'' Isaya 16:11<br><br>''Moyo wangu umegeuka ndani yangu, huruma zangu zimewaka pamoja.'' Hosea 11:8 | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anasahau? | ''Ee BWANA, hata lini utanisahau, hata milele? Hata lini utanificha uso wako?'' Zaburi 13:1<br><br>'… Kwa nini umenisahau…'' Zaburi 42:9<br><br>''Mbona unatuficha uso wako, Na kusahau kuonewa na kudhulumiwa kwetu?'' Zaburi 44:24<br><br>''Mungu amesahau fadhili zake? '' Zaburi 77:9 | ("… Mola wangu hapotei wala hasahau.") Ta ha 52. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale Hatatenda fadhili tena? | ''[7]Je! Bwana atatupa milele na milele? Hatatenda fadhili tena kabisa? [8]Rehema zake zimekoma hata milele?... '' Zaburi 77:7-8 | (Sema, "Enyi waja wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu…) Az-Zumar 52 |
| (Nafsi ya pili "Yesu") ambaye ni miongoni mwa utatu wa Nafsi aliyetundikwa msalabani, je, amelaaniwa na Mungu?! | ''[22]Akiwa mtu ametenda dhambi ipasayo kufa, akauawa, nawe ukamtundika juu ya mti; [23]mzoga wake usikae usiku kucha juu ya mti; lazima utamzika siku hiyo hiyo; kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu…' Kumbukumbu la Torati 21:22-23 | Masihi Isa, amani iwe juu yake hajalaaniwa. Naye hajauawa wala hajasulubiwa hata japo kidogo kuwekwa msalabani. Yeye ni katika Mitume Mikuu. (… hali hawakumwua wala hawakumsulubu, bali walibabaishiwa (mtu mwingine wakamdhani nabii Isa…). An-nisaa 157. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale hafanyi lolote bila kuwafunulia manabii? | ''[7]Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake.'' Amosi 3:7 | (Na Mayahudi walisema: "Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba; (hatuoni kupata mali kama zamani)." (siyo, bali) mikono yao ndio iliyofumba (haifanyi kheri ila kudhulumu na kupokonya); na wamelaaniwa kwa sababu ya yale waliyosema. Lakini mikono yake |

| | | |
|---|---|---|
| | | (Mwenyezi Mungu) iwazi, hutoa apendavyo….) Al-Maidah 64. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale analipiza kwa kutuma wanyama wawili wawashambulie watoto 42 kwa sababu watoto hao walisema "Panda ewe kialaza"?! | ''… naye alipokuwa akienda njiani, wakatoka vijana katika mji, wakamfanyizia mzaha, wakamwambia, Paa wewe mwenye upaa! Paa wewe mwenye upaa! [24]Akatazama nyuma akawaona, akawalaani kwa jina la BWANA. Wakatoka dubu wawili wa kike mwituni, wakawararua vijana arobaini na wawili miongoni mwao.'' 2 Wafalme 2:22-24 | (Ameepukana Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi – na hayo wanayomsifia). Az-Zukhruf 82. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale hasikii? | ''Ee BWANA, nilie hata lini, wewe usitake kusikia?'' Habakuki 1:2 | (… Hakika Mola wangu ni Mwenye kusikia maombi (ya waja wake…). Ibrahim 39. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anachukua maamrisho kutoka kwa wanadamu? | ''… fumbua macho yako, Ee BWANA, uone….'' 2 Wafalme 19:16 ''[15]…Tega sikio lako, Ee BWANA, usikie; fumbua macho yako, Ee BWANA, uone; uyasikie maneno...'' 2 Wafalme 19:15-16, | (Bila shaka Mwenyezi Mungu anajua yaliyofichikana mbinguni na ardhini; na Mwenyezi Mungu anaona mnayoyatenda (yote). Al-zumar 18 |
| Je, nywele za kichwa cha Mungu wa Agano la Kale ni kama sufi safi? | ''… mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto...'' Danieli 7:9 | (Ameepukana Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi – na hayo wanayomsifia). Az-Zukhruf 82. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni kama "tiniini" hivyo anatoa moshi puani kwake na moto mdomoni kwake? | '' [27]… midomo yake imejaa ghadhabu, na ulimi wake ni moto ulao; [28]na pumzi yake ni kijito kifurikacho...'' Isaya 30:27-28<br><br>''Hizo mbingu hupambwa kwa roho yake; Mkono wake umemchoma nyoka aendaye mbio.'' Ayubu 26:13<br><br>''Kukapanda moshi kutoka puani mwake, Moto ukatoka kinywani mwake…'' 2 Samweli 22:9 | (….Hakuna chochote mfano wake; naye ni mwenye kusikia, mwenye kuona.) As-shuura 11. |

| | | |
|---|---|---|
|  | ''Kukapanda moshi kutoka puani mwake, Moto ukatoka kinywani mwake ukala, Makaa yakawashwa nao.'' Zaburi 18:8 | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale haaminiki na matendo yake ni kupotosha? | ''Tafakari vema kazi yake Mungu; kwa sababu ni nani awezaye kukinyoosha kitu kile alichokipotosha yeye?'' Mhubiri 7:13 | (Mwenyezi Mungu yu mbali na sifa wanazompa.) As-saaffat 159. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaziinamisha mbingu na chini ya miguu yake kuna giza kuu? | ''Aliziinamisha mbingu akashuka, Kukawa na giza kuu chini ya miguu yake''. Zaburi 18:9 na 2 Samweli 22:10<br><br>''… chini ya miguu yake palikuwa na kama sakafu iliyofanyizwa kwa yakuti samawi, kama zile mbingu zenyewe kwa usafi wake.'' Kutoka 24:10 | (Ameepukana Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi – na hayo wanayomsifia). Az-Zukhruf 82. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anatengua / anavunja ahadi? | '' [38]Walakini Wewe umemtupa na kumkataa, Umemghadhibikia masihiwako. [39]Umechukizwa na agano la mtumishi wako, Umeinajisi taji yake na kuitupa chini.'' Zaburi 89:38-39<br><br>[43]Pia umeurudisha nyuma ukali wa upanga wake; Wala hukumsimamisha vitani.'' Zaburi 89:43 | (Hii ni) ahadi ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake, lakini watu wengi hawajui). Ar-um 6. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni mkaidi akiwa na wapotofu? | ''[26]Kwake ajitakasaye utajionyesha kuwa mtakatifu; Na kwa mpotovu utajionyesha kuwa mkaidi.'' Samweli wa 2 27:22, Zaburi 18:26 | (… Basi msifuate matamanio mkaacha kufanya uadilifu. Na kama mkipotoa (shahada) au mkajitenga (na kushuhudia, Mwenyezi Mungu atakuteseni); na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyatenda.) An-nisaa 135. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale hajui adabu za mazungumzo ya kidini yenye heshima? | ''… enyi wana wa mwanamke mchawi, uzao wa mzinzi na kahaba.'' Isaya 57:3<br><br>''Ole wake yeye aliyeasi na kutiwa unajisi!'' Sefania 3:1 | Ni lazima kwa Muislamu kujiepusha na maneno mabaya na machafu, na auzoeshe ulimi wake kusema ya heri, kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: (… na semeni na watu kwa wema…) Al-baqarah 82. Kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | ‘‘Lakini mpumbavu aweza kupata ufahamu, Ingawa mwanadamu huzaliwa kama mtoto wa punda-mwitu.’’ Ayubu 11:12<br><br>‘’… Wewe, mwana wa mke mkaidi, asi … kwa aibu yako mwenyewe, na kwa aibu ya uchi wa mama yako.’’ 1 Samweli 20:30<br><br>‘’… akitenda maovu nitamwadhibu kwa fimbo ya binadamu na kwa mapigo ya wanadamu.’’ 2 Samweli 7:14 | hakika imethibiti katika Hadithi ya kuwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: “Muumini si mwenye kuwasema watu vibaya, wala mwenye kulaani watu wala kufanya machafu wala mambo mabaya”. Imepokewa na Tirmidhiyu na Alhaakimu, na Albani ameiona ni sahihi. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anapokasirika anahimiza kumtusi Daudi? | ‘’ [10]… Kwa sababu yeye analaani, na kwa sababu BWANA amemwambia, Mlaani Daudi… [11]… Mwacheni alaani, kwa sababu BWANA ndiye aliyemwagiza. [12]Labda BWANA atayaangalia mabaya yaliyonipata, naye BWANA atanilipa mema kwa sababu ya kunilaani kwake leo.’’ 2 Samweli 16:10-12 | Ni haramu kwa Muislamu kutukana: (Na wale wanaowaudhi wanaume Waislamu na wanawake Waislamu pasipo wao kufanya kosa lolote, bila shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhahiri). Al-Ahzab 58. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anajipinga yeye mwenyewe katika kisa cha kumuumba Adamu? Je, aliwaumba wanyama kabla ya mwanadamu? Au alimuumba mwanadamu kabla ya wanyama? | **Ameumba wanyama kabla ya wanadamu:**<br>‘’[24]Mungu akasema, Nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake; ikawa hivyo. [25]Mungu akafanya mnyama wa mwitu kwa jinsi zake, na mnyama wa kufugwa kwa jinsi zake, na kila kitu kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake... [26]Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura<br><br>**Ameumba wanadamu kabla ya wanyama:**<br>‘’[18]BWANA Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye.<br><br>[19]BWANA Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina | Muslimu amepokea kutoka kwa Abuu Huraira, Allah amuwie radhi amesema: Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alinishika mkono na akasema: Allah Mtukufu aliyetukuka ameumba udongo siku ya Jumamosi. Na akaumba ndani yake milima siku ya jumapili. Na akaumba mimea siku ya Jumatatu. Na akaumba machukizo siku ya Jumanne. Na akaumba nuru siku ya Jumatano. Na akawatawanya wanyama katika huo udongo siku ya Alhamisi. Na akamuumba Adamu, amani iwe juu yake, baada ya laasiri katika siku ya Ijumaa, mwishoni mwa kuumba saa ya mwisho miongoni mwa saa za Ijumaa, baina ya laasiri na kuelekea usiku. |

| | | |
|---|---|---|
| | yetu...'' Mwanzo 1:24-26<br>lake.'' Mwanzo 2:18-19 | Allah Mtukufu aliyetukuka amemuumba mwanadamu ili amuabudu yeye peke yake bila ya kumshirikisha. Na amemtukuza juu ya viumbe vyote na akaufanya ulimwengu wote umtumikie mwanadamu. (Na hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewapa vya kupanda barani na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba, kwa utukufu ulio mkubwa (kabisa). Bani Israil 70. |
| Je, kwa Mungu sauti ya farasi ni "Aha!"? na sauti ya muungurumo wa mataifa ni kama sauti ya maji ni mengi? | " [19]Je! Wewe ulimpa farasi uwezo wake?... [25]Kila ipigwapo baragumu yeye husema, Aha! ...'' Ayubu 39:19-25<br><br>[13] Mataifa wananguruma kama ngurumo ya maji mengi...'' Isaya 17:13 | (Hakika Mola wako ndiye Muumbaji (na ndiye) Mjuzi.) Al-Hijr 86.<br><br>(Kuteremshwa kwa kitabu (hiki) kunatokana kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye kujua). Muumin 2. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale hajui sehemu alipo Adam? Wala sehemu alipo Habili? | " [9]BWANA Mungu akamwita Adamu, akamwambia, <u>Uko wapi</u>? ... Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale?'' Mwanzo 3:9-11<br><br>''BWANA akamwambia Kaini, <u>Yuko wapi Habili ndugu yako?</u> Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?'' Mwanzo 4:9 | Allah anasifika kwa ukamilifu wa elimu: (... Na Mola wao akawaita (akawaambia),"je, sikukukatazeni mti huu na kukwambieni ya kwamba shetani ni adui yenu aliyedhahiri?) Al-aaraf 22. |
| Nani aliyeongea andiko hili, Je, ni Mungu wa Agano la Kale au Musa au asiyejulikana? | ''[5]Basi Musa, mtumishi wa BWANA, akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la BWANA. [6]Akamzika bondeni, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth-peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo.'' Kumbukumbu la Torati 34:5-6 | (Hawaizingatii nini, hii Qurani? Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi.) An-nisaa 82 |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni fundi cherehani | ''BWANA Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.'' Mwanzo 3:21 | (Kisha Adam akapokea maneno (ya maombi) kwa Mola wake, (akaomba), na Mola wake |

| | | |
|---|---|---|
| wa mavazi ya ngozi? | Swali: Je, hili halioneshi kuwa BWANA amesamehe dhambi na kosa la Adamu na Eva? Lau kama hakuwasamehe, basi angewaacha wawinde wenyewe kisha watengeneze nguo za ngozi wao wenyewe ili kuwataabisha na kutekeleza ahadi yake kwao ya kuwa atawaadhibu katika nchi? | akapokea toba yake; hakika yeye ndiye mwingi wa kupokea toba (kwa wenye kutubia) na mwingi wa kurehemu (kwa wanaostahiki kurehemewa. Ama Iblis hakutubia kwa hivyo hakustahiki kurehemewa.) Al-Baqarah 37. |
| Je, shetani ni mkweli zaidi kuliko Mungu wa Agano la Kale, kwa kuwa Adamu hajafa baada ya kula ule mti isipokuwa aliishi miaka 930? | ''[16]BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, [17]walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.'' Mwanzo 2:16-17<br><br>''[4] Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, [5]kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.' Mwanzo 3:4-5 | (Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu na yeye ndiye Mlinzi juu ya kila kitu.) Azzumar 62.<br><br>(Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtihani); ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye nguvu Mwenye msamaha.) Al-Mulk 2. |
| Je, shetani anamiliki uhai na kifo? | ''BWANA akamwambia Shetani, Tazama, yeye yumo mkononi mwako; lakini tunza tu uhai wake.'' Ayubu 2:6 | (…Mwenyezi Mungu ndiye Mbora wa kulinda, naye ndiye anayerehemu kweli kweli kuliko wenye kurehemu wote.) Yusuf 64. |
| Je, Mungu anamwamuru Ezekieli alale chini kwa ubavu wake ili abebe madhambi ya Wana wa Israeli? | '' [4]Tena lala chini kwa ubavu wako wa kushoto, ukaweke huo uovu wa nyumba ya Israeli juu yake… [6]… utalala kwa ubavu wako wa kuume, nawe utauchukua uovu wa nyumba ya Yuda; siku arobaini...'' Ezekieli 4:4-6 | (Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila umma ya kwamba "Mwabuduni Mwenyezi Mungu na mwepukeni (Iblisi) muovu." …. Basi wko miongoni mwao upofu (upotevu) umethubutu juu yao. Basi tembeeni katika ardhi na mwangalie ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha.) Annahli 36. |
| Kwa nini Mungu wa Agano la Kale ananyoa nywele za miguuni kwa (wembe | ''Katika siku hiyo Bwana atanyoa kichwa na malaika ya miguuni, kwa wembe ulioajiriwa pande za ng'ambo ya Mto, yaani, kwa mfalme wa Ashuru, nao utazimaliza ndevu nazo.'' Isaya 7:20 | (Na siku ya Kiyama utawaona wale waliomsingizia uwongo Mwenyezi Mungu nyuso zao zimekuwa nyeusi. Je, si katika Jahanamu makazi ya wale wanaotakabari?) Azzumar 60. |

| | | |
|---|---|---|
| ulioajiriwa) kama wanawake? | | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anawapotosha waja wake kwa makusudi? | ''[25]Tena naliwapa amri zisizokuwa njema, na hukumu ambazo hawakuweza kuishi kwazo; [26]nami nikawatia unajisi kwa matoleo yao wenyewe, kwa kuwa walipitisha motoni wote waliofungua tumbo; ili kuwafanya kuwa ukiwa...'' Ezekieli 20:25-26 | (Na nani dhalimu mkubwa kuliko Yule anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu....) Al-Ankabuuti 68. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anatembea makambini? Wala haamrishi kujisafisha baada ya kujisaidia haja kubwa? | ''[13]nawe uwe na jembe dogo katika silaha zako; napo uotamapo nje uchimbe kwa lile jembe, na kugeuka na kukifunika kikutokacho; [14]kwa kuwa BWANA. Mungu wako, yuatembea katika kituo akuokoe, na kukutolea adui zako mbele yako; kwa hiyo na kiwe kitakatifu kituo chako; asije akaona kitu kwako kisichokuwa safi, akageuka na kukuacha.'' Kumbukumbu la Torati 23:13-14 | (... Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanaojitakasa.) Al-Baqarah 222. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni mbaguzi wa rangi kwa kukiadhibu kizazi cha Kanaani "kiwe watumwa" kwa kosa alilolifanya Nuhu kwa kunywa pombe na kukaa uchi? | ''[21]akanywa divai, akalewa; akawa uchi katika hema yake. [22]Hamu, baba wa Kanaani, akauona uchi wa baba yake, akawaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje. [23]Shemu na Yafethi wakatwaa vazi, wakalitanda mabegani mwao wote wawili, wakaenda kinyumenyume, wakaufunika uchi wa baba yao; na nyuso zao zilielekea nyuma, wala hawakuuona uchi wa baba yao.[24]Nuhu akalevuka katika ulevi wake, akajua mwana wake mdogo alivyomtendea. [25]Akasema, Na alaaniwe Kanaani; Atakuwa mtumwa kabisa kwa ndugu zake. [26]Akasema, Na atukuzwe BWANA Mungu wa Shemu; Na Kanaani awe mtumwa wake. [27]Mungu akamnafisishe Yafethi. Na akae katika hema za Shemu; Na Kanaani awe mtumwa wake.'' Mwanzo 9:21-27<br><br>Je, ubaguzi unaanza katika kisa cha Nuhu na mjukuu wake Kanaani?<br><br>''[11]Malaika wa BWANA akamwambia, Tazama! Wewe una mimba, utazaa mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Ishmaeli, maana BWANA | (Na pia akawaambia) "Enyi kizazi cha wale tuliowapandisha (katika jahazi) Nuhu! (kuweni wenye shukrani kama mzee wenu huyo). Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani.) Bani Israili 3.<br><br>(Amani kwa Nuhu ulimwenguni kote.) Assaaffat 79.<br><br>(Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adam na Nuhu na kizazi cha Ibrahimu na kizazi cha Imrani (Babaake Musa); na Imrani mwingine aliye baba yake Maryamu) juu ya walimwengu wote (wa zama zao). Aal-Imrani 33.<br><br>Allah amemruzuku Ibrahimu, Amani iwe juu yake Ismaili na Is-haqa. ("Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa juu ya uzee (wangu watoto wawili hawa:-) Ismaili na Is-haqa. Hakika Mola |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni mwenyeji kujipinga mwenyewe, kwa kumbariki Ismaili na kukifanya kizazi chake kuwa umma mtukufu wenye kutoa matunda mazuri ili hali huyo Ismaili ni mtu muovu?!<br><br>Je, Mungu anamwamrisha Ibrahimu asikie maneno ya mkewe Sara?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale anamwamrisha Hajiri ambebe kijana wa miaka 14 "Ondoka, ukamwinue kijana, ukamshike mkononi mwako"? | amesikia kilio cha mateso yako. [12]Naye atakuwa kama punda-mwitu ...'' Mwanzo 16:11-12<br><br>''[12]Mungu akamwambia Ibrahimu, Neno hili lisiwe baya machoni pako, kwa ajili ya huyo mwana, na huyo mjakazi wako. Kila akuambialo Sara, sikiza sauti yake, kwa maana katika Isaka uzao wako utaitwa... [17]... Malaika wa Mungu akamwita Hajiri kutoka mbinguni, akamwambia, Una nini, Hajiri? Usiogope... [18]Ondoka, ukamwinue kijana, ukamshike mkononi mwako, kwa kuwa nitamfanya kuwa taifa kubwa.'' Mwanzo 21:12-18<br><br>''[19]Mungu akasema... [20]Na kwa habari za Ishmaeli nimekusikia, nimembariki, nitamzidisha, nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi na wawili, nami nitamfanya awe taifa kuu.'' Mwanzo 17:19-20<br><br>Umri wa Ismaili wakati huu kwa uchache ulikuwa ni miaka 14 na hii ndio tofauti ya miaka baina ya Ismaili na Isaka. Ibrahimu amani iwe juu yake, alimzaa Ismaili akiwa na miaka 86 (Mwanzo 16:16) na alimzaa Isaka akiwa na miaka 100 (Mwanzo 21:5). Kwa maana hiyo, ni kuwa Ismaili alishakuwa kijana mwenye nguvu, sasa iweje BWANA amwambie Hajiri: Ondoka, ukamwinue kijana, ukamshike mkononi mwako? Je, kwa Wana wa Israeli, mtoto aliyefikia miaka 14 bado anazingatiwa kuwa ni mchanga na kubebwa na mamaye?<br><br>Kwa hakika hawa ni watoto wa Ishmaeli waliobarikiwa, kuzidishwa, nkuongezwa sana sana na kufanywa wawe taifa kuu. Mwanzo 17:19-20. Ni nani huyo nabii ambaye chini ya uongozi wake | wangu ni mwenye kusikia maombi yangu (mengine). Ibrahimu 39.<br><br>Allah alimwamrisha Ibrahimu awapeleke Ismaili na Mama yake Hajari eneo Takatifu la Makka. Ibrahimu aliona ndotoni kuwa Allah anamwamrisha amchinje mwanawe. Ibrahimu akatii na alikaribia kumchinja mwanawe (Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu). Assaffat 107. Kisha Allah akambashiria Ibrahimu, amani iwe juu yake, kuwa atapata mtoto mwingine naye ni Is-haqa (Tena tukambashiria (kumzaa) Is-haqa, (mtoto wake wa pili). Nabii miongoni mwa watu wema (kabisa). Assaffat 112.<br><br>Allah amemwamrisha Ibrahimu, amani iwe juu yake, ajenge nyumba ya kwanza ya kumwabudia Allah (Alkaaba) huko Makka. Na Ibrahimu alipoijenga hiyo nyumba aliamrishwa na Allah awaite watu waje kuihiji. Na Ibrahimu, amani iwe juu yake, akaiombea dua Makka na vilivyomo ndani yake, na akamuombea Ismaili na kizazi chake. Kisha akawaombea watu wa Makka Allah awaletee Mtume miongoni mwao atakayewaita kumwabudu Allah peke yake. Akasema: ("Ee, Mola wetu! Waletee Mtume anayetokana na wao, awasomee aya zako, na kuwafundisha Kitabu (chako) na hikima (nyingine) na awafundishe kujitakasa (na kila mbaya). Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, na |

| | | |
|---|---|---|
| Ni akina nani hao QAYADAARU na NIYAYUTI?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale ni mbaguzi na kuwabughudhi ISUUU ambaye ni mtoto wa kwanza wa Is-haka bila ya sababu?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale ni mbaguzi na kuadhibu kwa kuwalaani wasiozungumza lugha ya Kiyahudi?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale ni mbaguzi na kuwafanya watu wasio wayahudi ni watu wasio na maana/duni na inawezekana kuwafanya watumwa kwa kuwatawala na kuwadhalilisha hadi wawasujudie wao na | watu wa peninsula ya Uarabuni walikusanyika na kumwabudu Mwenyezi Mungu Mmoja peke yake baada ya kuwa walikuwa wakiabudu masanamu?... Je, nabii huyo ni Yesu Mnazareti, au Paulo au Muhammad, rehema na amani ziwe juu yake?<br><br>---<br><br>Esau alipatwa na kutumiwa vibaya na nduguye ambaye ni Yakobo. Kiasi cha Esau kuuza haki ya uzaliwa wake wa kwanza kwa mkate na chakula cha dengu!! (Mwanzo 25:29-34). Pia Esau aliibiwa Baraka zake za kuwa mtoto wa kwanza pale Yakobo alipomuongopea baba yake ambaye ni Isaka na kujifanya kuwa yeye ndiye Esau. (Mwanzo 27:19-29) ''[2]... Asema BWANA; ila nimempenda Yakobo; [3]bali Esau nimemchukia na kuifanya milima yake kuwa ukiwa, na urithi...'' Malaki 1:2-3<br><br>''[24]na watoto wao wakanena nusu kwa lugha ya Ashdodi, wala hawakuweza kunena kwa Kiyahudi, bali kwa lugha ya watu hao mojawapo. [25]Nikagombana nao, nikawalaani, nikawapiga baadhi yao, na kuwang'oa nywele zao; nikawaapiza kwa Mungu, nikasema, Msiwaoze wana wao binti zenu, wala msiwatwae binti zao ili waolewe na wana wenu, wala na ninyi wenyewe.'' Nehemia 13:24-25<br><br>''[22]Bwana MUNGU asema hivi, Tazama, nitawainulia mataifa mkono wangu, na kuwatwekea kabila za watu bendera yangu... watainama mbele yako kifudifudi, na kuramba mavumbi ya miguu yako; nawe utajua ya kuwa mimi ni BWANA, tena waningojeao hawatatahayarika.'' Isaya 49:22-23 | ndiye Mwenye hikima.) Albaqara 129.<br><br>Allah alipokea dua ya Nabii wake Ibrahimu, amani iwe juu yake, na akaifanya Makka kuwa mji wa amani na kuwaruzuku watu wake matunda, na akawapelekea Mtume miongoni mwao naye ni Mtume wa mwisho naye ni Muhammad, Rehema na amani ziwe juu yake.<br><br>Katika kitabu cha Ahmadi, kutoka kwa Abuu Nasrata, Radhi za Allah ziwe juu yake, hakika alimsikia Yule aliyemsimulia hotuba ya Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, katika ya siku za Tashriiqi, akisema: "Enyi watu, zindukeni, kwa hakika Mola wenu ni mmoja. Na baba yenu ni mmoja. Zindukeni, hakuna ubora kwa Mwarabu kuliko asiyekuwa Mwarabu. Wala kwa mwekundu kuliko mweusi. Wala mweusi kuliko mwekundu. Isipokuwa kwa kumcha Mwenyezi Mungu. Nimefikisha". Wakasema: Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake ameshafikisha.<br><br>(Na miongoni mwao kuna baadhi yao wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) kitabu ili mpate kuyafikiri (maneno) yao hayo kuwa ni ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu); wala si ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu), na wanasema: "Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu", na hali hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu; na |

| | | |
|---|---|---|
| kuwaramba vumbi la miguu yao? | ''[44]Tena katika habari za watumwa wako na wajakazi wako, utakaokuwa nao; mataifa walio kando-kando yenu, katika hao mtanunua watumwa na wajakazi... [46]Nanyi mtawafanya kuwa urithi kwa watoto wenu baada yenu, wawe milki yao; siku zote...'' Mambo ya Walawi 25:44-46<br><br>''[20]Mtu akimpiga mtumwa wake, au kijakazi chake, kwa fimbo, naye akifa mkononi mwake, hana budi ataadhibiwa. [21]Lakini akipona siku moja au mbili hataadhibiwa; maana, ni mali yake.'' Kutoka 21:20-21 | wanamsingizia Mwenyezi Mungu uwongo na hali wanajua (kuwa huo ni uwongo). Aali Imran 78. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaapia kwa Yakobo na hali yakuwa huyo Yakobo ni: (Mwizi na mdanganyifu)? | ''BWANA ameapa kwa fahari ya Yakobo, Hakika sitazisahau kamwe kazi zao hata mojawapo.'' Amosi 8:7<br><br>Je, Yakobo aliiba utume toka kwa ndugu yake Esau? Mwanzo 27:36<br><br>Je, Yakobo alimdanganya mjomba wake Labani katika maswala ya mbuzi? Mwanzo 30:32-43. | Sheikh al-Islaam Allah amrehemu amesema: "Kwa hakika Allah anaapia kwa anachoapia miongoni mwa viumbe wake kwa kuwa viumbe wake ni alama zake na ni viumbe wake. Hivyo viumbe ni dalili ya ulezi wake, uungu wake, upweke wake, elimu yake, uweza wake, matakwa yake, rehema zake, hekima zake, utukufu wake, na nguvu zake. Yeye mtukufu anaviapia hivyo viumbe; kwa kuwa kwake yeye kuviapia hivyo ni kumtukuza yeye Mtukufu. Ama sisi viumbe haturuhusiwi kuviapia viumbe kwa ushahidi wa maandiko na makubaliano ya wanazuoni" mwisho, kutoka katika Majumuu Alfatawaa) (1/290). |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni "mzembe/mpuuzaji" hadi inafikia vitabu vyake vinapotea na kukosekana? | Vitabu kadhaa vya Taurati havipo, kwa mfano:<br><br>1- Kitabu cha Vita vya BWANA kilichotajwa katika (Hesabu 21:14).<br>2- Kitabu cha Yashari kilichotajwa katika (Yoshua 10:13).<br>3- Kitabu cha Mambo ya Sulemani kilichotajwa katika (1 Wafalme 11:41). | (Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahali pake, husema (midomoni mwao): "Tumesikia"; Na (nyoyoni mwao husema): "Tumeasi". (Na wanasema kumwambia Mtume): "Sikia bila kusikilizwa;" Na (hulitamka tamko |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni mpotoshaji, kiasi kwamba anatolea ushahidi wa aya za maandiko ya kitabu chake ambazo hazipo? | 4- Kitabu cha Maombolezo ya Yeremia kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 55:25).<br>5- Kitabu cha Mambo ya Yosia ʼʼyameandikwa katika Torati ya BWANAʼʼ kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 35:26).<br>6- Kitabu cha Maombolezo ya Yosia ʼʼyameandikwa katika Torati ya BWANAʼʼ kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 35:26).<br>7- Kitabu cha Nathani nabii kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 9:29).<br>8- Kitabu cha Unabii wa Ahiya Mshiloni kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 9:29).<br>9- Kitabu cha Maono ya Ido Mwonaji kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 9:29).<br>10- Kitabu cha Gadi Mwonaji kilichotajwa katika (1 Mambo ya Nyakati 29:29).<br>11- Kitabu cha Tarehe cha Wafalme wa Yuda kilichotajwa mara 18 katika (2 Wafalme 24:5, 23:28, 21:25, 21:17, 20:20, 16:19,…).<br>12- Kitabu cha Wafalme wa Israeli na Yuda kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 35:27, 36:8, 27:7).<br>13- Kitabu cha Tarehe za Shemaya Nabii na Ido mwonaji kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 12:15). | la): “*Raainaa*” kwa kuzipotoa ndimi zao (hata igeuke maana yake) ili kuitukana dini. Na kama wao wangalisema, kwa tamko la *Undhurnaa* badala ya tamko la *Raainaa*), ingalikuwa bora kwao na vizuri zaidi. Lakini Mwenyezi Mungu amewalaaani kwa kufuru zao; basi hawaamini ila kidogo tu.) Annisaa 46. |
| Mungu wa Agano la Kale anakusudia nini kwa kutolea ushahidi vitabu visivyokuwepo? | 14- Kitabu cha Mambo ya Uzia yaliyosalia yaliyoandikwa na Isaya Nabii mwana wa Amozi kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 26:22).<br>15- Kitabu cha Wafalme kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 24:27).<br>16- Kitabu cha Tarehe ya Hozai kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 33:19).<br>17- Kitabu cha BWANA kilichotajwa katika (Isaya 34:16).<br>18- Kitabu cha Tarehe ya Yehu mwana wa Hanani iliyotajwa katika kitabu cha Wafalme wa Israeli, kilichotajwa katika (2 Mambo ya Nyakati 20:34).<br>19- Kitabu cha Tarehe cha Wafalme wa Israeli kilichotajwa katika (1 Wafalme 14:19, 16:5, 16:14). | (Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wale wafanyao haraka kukufuru, miongoni mwa wale wanaosema, kwa vinywa vyao, “Tumeamini,” hali nyoyo zao haziamini; na miongoni mwa Mayahudi wanaokuja kusikiliza unayoyasema kwa ajili wakaseme uwongo; wanaokuja kusikiliza kwa ajili ya watu wengine wasiokufikia; (wale wakubwa wao ambao) huyabadilisha maneno (ya Taurati) baada ya kuwa mahali pake, ambao wanasema (kuwaambia hao wafuasi wao): “Mkipewa (na Muhammad) haya (tunayokwambieni) basi |

| | | |
|---|---|---|
| Kuna maana gani kwa Mungu wa Agano la Kale kuteremsha kitabu kisha kuonesha katika kitabu hicho hicho kitabu kingine kama rejea cha kurejelea kwa wasomaji na hicho kitabu kingine hakipo kabisa kabisa? | 20- Kitabu cha Torati ya Mungu kilichotajwa katika (Yoshua 24:26).<br>21- Kitabu cha Torati ya Musa kilichotajwa katika (Yoshua 8:31).<br>22- Kitabu cha Sheria ya Musa kilichotajwa katika (Yoshua 23:6).<br>23- Kitabu cha Tarehe kilichotajwa katika (Nehemia 12:23).<br>24- Kitabu cha Tarehe ya Samweli Mwonaji kilichotajwa katika (1 Mambo ya Nyakati 29:29).<br>25- Kitabu cha Agano kilichotajwa katika (Kutoka 24:7). | yashikeni, na msipopewa haya jihadharini." Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumtia mtihani, hawezi kumpatia mbele ya Mwenyezi Mungu cho chote. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo zao (kwa kuwa wenyewe hawana raghba (mapenzi)). Watakuwa na fedheha duniani; na katika akhera watakuwa na adhabu kubwa). Almaidah 41. |
| Je, katika vitendo vya Mungu wa Agano la Kale ni kuwa yeye anapotosha, anaongopa na kuhadaa? | ''Ee BWANA, mbona umetukosesha njia zako...'' Isaya 63:17<br><br>''Nami nikasema, Aa, Bwana MUNGU! Hakika umewadanganya sana...'' Yeremia 4:10<br><br>''... mimi, BWANA, nimemdanganya nabii yule, ...'' Ezekieli 14:9<br><br>''... BWANA asema hivi, Tazama, ninafinyanga mabaya juu yenu...'' Yeremia 18:11 | (Basi adhabu kali itawathibitikia wanaoandika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: "Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu." (Wanasema uwongo huo) Ili wachukue thamani ndogo ya kilimwengu. Basi ole wao kwa yale waliyoyaandika kwa mikono yao (wakasingizia kuwa ya Mungu). Na ole wao kwa yale wanayoyachuma). Al Baqara 79. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anafunua kuwa, | Kuna tafsiri tofautitofauti za Mhubiri 7:11 | Hekima ni akili na kujidhibiti katika dini ya Allah. Nayo ni |


| | | |
|---|---|---|
| hekima pamoja na utajiri ni bora kwa mwanadamu? | Hekima pamoja na utajiri ni njema na ina manufaa zaidi kwa mwanadamu, kwa kuwa anakuwa na amani...'' (Tafsiri ya Pamoja.)<br><br>Hekima ni njema, mfano wa urithi; Naam, nayo ni bora kwao walionao jua.'' (Tafsiri ya Vandayk)<br><br>Hekima pamoja na urithi ni njema; na ina manufaa kwa waliohai". (Tafsiri ya kitabu cha Uhai) | kuitumia vizuri elimu na kutenda vizuri.<br><br>(Mwenyezi Mungu) Humpa hekima (akili yenye nafuu) amtakaye, na aliyepewa hekima bila shaka amepewa kheri nyingi. Na hawakumbuki ila wenye akili.) Albaqarah 269. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaibeza hekima ya masikini? | '... walakini hekima ya masikini hudharauliwa, wala maneno yake hayasikilizwi. '' Mhubiri 9:16 | (Na kwa yakini tulimpa Luqmani hekima, tukamwambia Mshukuru Mwenyezi Mungu...) Luqmani 12. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anafunua kuwa, mlo wa Suleimani ulikuwa wa kichokozi? | '' [22]Na vyakula vya Sulemani vya siku moja vilikuwa kori thelathini za unga mzuri, na kori sitini za ngano, [23]na ng'ombe kumi walionona, na ng'ombe ishirini za malisho, na kondoo mia, pamoja na ayala, na paa, na kulungu, na kuku walionona.'' 1 Wafalme 4:22-23 | Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Binadamu hajapatapo kujaza chombo cha shari zaidi kuliko tumbo. Binadamu inamtosha milo inayousimamisha mgongo wake. Na ikiwa lazima ale, basi aligawe tumbo lake, theluthi kwa ajili ya chakula, theluthi kwa vinywaji na theluthi kwa kupumulia). Imepokewa na Imamu Ahmad na Attirmidhiyyu. |
| Je, kwa Mungu wa Agano la Kale kuna mambo yanaingia moyoni mwake? | ''Nao wamepajenga mahali palipoinuka pa Tofethi, palipo katika bonde la mwana wa Hinomu, ili kuwateketeza wana wao na binti zao motoni; jambo ambalo mimi sikuliagiza, wala halikuingia moyoni mwangu.'' Yeremia 7:31 | (Mwenyezi Mungu yu mbali na sifa wanazompa.) As-saaffat 159. |
| Je, Mungu anahitaji azinduliwe ili afanye uadilifu? | ''Ee BWANA, unirudi kwa haki; si kwa hasira yako, usije ukaniangamiza.'' Yeremia 10:24 | (...Hakuna chochote mfano wake; naye ni mwenye kusikia, mwenye kuona.) As-shuura 11. |

<table>
<tr><td>Je, Mungu ana maliwato / bakuli la kunawia anawekea viatu vyake?</td><td>''[6]Mungu amenena kwa utakatifu wake,… [8]Moabu ni bakuli langu la kunawia.<br><br>Nitamtupia Edomu kiatu change...'' Zaburi 60:6-8</td><td>(Wala msiseme, kwa sababu ya uwongo usemao ndimi zenu, "Hii ni halali na hii ni haramu," msije mkamzulia uwongo Mwenyezi Mungu…). Annahli 116</td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale anajutia / anaghairi matendo yake?</td><td>''BWANA akaghairi...'' Amosi 7:3<br><br>''… maana BWANA alighairi...'' Waamuzi 2:18<br><br>''… naye BWANA akaghairi...'' 1 Samweli 15:35<br><br>''… naye BWANA akaghairi...'' Yeremia 26:19<br><br>''… kwa maana nayajutia mabaya niliyowatenda.'' Yeremia 42:10<br><br>''BWANA akaghairi...'' Mwanzo 6:6<br><br>''Huenda MUNGU akarudi na kughairi…) Yonani 3:9.</td><td>Allah ameepukana na kujuta: (Na ni nini dhana ya wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo, juu ya siku ya Qiayama? Hakika Mwenyezi Mungu ana fadhila (wema) nyingi juu ya watu. Lakini wengi wao hawashukuru). Yunus 60.</td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale anasifika na sifa (badaa) ya kubadili mtazamo wake?</td><td>Sifa ya BADAA: ni kubalisha rai baada ya jambo fulani kumdhihirihikia, jambo ambalo halikuwa limemdhihirihikia hapo kabla). Na sifa hii ya badaa kwa BWANA inapatikana katika Kutoka 32:14 licha ya tafsiri tofautofauti.<br><br><table><tr><td>BWANA akaghairi…</td><td>BWANA akarejea…</td><td>BWANA akajuta…</td></tr></table></td><td>(Na nani dhalimu zaidi kuliko Yule amzuliaye uwongo Mwenyezi Mungu au azikadhibishaye hoja zake?...) Al-An-am 21.</td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale anahuzunika na anaghairi?</td><td>''[6]BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo. [7]… kwa maana naghairi ya kwamba nimewafanya.'' Mwanzo 6:6-7</td><td>(Na nani dhalimu mkubwa kuliko Yule anayemzulia uwongo Mwenyezi Mungu….) Al-Ankabuuti 68.</td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale anachoka?</td><td>'' [14]Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zenu zilizoamriwa, nafsi yangu yazichukia; mambo hayo yanielemea; nimechoka kuyachukua.'' Isaya 1:14</td><td>(Na nani dhalimu mkubwa wa nafsi yake kuliko Yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo…). Assaff 7.</td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale hakumbuki ahadi yake ila kwa njia</td><td>''Mungu akasikia kuugua kwao, Mungu akakumbuka agano lake...'' Kutoka 2:24</td><td>(… Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko Yule afichae ushahidi alio nao utokao kwa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu si</td></tr>
</table>

<table>
<tr><td>ya upinde wa mvua?<br></td><td>“ [11]Na agano langu nitalithibitisha nanyi… [13] Mimi nauweka upinde wangu winguni, nao utakuwa ni ishara ya agano kati yangu na nchi. [14]Hata itakuwa nikitanda mawingu juu ya nchi… [16]Basi huo upinde utakuwa winguni; nami nitauangalia nipate kulikumbuka agano la milele…’’ Mwanzo 9:11-17</td><td>Mwenye kughafilika na hayo mnayoyafanya.) Albaqarah 140.</td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale anawafunulia Manabii kwa kauli ya kujisemea: “Ole wangu”?</td><td>‘’Ole wangu!...’’ Mika 7:1<br><br>“ [19 Ole wangu, kwa sababu ya jeraha yangu! Pigo langu laumia; lakini nalisema, Kweli, ni huzuni yangu mimi, nami sina budi kuivumilia.’’ Yeremia 10:19</td><td>(“Akasema: “Ilimu yake iko kwa Mola wangu katika kitabu (chake kilichokusanya kila kitu). Mola wangu hapotei wala hasahau.”) Ta ha 52.</td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale ana pindo za vazi lake?</td><td>‘’Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.’’ Isaya 6:1</td><td>(Na nani dhalimu mkubwa wa nafsi yake kuliko Yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo…). Assaff 7.</td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale ana maarifa?</td><td>‘’Nao husema, Mungu ajuaje? Yako maarifa kwake aliye juu?’’ Zaburi 73:11</td><td>(Je, huwajui kwamba Mwenyezi Mungu anajua siri zao na minong`ono yao, na kwamba Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye mambo ya ghaibu?) Attawba 78.</td></tr>
<tr><td>Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni neema ya kuwapigia kelele inzi, nyuki na Wamisri?</td><td><table><tr><td>Tafsiri ya Fandiyiku</td><td>Tofauti katika tafsiri ya Alhayatu</td></tr><tr><td>‘’Tena itakuwa katika siku hiyo BWANA atampigia kelele inzi aliye katika pande za mwisho za mito ya Misri, na nyuki aliye katika nchi ya Ashuru’’. Isaya 7:18</td><td>‘’Tena itakuwa katika siku hiyo BWANA atawapigia kelele wamisri na watakujieni katika kila pande za mwisho za mito ya Misri, na nyuki aliye katika nchi ya Ashuru na watakujieni kama makundi ya nzige.’’ Isaya 7:18</td></tr></table></td><td>(Na miongoni mwao kuna baadhi yao wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) kitabu ili mpate kuyafikiri (maneno) yao hayo kuwa ni ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu); na wanasema: “Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu”, na hali hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu; na wnamsingizia Mwenyezi Mungu uwongo na hali wanajua (kuwa huo ni uwongo). Aali Imran 78.</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| | ''…Naye atawapigia miunzi (miruzi) tokea mwisho wa nchi…'' Isaya 5:26<br><br>''Nitawapigia kelele, na kuwakusanya pamoja....'' Zekaria 10:8<br><br>Swali: Je, jeshi la Misri ni inzi? Na je, Mungu analipigia (miruzi) miunzi/kelele jeshi? | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anapiga makofi kwa kiganja na kiganja? | '' [14]Basi, wewe mwanadamu, tabiri, ukapige makofi… [17]Mimi nami nitapiga makofi, mimi nami nitashibisha ghadhabu yangu; mimi, BWANA, nimenena neno hili.'' Ezekieli 21:14-17 | (Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko Yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo?...) Hud 18. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni Mungu wa kisasi? | ''Ee BWANA, Mungu wa kisasi, Mungu wa kisasi, uangaze.'' Zaburi 94:1 | (Sema: "Enyi watu wa Kitabu! Je, mnatuona na kosa kwa kuwa tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyoteremshiwa na yale yaliyoteremshwa zamani, na kuwa wengi katika nyinyi ni maasi?...). Almaidah 59. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa yeye ni mwenye kuogofya? | ''nikasema, Nakusihi, Ee BWANA, Mungu wa mbinguni, Mungu mkuu, mwenye kuogofya…'' Nehemia 1:5<br><br>''Basi sasa, Ee Mungu, mkuu, mwenye uweza, Mungu wa kuogofya…'' Nehemia 9:32 | (Na ni nini dhana ya wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo, juu ya siku ya Kiyama? Hakika Mwenyezi Mungu anafadhila (wema) nyingi juu ya watu. Lakini wengi wao hawashukuru.) Yunus 60. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaamrisha kutengeneza sanamu za bawasiri/majipu? | ''Kwa hiyo mtafanyiza sanamu za majipu yenu, na sanamu za panya wenu wanayoiharibu nchi...'' 1 Samweli 6:5 | (Mwenyezi Mungu yu mbali na sifa wanazompa.) As-saaffat 159. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaadhibu tupu ya nyuma kwa bawasiri? | ''Lakini mkono wa BWANA ulikuwa mzito… akawapiga kwa majipu…'' 1 Samweli 5:6<br><br>''… akawapiga watu wa mjini… wakapatwa na majipu.'' 1 Samweli 5:9<br><br>''…walipigwa kwa yale majipu...'' 1 Samweli 5:12<br><br>''BWANA atakupiga kwa majipu ya Misri, na kwa bawasiri...'' Kumbukumbu la Torati 28:27 | (Ameepukana Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi – na hayo wanayomsifia). Az-Zukhruf 82. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuridhia dhulma dhidi ya Manabii?<br><br>Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kudhihirika kwa watu, kula na kunywa? | ''Naye Abramu akamwambia Sarai, Tazama, mjakazi wako yu mkononi mwako, mtendee lililo jema machoni pako. Sarai akamtesa, naye akakimbia kutoka mbele yake.'' Mwanzo 16:6<br><br>Swali: Je Mungu anaridhia dhuluma na udhalilishaji wa Sarai kwa Hajari?<br><br>''BWANA akamtokea Ibrahimu karibu na mialoni ya Mamre, alipokuwa ameketi mlangoni pa hema yake... [8]Akatwaa siagi na maziwa, na ndama aliyoiandaa, akawaandikia mbele yao, akasimama karibu nao chini ya mti, nao wakala. [9] Wakamwambia, Yu wapi Sara mkeo? Akasema, Yumo hemani... [16] ibrahimu akaenda pamoja nao awasindikize. [17] BWANA akanena, Je! Nimfiche Ibrahimu jambo nilifanyalo… [22] Basi wale watu wakatoka huko wakaelekea Sodoma; lakini Ibrahimu alikuwa akali akasimama mbele za BWANA [23] Ibrahimu akakaribia, akasema, Je! Utaharibu mwenye haki pamoja na mwovu?'' Mwanzo 18:1-23 | Wageni wa Ibrahimu, amani iwe juu yake, ni malaika. (Walipoingia kwake wakasema: "Salaam (Alaykum);" na (yeye ibrahimu ) akasema: "(Alaykums) salaam." (Na katika moyo wake anasema): "Nyinyi watu nisiokujueni." Mara akaenda kwa ahli yake na akaleta ndama aliyenona. akampeleka karibu yao. (Walipokuwa hawajanyoosha mikono kula) Alisema: "Mbona hamli!") Adh-dhaariyat 25-27.<br><br>(Akasema: "(Tena) kusudi lenu (jengine) ni nini enyi mliotumwa?" Wakasema: "Hakika sisi tumetumwa kwa wale watu wakosaji (tukawaangamize)." (Watu wa Nabii Luti.) "Isipokuwa waliomfuata Luti. Bila shaka sisi tutawaokoa wote hao (waliomfuata Luti)". "Isipokuwa mkewe. Tunapimia ya kuwa atakuwa miongoni mwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | watakaokaa nyuma (waangamizwe)." Al-Hijr 57-60. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kusimama juu ya ngazi?<br> | " [12] … na tazama, ngazi imesimamishwa juu ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni... [13] Na tazama, BWANA amesimama juu yake...'' Mwanzo 28:12-13 | (Sema: "Wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo hawatafaulu.") Yunus 69. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuteremka ili kuokoa, kuamka na kukaa katika wangwa (bonde) Yehoshafau? | ''Nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri...'' Kutoka 3:8<br><br>''Mimi nitashuka pamoja nawe mpaka Misri; nami nitakupandisha tena…'' Mwanzo 46:4<br><br>''Mataifa na wajihimize, wakapande juu katika bonde la Yehoshafau; maana huko ndiko nitakakoketi niwahukumu mataifa yote yaliyo pande zote.'' Yoeli 3:12 | (Na hawakumheshimu Mwenyezi Mungu hishima ipasayo. Na siku ya Kiama ardhi yote itakuwa mkononi Mwake, na mbingu zitakunjwa katika mkono Wake wa kuume, (kulia). Ameepukana na upungufu na yu juu kabisa kuliko yale wanayomshirikishiya.) Azzumar 67. |
| Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano | ''[2] BWANA akaniambia, Lango hili litafungwa, halitafunguliwa, wala mtu awaye yote hataingia kwa lango hili, kwa maana BWANA, Mungu wa | (Basi ni nani dhalimu kuliko yule amtungiaye Mwenyezi Mungu uwongo, na akadhibishaye Aya |

| | | |
|---|---|---|
| la Kale ni kuingia mlangoni? | Israeli, ameingia kwa hilo; basi kwa sababu hiyo litafungwa.'' Ezekieli 44:2 | zake? Hakika hawafaulu wale wafanyao maovu.) Yunus 17. |
| Je, miongoni mwa maamrisho ya Mungu wa Agano la Kale ni kuwakopesha kwa riba wasiokuwa Wayahudi? | ''Usimkopeshe ndugu yako kwa riba; riba ya fedha, riba ya vyakula, riba ya kitu cho chote kikopeshwacho kwa riba; mgeni waweza kumkopesha kwa riba, ili BWANA, Mungu wako, apate kukubarikia…'' Kumbukumbu la Torati 23:19-20 | (Wale wanaokula riba, hawasimami (kuendesha yao) ila kama anavyosimama Yule ambaye Shetani kamzuga kwa kumgusa; (wako mbioni tu, hawana kituo)… Albaqarah 275<br><br>(Mwenyezi Mungu huyafutia (Baraka mali ya) riba. Na huyatia Baraka (mali yaliyotolewa) sadaka...) Albaqarah 275 |
| Je, miongoni mwa maamrisho ya Mungu wa Agano la Kale ni kumwadhibu mtoto mkaidi kwa kumpopoa mawe hadi afe badala ya kumnasihi? | ''Mtu akiwa na mwana mkaidi, mshupavu, asiyetii sauti ya baba yake, wala sauti ya mama yake, nao wajapomwadhibu hawasikizi, ndipo babaye na mamaye na wamkamate, na kumpeleka kwa wazee wa mji wake, katika lango la mahali pake; wawaambie wazee wa mji wake, Huyu mwana wetu ni mkaidi, mshupavu, hasikizi sauti yetu; ni mwasherati, tena ni mlevi. Waume wote wa mji wake na wamtupie mawe, afe…'' Kumbukumbu la Torati 21:18-21<br><br>Swali: kwa nini baba na mama wanamzidishia mtoto wao sifa ambazo si zake, nazo ni ''mwasherati, mlevi''… Je, ni kuwaridhisha wazee wa mji wampige mawe? | Kuendelea kuwanasihi watoto, na kupandikiza mahaba ya Allah na Mtume wake, Rehema na amani ziwe juu yake, katika nyoyo zao, na kuwaepusha na marafiki waovu, na kuwavutia wapende kukaa na watu wema pamoja na kukimbilia kwa Allah kwa kuomba dua ili watengenekewe.<br><br>(Na wale wanaosema: "Mola wetu! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho (yetu) (nyoyo zetu), na utujaalie kuwa waongozi kwa wamchao (Mungu). Alfurqan 74. |
| Je, Mungu wa majeshi ni mwenye kuketi katika tabuti akitazama dansi? Je, Mungu anamruhusu nabii Daudi | " [5] Daudi na nyumba yote ya Israeli wakacheza mbele za BWANA kwa nguvu zao zote, kwa nyimbo, na kwa vinubi, na kwa vinanda, na kwa matari, na kwa kayamba, na kwa matoazi.'' 2 Samweli 6:5 | (…Hakuna chochote mfano wake; naye ni mwenye kusikia, mwenye kuona.) As-shuura 11. |

| | | |
|---|---|---|
| acheze dansi na kuwataka watumishi wapige vinanda na vinubi? | ''Daudi akacheza mbele za BWANA kwa nguvu zake zote...'' 2 Samweli 6:5,14<br><br>''Tena Daudi na maakida wa jeshi wakatenga kwa utumishi baadhi ya wana wa Asafu, na wa Hemani, na wa Yeduthuni, watakaotabiri kwa vinubi na vinanda, na matoazi; hii ndiyo hesabu ya wafanya kazi sawasawa na utumishi wao;'' 1 Mambo ya Nyakati 25:1 | |
| Je, alipopiga kinanda; mkono wa Mungu ulikuwa juu yake?<br><br>Je, Manabii wa kike wa Mungu wanabashiri kwa madufu/tari na kudansi?! | ''[14]Elisha akasema... [15]Ila sasa niletee mpiga kinanda. Ikawa, mpiga kinanda alipokipiga, mkono wa BWANA ukamjia juu yake.'' 2 Wafalme 3:14-15<br>---<br>''Na Miriamu, nabii mke, ndugu yake Haruni, akatwaa tari mkononi mwake; wanawake wakatoka wote wakaenda nyuma yake, wenye matari na kucheza.'' Kutoka 15:20 | (Mwenyezi Mungu yu mbali na sifa wanazompa.) As-saaffat 159. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaruhusu Agano la Kale lipotoshwe? Na kuruhusu matendo ya Manabii na Makuhani ili kujipatia pato la uovu na uongo? | ''[8] Mwasemaje, Sisi tuna akili, na torati ya BWANA tunayo pamoja nasi? Lakini, tazama, kalamu yenye uongo ya waandishi imeifanya kuwa uongo. [9]Wenye hekima wametahayari, wamefadhaika na kushikwa; tazama, wamelikataa neno la BWANA, wana akili gani ndani yao? [10]Basi, kwa hiyo nitawapa watu wengine wake zao na mashamba yao nitawapa wale watakaowamiliki; maana kila mmoja wao, tangu aliye mdogo hata aliye mkubwa, ni mtamanifu; tangu nabii hata kuhani, kila mmoja hutenda mambo ya udanganyifu.'' Yeremia 8:8-10 | (Basi adhabu kali itawathibitikia wanaoandika kitabu kwa mikono yao, kisha wakasema: "Hiki kimetoka kwa Mwenyezi Mungu." (Wanasema uwongo huo) Ili wachukue thamani ndogo ya kilimwengu. Basi ole wao kwa yale waliyoyaandika kwa mikono yao (wakasingizia kuwa ya Mungu). Na ole wao kwa yale wanayoyachuma.) Al Baqara 79. |

| | | |
|---|---|---|
| Ni nani aliyemuamrisha Daudi kufanya sensa? Je, ni Mungu au Shetani? | ''Tena hasira ya BWANA ikawaka juu ya Israeli, akamtia Daudi nia juu yao, akisema, Nenda, ukawahesabu Israeli na Yuda.'' 2 Samweli 24:1<br><br>''Tena shetani akasimama juu ya Israeli, akamshawishi Daudi kuwahesabu Israeli.'' 1 Mambo ya Nyakati 21:1 | (... Basi ni nani dhalimu mkubwa kuliko Yule amzuliaye Mwenyezi Mungu uwongo?) AlKahf 15. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaadhibu kwa kufunua kipara? | ''Nami nitazigeuza sikukuu zenu kuwa maombolezo, na nyimbo zenu zote kuwa vilio; nami nitatia nguo za magunia katika viuno vyote, na upaa (upara) katika kila kichwa...'' Amosi 8:10 | |
| Je, manabii wa Mungu wa Agano la Kale wanamwendea Mungu kwa utovu wa adabu, ufedhuli na ujasiri? | Mussa anaongea na Mungu kwa ufedhuli wote<br><br>''[11] Musa akamwambia BWANA, Mbona umenitenda uovu mimi mtumishi wako? Kwa nini sikupata neema machoni pako?... [12]Je! Ni mimi niliyewatungisha mimba watu hawa wote je! Ni mimi niliyewazaa, hata ikawa wewe kuniambia, Haya, wachukue kifuani mwako... Mimi siwezi kuwachukua watu hawa wote peke yangu, kwa kuwa ni mzigo mzito sana wa kunishinda. [15]Na kama ukinitenda hivi, nakuomba uniulie mbali... Musa anakabiliana na Mungu kwa ujasiri.'' Hesabu 11:11-15<br><br>Musa anakabiliana na Mungu kwa ujasiri:<br><br>''[22]Musa akarudi kwa BWANA, akasema, BWANA, mbona umewatenda mabaya watu hawa? Kwani kunituma mimi?: [23]Kwa maana tangu nilipokwenda kwa Farao, kusema naye kwa jina lako, amewatenda mabaya watu hawa; wala hukuwaokoa watu wako hata kidogo.'' Kutoka 5:22-23<br><br>Nabii Eliya anampayukia Mungu kwa maneno yasiyofaa:<br><br>'' [20] Akamwomba BWANA, akanena, Ee BWANA, Mungu wangu, je! Umemtenda mabaya mjane | Muislamu anamnyenyekea Allah Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu.<br><br>(Anayeghufiria dhambi na nayepokea toba, Mkali wa kuadhibu, Mwenye ukarim; hakuna aabudiwaye kwa haki ila yeye; (na) marejeo ni kwake.) Muumin 3.<br><br>Ilikuwa ni lazima kwa kila Muislamu mwanamume na muislamu mwanamke atekeleze adabu za kuomba dua, ili dua yake ikubaliwe, na kwa kufanya hilo atakuwa anafuata mwongozo wa Mtume Rehema na amani ziwe juu yake katika kuomba dua. |

| | | |
|---|---|---|
| | huyu ninayekaa kwake hata kumfisha mwanawe. [21]Akajinyosha juu ya mtoto mara tatu, akamwomba BWANA, akanena, Ee BWANA, Mungu wangu...'' 1 Wafalme 17:20-21 | |
| Je, miongoni mwa sifa za Yesu (Nafsi ya pili) ni kuwa yeye awe na miujiza midogo kuliko ya Eliya? | Eliya anakifanya chakula kiwe kingi kwa idhini ya Mungu: ''[12]Naye akasema, Kama BWANA, Mungu wako, aishivyo, sina mkate, ila konzi ya unga katika pipa, na mafuta kidogo katika chupa… [15]Basi akaenda, akafanya kama alivyosema Eliya; na yeye mwenyewe, na Eliya, na nyumba yake, wakala siku nyingi. [16]Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha, sawasawa na neno la BWANA alilolinena kwa kinywa cha Eliya.'' 1 Wafalme 17:12-16<br><br>Eliya na Eliasa wanafufua wafu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu: [17]Ikawa, baada ya hayo, mwana wake yule mwanamke, bibi wa nyumba ile, akaugua; ugonjwa wake ukazidi hata akawa hana pumzi tena… [21]... Akajinyosha juu ya mtoto mara tatu, akamwomba BWANA, akanena, Ee BWANA, Mungu wangu, nakusihi, roho ya mtoto huyu imrudie ndani yake tena. BWANA akaisikia sauti ya Eliya; na roho ya mtoto ikamrudia akafufuka.'' 1 Wafalme 17:17-22 ''[32]Basi Elisha alipofika nyumbani, tazama, mtoto amekwisha kufa, amelazwa kitandani pake. [33]Basi akaingia ndani, akajifungia mlango, yeye na yule mtoto wote wawili, akamwomba BWANA. [34] … akapanda, akajinyosha juu yake; na yule mtoto akapiga chafya mara saba, na mtoto akafumbua macho yake.'' 2 Wafalme 4:32-35<br><br>Eliya anaomba mvua na mvua inanyesha kwa idhini ya Mungu: ''Kawa baada ya siku nyingi, neno la BWANA likamjia Eliya, katika mwaka wa tatu, kusema, Enenda, ukajionyeshe kwa Ahabu; nami nitaleta mvua juu ya nchi…. 45 Ikawa, muda si | Muujiza ni jambo lililo nje ya kanuni za kimaumbile ya kawaida linalodhihirishwa na Allah Mtukufu kwa idhini yake katika mikono ya manabii na mitume yake. Ukiwa ndio ushahidi wa ukweli wa utume wao, pia ni changamoto kwa washirikina. Hivyo ni lazima kwa kila muujiza uwe nje na kanuni za kimaumbile zilizozoeleka. Pia muujiza unabeba ujumbe kwenda katika akili za watu. Hivyo mtu anapokubali ushahidi wa muujiza anamwamini Mtume na kuuthibitisha utume wake.<br><br>Miujiza yote ya Nabii Issa, amani iwe juu yake, ni kwa idhini ya Allah, kwa mfano: Kuwaponya wenye mbaranga, vipofu, na kuhuisha wafu, na kutengeneza sanamu la ndege kwa udongo kisha kulipulizia na hilo sanamu kuwa ndege wa ukweli. Na kushuka kwa meza yenye chakula kutoka mbinguni.<br><br>Miujiza yote ya Mtume Muhammad, Rehema na amani ziwe juu yake, ni kwa idhini ya Allah, kwa mfano: Muujiza wa Quran Tukufu (Maneno ya Allah Mtukufu), kupasuka kwa mwezi, |

| | | |
|---|---|---|
| | muda, mbingu zikawa nyeusi kwa mawingu na upepo, ikanyesha mvua nyingi…'' 1 Wafalme 18:1-45<br><br>Eliya anahudumiwa na Malaika kwa idhini ya Mungu: [5] …na tazama, malaika akamgusa, akamwambia, Inuka, ule. [6] Akatazama, kumbe! Pana mkate umeokwa juu ya makaa, na gudulia la maji, kichwani pake. Akala, akanywa, akajinyoosha tena. [7]Malaika wa BWANA akamwendea mara ya pili, akamgusa, akasema, Inuka, ule; maana safari hii ni kubwa mno kwako.'' 1 Wafalme 19:5-7<br><br>Eliya anateremsha mvua kutoka mbinguni kwa idhini ya Mungu: ''[10]Eliya akajibu, akamwambia yule akida wa hamsini, Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka mbinguni, ukuteketeze wewe na hamsini wako. Moto ukashuka, ukamteketeza, yeye na hamsini wake.'' 2 Wafalme 1:10<br><br>Eliya amepiga maji, yakagawanyika huku na huku:<br><br>''Eliya akalitwaa vazi lake la juu, akalikunja, akayapiga maji, yakagawanyika huku na huku, na hao wawili wakavuka pakavu.'' 2 Wafalme 2:8<br><br>Eliya anapanda mbinguni kwa idhini ya Mungu<br><br>''Ikawa, walipokuwa wakiendelea mbele na kuongea, tazama! Kukatokea gari la moto, na farasi wa moto, likawatenga wale wawili; naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli.'' 2 Wafalme 2: 11<br><br>Elisha alisha watu mia moja kwa mikate ishirini tu: ''[42]Tena, akaja mtu kutoka Baal-shalisha, | Safari ya Israa na Miraji (kupanda mbinguni), kukifanya chakula na kinywaji kiwe kingi, kuomba mvua na mvua kunyesha. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, miongoni mwa sifa za Yesu (Nafsi ya pili) ni kuwa yeye awe na miujiza midogo kuliko ya Elisha? | akamletea mtu wa Mungu chakula cha malimbuko, mikate ishirini ya shayiri… Akasema, Uwape watu, ili wale… [44] Basi akawaandikia, nao wakala, wakasaza, sawasawa na neno la BWANA. '' 2 Wafalme 4:42-44<br><br>Elisha anaponya wagonjwa kwa idhini ya Mungu: […. 14 Basi Naamani akaja na farasi wake na magari yake, akasimama mlangoni pa nyumba ya Elisha….. Ndipo akashuka, akajichovya mara saba katika Yordani, sawaswa na neno lake Yule mtu wa Mungu; nayo nyama ya mwili wake ikarudi ikawa kama nyama ya mwili wa mtoto mchanga, akawa safi.'' 2 Wafalme 5:3-14<br><br>Elisha anajua mambo yaliyofichikana kwa idhini ya Mungu: ''[12]Mmojawapo wa watumishi wake akasema, La, bwana wangu, mfalme; lakini Elisha, yule nabii aliye katika Israeli, humwambia mfalme wa Israeli maneno uyanenayo katika chumba chako cha kulala.'' 2 Wafalme 6:12,20<br><br>Elisha anamponya kipofu kwa idhini ya Mungu: ''[20]Hata walipokwisha kuingia Samaria, Elisha akasema, BWANA wafumbue macho watu hawa, wapate kuona. BWANA akawafumbua macho wakaona; kumbe! Walikuwa katikati ya Samaria.'' 2 Wafalme 6:20 | |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| | Mpendwa msomaji:<br><br>Baada ya kusoma sura ya nne katika kitabu hiki.<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale ana matendo, kufanana, sifa na amri za kuchukiza? | |
| Sura ya Tano: Je, miongoni mwa sifa za Mungu ni kwamba yeye ni Mbabe wa kivita na mhamasishaji Ugaidi? | | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni gaidi anayeamrisha mauaji, kuangamiza watu, kuweka makazi ya walowezi, kufukuza wakazi na ubakaji?<br><br>Je, maamrisho ya Mungu ni uuaji na kubeba upanga?<br><br>Je, Mungu ni mbabe wa kivita hadi anaamrisha mauaji? | ''BWANA ni mtu wa vita...'' Kutoka 15:3 ''BWANA atatokea kama shujaa; Ataamsha wivu kama mtu wa vita; Atalia, naam, atapiga kelele; Atawatenda adui zake mambo makuu.'' Isaya 42:13<br><br>''[5]… Piteni kati ya mji nyuma yake, mkapige; jicho lenu lisiachilie, wala msione huruma; [6] Waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika patakatifu pangu. Basi, wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba. [7]Akawaambia, itieni nyumba unajisi, mkazijaze nyumba mizoga ya hao waliouawa; haya, enendeni. Wakaenenda, wakapiga-piga katika mji.'' Ezekieli 9:5-7 ''[17]Na mji huu utakuwa wakfu kwa BWANA… [21]Basi wakaangamiza kabisa vitu vyote vilivyokuwa ndani ya mji, wanaume na wanawake, watoto na wazee, na ng'ombe, na kondoo, na punda, kwa makali ya upanga.'' Yoshua 6:17-21 ''BWANA, Mungu wako, atakapoyakatilia mbali hayo mataifa mbele yako, huko uingiako kuyamiliki, nawe ukawatwaa, na kuketi katika nchi yao.'' Kumbukumbu 12:29<br><br>''Akawaambia, BWANA, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata | Vita katika Uislamu ina falsafa inayoweza kufupishwa katika nukta zifuatazo:<br><br>Mosi: Vita katika Uislamu ni vita ya kusimika haki na kuondosha batili.<br><br>Pili: Vita katika Uislamu ni vita ya kuurejesha nyuma uadui na kuutokomeza uadui.<br><br>Tatu: Vita ya kutangaza itikadi ya Kiislamu na kuilinda, bila ya kumlazimisha yeyote asilimu.<br><br>Nne: vita ya kuondoa dhulma na ufisadi duniani.<br><br>Allah anamwamrisha Mtume wake Muhammad, Rehema na amani ziwe juu yake, apigane vita ili kulinda roho, heshima, mali na dini. Kwa hiyo Uislamu sio dini ya kuangamiza wengine na ugaidi, hakuna katika Quran Tukufu Waueni wazee, wanawake, watoto na |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu anaamrisha mauaji ya kimbari hadi kuwamaliza wanaouawa?<br><br>Je, Mungu anaamrisha kuua kwa upanga?<br><br>Je, Mungu anaamrisha kuangamiza miji ya waabudu masanamu?<br><br>Kwa mfano, kwa nini Mungu hawatangazii watu waingie katika dini ya Kiyahudi au vinginevyo walipe kodi?<br><br>Je, sheria ya Mungu wakati wa kuzingira na kuteka miji ya ahadi ni kuwaangamiza | mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake.'' Kutoka 32:27 ''[11] Itakuwa utakapokujibu kwa amani, na kukufungulia, ndipo watu wote watakaoonekana humo watakufanyia kazi ya shokoa, na kukutumikia. [12]Na kwamba hautaki kufanya amani nawe, lakini utafanya vita juu yako, ndipo uuhusuru; [13]na BWANA, Mungu wako, autiapo mkononi mwako, mpige kila mume aliyemo kwa makali ya upanga; [14]lakini wanawake na watoto, na wanyama wa miji, na vilivyo mjini vyote, navyo ni nyara zake zote, uvitwae viwe mateka kwako; nawe utakula nyara za adui zako alizokupa BWANA, Mungu wako. [15]Utaifanyia vivyo miji yote iliyo mbali sana nawe, isiyokuwa miji ya mataifa haya. [16]Lakini katika miji ya mataifa haya akupayo BWANA, Mungu wako, kuwa urithi, usihifadhi kuwa hai kitu cho chote kipumzikacho; [17]lakini uwaangamize kabisa, Mhiti, na Mwamori, na Mkanaani, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi…'' Kumbukumbu la Torati 20:11-17 ''Nami nitawatawanya kwa pepo zote wote wamzungukao ili wamsaidie, na vikosi vyake vyote; nami nitaufuta upanga nyuma yao.'' Ezekieli 12:14<br><br>''Ninyi mmeuogopa upanga; nami nitauleta upanga juu yenu, asema Bwana MUNGU.'' Ezekieli 11:8<br><br>''[15]hakika yako uwapige wenyeji wa mji ule kwa makali ya upanga…. [16]Na nyara zake zote uzikusanyie katikati ya njia yake; na mji uuteketeze kwa moto, na nyara zake zote, kuwe sadaka.'' Kumbukumbu la Torati 13:15-16<br><br>''Kisha BWANA akamwambia Musa, Watwae wakuu wote wa hao watu, ukamtungikie BWANA watu hao mbele ya jua, ili kwamba hizo hasira kali za BWANA ziwaondokee Israeli.'' Hesabu 25:4 | waliojitenga na vita… hii ni tofauti na maandiko ya Biblia.<br><br>Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, ameliusia jeshi la mujahidina kwa kusema: (Nendeni kwa jina la Allah, na kwa ajili ya Allah, na kwa mila ya Mtume wa Allah, wala msimuue mzee mkongwe, wala kichanga, wala mtoto, wala mwanamke, msizidishe, waunganisheni wanyama wenu, tengenezeni, fanyeni wema, hakika Allah anawapenda wafanya wema.) Ziada ya Aljaamiu Asswaghiiru – cha Imamu Assuyuutwiyu.<br><br>Na kauli ya Mtume, Rehema na amani ziwe juu yake, Nendeni kwa jina la Allah, na katika njia Allah, muueni aliyemkufuru Allah, wala msicharangecharange maiti, wala msiende kinyume na makubaliano, wala msizidishe, wala msimuue mtoto mchanga). (Imepokewa na Muslimu katika sahihi yake 3/1357 pia imepokewa na Ibnu Maajah).<br><br>Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetukuka anasema: (… Na wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni). Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi warukao mipaka.) Albaqarah 190. |

| | | |
|---|---|---|
| kabisakabisa watu wa mataifa sita yaliyoishi kabla yao?<br><br>Je, sheria ya Mungu wakati wa kuzingira na kuteka miji ya mbali ni<br><br>kuwatia wakazi wake utumwani au kuwazingira. Na ukipatikana ushindi ni kuwauwa wanamume wote na kuwateka wanawake na watoto, kupora na kufaidi nyara?<br><br>Je, huyu ni Mungu mlezi asiyebagua baina ya viumbe wake?<br><br>Je, hasira kali za BWANA zinapoa na kurudi nyuma endapo wakuu wa watu watatungikwa na | ''Naye akawatoa watu waliokuwamo, akawaweka kwenye kazi ya misumeno, na sululu za chuma, na mashoka ya chuma, akawatumikisha tanuuni mwa matofali; ndivyo alivyoifanya miji yote ya wana wa Amoni. Kisha Daudi akarudi na watu wote Yerusalemu.'' 2 Samweli 12:31 ''Na hao watu waliokuwamo akawatoa, akawakata-kata kwa misumeno, na kwa sululu za chuma, na kwa mashoka...'' 1 Mambo ya Nyakati 20:3<br><br>''[10]Utakaposogea karibu ya mji kwenda kupigana juu yake, ndipo utakapowapigia ukelele wa amani. [11]Itakuwa utakapokujibu kwa amani, na kukufungulia, ndipo watu wote watakaoonekana humo watakufanyia kazi ya shokoa, na kukutumikia. [12]Na kwamba hawataki kufanya amani nawe, lakini utafanya vita juu yako, ndipo uuhusuru; [13]na BWANA, Mungu wako, autiapo mkononi mwako, mpige kila mume aliyemo kwa makali ya upanga; [14]lakini wanawake na watoto, na wanyama wa miji, na vilivyo mjini vyote, navyo ni nyara zake zote, uvitwae viwe mateka kwako; nawe utakula nyara za adui zako alizokupa BWANA, Mungu wako. [15]Utaifanyia vivyo miji yote iliyo mbali sana nawe, isiyokuwa miji ya mataifa haya.'' Kumbukumbu la Torati 20:10-15<br><br>''Kwa maana nitawakusanya mataifa yote walete vita juu ya Yerusalemu; na huo mji utapigwa, nazo nyumba zitatekwa, nao wanawake watatendwa jeuri; na nusu ya watu wa mji watatoka kwenda utumwani; ila mabaki ya watu wa mji hawatakatiliwa mbali.'' Zekaria 14:2<br><br>Swali: Je, Wayahudi na Wakristo walilisoma vizuri Agano la Kale pale walipozivamia na kuziteka kwa mfano: Nchi ya Palestina na mabara ya Amerika na | (… atakayemwua mtu bila ya yeye kuua mtu, au bila ya kufanya fisadi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote; na mwenye kumwacha mtu hai (kumsaidia kuishi) ni kama amewaacha hai watu wote...) Almaidah 32.<br><br>(Wala msifanye uharibifu katika nchi baada ya kuwa imekwisha kutengenezwa…). Al-Aaraf 57.<br><br>(… (Pia) wala msiwapunguzie watu vitu vyao wala msifanye uharibifu katika ardhi baada ya kutengenea kwake. Hivi ndivyo bora kwenu ikiwa nyinyi mmeamini." Al-Aaraf 85.<br><br>Waislamu hawajapatapo kupigana vita na upande wowote bila ya sababu, kwa ajili hiyo amesema Mola Mtukufu Aliyetukuka: (Mmelazimishwa kupigana vita (kwa ajili ya dini). Nalo ni jambo zito kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu, nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu ndiye anayejua, (lakini) nyinyi hamjui.) Albaqarah 216.<br><br>Na ayah hii ndio aya ya kwanza kutermka katika aya za vita. Na |

<table>
<tr>
<td>
kusulubiwa juani?
Je, Mungu anaamrisha watu wapasuliwe kwa misumeno?
Je, Mungu anaamrisha wauliwe wanamume, kuwafedhehesha wanawake na kuwateka mabinti mabikra?
Je, Mungu ni mwovu wa kivita hadi aamrishe kuuwawa kwa watoto?
Je, Mungu ni gaidi! Hadi anaamrisha kuwaangamiza kikamilifu?
</td>
<td>
Australia na kutekeleza vilivyo mafundisho ya (kitabu cha Kumbukumbu la Torati 20:10-17?!
<table>
<tr>
<td>Na watoto wao wachanga watapasuliwa-pasuliwa mbele ya macho yao, nyumba zao zitaporwa, na wake zao watabakwa.</td>
<td>Na watoto wao wachanga watavunjwa-vunjwa mbele ya macho yao, nyumba zao zitatekwa nyara, na wake zao watatendwa jeuri.</td>
</tr>
<tr>
<td colspan="2">Isaya 13:16</td>
</tr>
</table>
‘’Heri yeye atakayewakamata wadogo wako, na kuwaseta wao juu ya mwamba.’’ Zaburi 137:9 ‘’Na nyuta zao zitawaangusha vijana; wala hawatahurumia mazao ya tumbo; jicho lao halitawahurumia watoto.’’ Isaya 13:18 ‘’Basi sasa enda ukawapige Amaleki, na kuviharibu kabisa vitu vyote walivyo navyo, wala msiwaachilie; bali waueni, mwanamume na mwanamke, mtoto naye anyonyaye, ng’ombe na kondoo, ngamia na punda.’’ 1 Samweli 15:3
‘’Nitawagonganisha, mtu na mwenzake, naam, baba za watu na watoto wao pamoja, asema BWANA; sitahurumia, wala sitaachilia, wala sitarehemu, hata nisiwaangamize.’’ Yeremia 13:14
‘’[5]… Piteni kati ya mji nyuma yake, mkapige; jicho lenu lisiachilie, wala msione huruma; [6] Waueni kabisa, mzee, na kijana, na msichana, na watoto wachanga, na wanawake; lakini msimkaribie mtu ye yote mwenye hiyo alama; tena anzeni katika patakatifu pangu. Basi, wakaanza kwa wazee waliokuwa mbele ya nyumba. [7]Akawaambia, itieni nyumba unajisi, mkazijaze nyua mizoga ya hao
</td>
<td>
sababu ya kushuka kwake ni uadui wa washirikina na makafiri unaoendelea dhidi ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na dhidi ya walioamini wito wake miongoni mwa waislamu. Kuna aya nyingine za kulinda nafsi na kumzuia adui…
Na aya za jihadi sio za kuwaua watu burebure. Na kwa hakika aya hizo ni za vita ya kisaikolojia zaidi kuliko vita ya vitendo vya mauaji. Kwani kuwapigania jihadi watu kwa maneno ndio jambo la kwanza kisha ndipo linakuja jambo lingine… na kupambana jihadi ya vitendo kunakuwa ama kwa kutumia nguvu, ndio ufumbuzi wa mwisho kwa mwislamu.
(… Na kama wakijitenga wasipigane nanyi na wakakuleteeni amani, basi Mwenyezi Mungu hakukufanyieni njia juu yao.) Annisaa 90.
(Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na wale wanaokupigeni, wala msipindukie mipaka (mkawapiga wasiokupigeni). Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi warukao mipaka. Lakini kama wakikoma, (basi); na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa
</td>
</tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| | waliouawa; haya, enendeni. Wakaenenda, wakapiga-piga katika mji.’’ Ezekieli 9:5-7 | kurehemu…). Albaqarah 190 – 193. |
| Je, Mungu anaamrisha kuuawa kwa watoto na kuwafedhehesha wanawake? | ‘’na ya kwamba ye yote asiyemtafuta BWANA, Mungu wa Israeli, atauawa, akiwa mdogo au mkubwa, kwamba ni mwanamume au mwanamke.’’ 2 Mambo ya Nyakati 15:13 | (Na piganeni nao mpaka yasiweko mateso, na dini iwe kabisa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu Anayaona wanayoyatenda). Al-Anfal 38. |
| Je, Mungu anaamrisha kuwasaga na kuchinja watu kwa njia za kishenzi?<br><br>Je, Mungu ni mshenzi hadi aamrishe kuwasagasaga watoto kwa jiwe? | ‘’[7]Nao wakapigana na Midiani kama BWANA alivyomwagiza Musa; nao wakamwua kila mume. [8]Nao wafalme wa Midiani wakawaua pamoja na watu wengine waliouawa… [9]Wana wa Israeli wakawachukua mateka wanawake wa Midiani na watoto wao; na ng’ombe zao wote, na kondoo zao wote, na mali zao zote, wakachukua nyara. [10]Na miji yao yote, kila mahali walipokuwa wakikaa, na marago yao yote wakayateketeza kwa moto. [11] Nao wakatwaa hizo nyara zote, na mateka yote, ya wanadamu na ya wanyama… [15]Musa akawauliza, Je! Mmewaponya wanawake wote hai? 16]Tazama, hawa ndio waliowakosesha wana wa Israeli… [17]Basi kwa ajili hiyo mwueni kila mume katika hao watoto, na kila mwanamke aliyemjua mume kwa kulala pamoja naye.’’ Hesabu 31:7-17 | (Basi waandalieni (wawekeeni tayari) nguvu mziwezazo (silaha), na mafarasi yaliyofungwa (kufuga), tayari tayari (mipakani). Ili kwazo (nguvu hizi) muogopeshe maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, (mnaowajua) na (pia maadui zenu) wengineo wasiokuwa wao, msiowajua nyinyi (lakini) Mwenyezi Mungu anawajua. Na chochote mtakachokitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu (kama hii misaada ya vita vya jihadi) mtarudishiwa kamili sawasawa wala hamtadhulumiwa. Na kama (hao maadui) wakielekea katika amani, nawe pia ielekee, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika yeye ndiye asikiaye (na) ajuaye.) An-Anfal 60 – 61 |
| Je, Mungu mwovu wa kivita?<br><br>Je, Mungu anafunua kuwachinja watu? | ‘’Basi Yoshua akaupiga moto mji wa Ai, na kuufanya kuwa ni chungu ya magofu hata milele, kuwa ni ukiwa hata siku hii ya leo.’’ Yoshua 8:28 ‘’Siku hiyo Yoshua akautwaa mji wa Makeda, akaupiga kwa makali ya upanga, na mfalme wake; akawaangamiza kabisa na wote pia waliokuwamo ndani yake, hakumwacha hata mmoja aliyesalia; naye akamfanyia huyo mfalme wa Makeda kama alivyomfanyia huyo mfalme wa Yeriko.’’ Yoshua 10:28 | (Isipokuwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa washirikina kisha hawakuwapunguzieni cho chote, wala hawakuwasaidia wo |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale anahubiri kuua bila ya huruma tena kwa misingi ya ukabila/ kibaguzi?<br><br>Je, Mungu ni adui wa mazingira?<br><br>Je, Mungu anafunua mambo yote haya ya kigaidi?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale ni mshenzi, mmwaga damu, mkatili na mwovu wa kivita!?<br><br>Je, Mungu ni mmwaga damu? | ''[38]Kisha Yoshua akarudi, na Israeli wote pamoja naye, hata Debiri; nao wakapigana nao; [39]kisha akautwaa, na mfalme wake, na miji yake yote; nao wakawapiga kwa makali ya upanga, wakawaangamiza kabisa wote pia waliokuwamo ndani yake; hakumwacha hata mmoja aliyesalia; kama alivyoufanyia Hebroni aliufanyia na Debiri vivyo, na mfalme wake; kama alivyoufanyia Libna, na mfalme wake. [40]Basi Yoshua akaipiga nchi hiyo yote, nchi ya vilima, na nchi ya Negebu, na nchi ya Shefela, na nchi ya matelemko, na wafalme wake wote; hakumwacha aliyesalia hata mmoja; lakini akawaharibu kabisa wote waliokuwa wavuta pumzi, kama BWANA, Mungu wa Israeli, alivyoamuru.'' Yoshua 10:38-40<br><br>''[33]BWANA, Mungu wetu, akamtoa mbele yetu, tukampiga yeye na wanawe, na watu wake wote. [34]Tukatwaa miji yake yote wakati huo, tukaharibu kabisa kila mji uliokuwa na watu, pamoja na <u>wanawake na wadogo; tusimsaze hata mmoja..</u>.'' Kumbukumbu la Torati 2:33-35<br><br>''Kwa maana BWANA atateta na wote wenye mwili, kwa moto na kwa upanga wake; nao watakaouawa na BWANA watakuwa wengi.'' Isaya 66:16<br><br>''Na alaaniwe mtu afanyaye kazi ya BWANA kwa ulegevu; na alaaniwe auzuiaye upanga wake usimwage damu.'' Yeremia 48:10<br><br>''Wafungapo, mimi sitasikia kilio chao; na watoapo sadaka za kuteketezwa na sadaka ya unga, sitazitakabali; bali nitawaangamiza kwa upanga, na kwa njaa, na kwa tauni.'' Yeremia 14:12 | wote juu yenu, basi watimizieni ahadi yao mpaka muda wao; hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda waogopao). Attauba 4.<br><br>(Na kama mmoja wa washirikina akikuomba ulinzi, basi mlinde mpaka asikie maneno ya Mwenyezi Mungu, kisha mfikishe mahali pake pa amani. Hayo ni kwa sababu ya kuwa hao ni watu wasiojua. Itakuwaje ahadi kwa washirikina mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya Mtume Wake isipokuwa wale walioahidiana nao mbele ya Msikiti Mtukufu? Basi maadamu wanawanyokeeni, nanyi pia wanyokeeni; hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wamwogopao.) Attauba 6 – 7<br><br>(… Na kama wakijitenga wasipigane nanyi na wakakuleteeni amani, basi Mwenyezi Mungu hakukufanyieni njia juu yao.) Annisaa 90.<br><br><u>Majibu kwa kutumia hadithi tukufu za Mtume</u><br><br>Katika vita vya Uhudi, Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alitoka vitani akiwa amejeruhiwa, amevunjwa jino la pembe nne, kapasuliwa uso, |

| | | |
|---|---|---|
| Je, historia inajirejea pamoja na umma wa wapelestina?<br><br>Picha ya Mungu wa Agano la Kale kama wanavyoitaswiri baadhi ya wachoraji wa mahekalu na makanisa. | ‘’Kwa sababu hiyo BWANA wa majeshi asema hivi, Tazama, nitawaadhibu watu hawa; vijana watakufa kwa upanga; wana wao na binti zao watakufa kwa njaa.’’ Yeremia 11:22 ‘’Bali, kama hawataki kusikia, kung’oa nitaling’oa taifa lile, na kuliangamiza kabisa, asema BWANA.’’ Yeremia 12:17 ‘’[3]Maana BWANA asema hivi, katika habari za wana, na katika habari za binti, wazaliwao mahali hapa, na katika habari za mama zao waliowazaa, na katika habari za baba zao waliowazaa, katika nchi hii; [4]watakufa kwa maradhi mabaya; hawataliliwa, wala hawatazikwa; watakuwa kama samadi juu ya uso wa nchi; nao wataangamizwa kwa upanga, na kwa njaa; na mizoga yao itakuwa chakula cha ndege wa angani, na cha wanyama wa nchi.’’ Yeremia 16:3-4 ‘’Maana hiyo ni siku ya Bwana, BWANA wa majeshi, Siku ya kisasi, ili ajilipize kisasi juu ya adui zake; Nao upanga utakula na kushiba, Utakunywa damu yao hata kukinai...’’ Yeremia 46:10 ‘’]Naye akawatoa watu waliokuwamo, akawaweka kwenye kazi ya misumeno, na sululu za chuma, na mashoka ya chuma...’’ 2 Samweli 12:31 ‘’na hasira yangu itawaka moto, nami nitawaua ninyi kwa upanga; na wake wenu watakuwa wajane, na watoto wenu mayatima.’’ Kutoka 22:24 ‘’Nami nitaweka wivu wangu juu yako, nao watakutenda mambo kwa ghadhabu; watakuondolea pua yako na masikio yako; na mabaki yako wataanguka kwa, upanga; watawatwaa wanao na binti zako; na mabaki yako watateketea motoni.’’ Ezekieli 23:25 ‘’Akawaambia, itieni nyumba unajisi, mkazijaze nyua mizoga ya hao waliouawa; haya, enendeni. Wakaenenda, wakapiga-piga katika mji.’’ Ezekieli 9:7 ‘’Tena nyara zote za miji hiyo, na wanyama wa miji, wana wa Israeli walitwaa kuwa nyara zao wenyewe; lakini kila mtu wakampiga kwa makali ya upanga, hata walipokuwa wamewaangamiza wote, wala hawakumsaza mmoja mwenye kuvuta pumzi.’’ Yoshua 11:14 | na kuingia vipingili viwili katika taya yake, Baadhi ya Maswahaba zake wakamwambia: Ungewaombea laana ewe Mtume wa Allah. Akawajibu: “hakika mimi sikutumwa kulaani laani, lakini nimetumwa nikiwa ni mlinganiaji na rehema… Ewe Mola wangu waongoze watu wangu kwani hakika wao hawajui”.<br><br>Na Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, katika moja ya vita vyake alimuona mwanamke miongoni mwa maadui kauliwa, Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, akakasirika, akapinga na kusema: “Je, sikukukatazeni kuua wanawake? Huyu mwanamke hakuwa wa kuuliwa”.<br><br>Wakati ulipokombolewa mji wa Makka na Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, akaingia Makka akiwa na jeshi la watu elfu kumi, akiwa ameshinda, na Makureyshi wakajisalimisha kisha wakasimama mbele ya Kaaba wakisubiri hukumu ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, juu yao, na hilo ni baada ya vita vingi baina yao.<br><br>Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, hakuzidisha chochote zaidi ya kusema: Enyi makundi |

| | | |
|---|---|---|
| Je, muumini wa Agano la Kale amelaaniwa na kufukuzwa kutoka katika rehema za Mwenyezi Mungu endapo kama hajaua na kumwaga damu? | ''[11]Liangalie neno hili ninalokuamuru leo; tazama, mbele yako namtoa Mwamori, na Mkanaani, na Mhiti, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi. [12]Ujihadhari nafsi yako, usije ukafanya agano na wenyeji wa nchi ile unayoiendea, lisiwe mtego katikati yako. [13]Bali utabomoa madhabahu zao, na kuvunja-vunja nguzo zao, na kuyakata-kata maashera yao.'' Kutoka 34:11-13<br><br>''[23]Kwa kuwa malaika wangu atatangulia mbele yako, na kukufikisha kwenye Mwamori, na Mhiti, na Mperizi, na Mkanaani, na Mhivi, na Myebusi; nami nitawakatilia mbali. [24]Usiisujudie miungu yao, wala kuitumikia; wala usitende mfano wa matendo yao; bali utaiangamiza kabisa, na nguzo zao utazivunja vipande vipande.'' Kutoka 23:23-24<br><br>------------------------------------------------------------------<br><br>''Lakini kama hakumvizia, ila Mungu amemtia mkononi mwake; basi nitakuonyesha mahali atakapopakimbilia.'' Kutoka 21:13<br><br>------------------------------------------------------------------<br><br>''[10] Utakaposogea karibu ya mji kwenda kupigana juu yake, ndipo utakapowapigia ukelele wa amani. [11]Itakuwa utakapokujibu kwa amani, na kukufungulia, ndipo watu wote watakaoonekana humo watakufanyia kazi ya shokoa, na kukutumikia. [12]Na kwamba hautaki kufanya amani nawe, lakini utafanya vita juu yako, ndipo uuhusuru; [13]na BWANA, Mungu wako, autiapo mkononi mwako, mpige kila mume aliyemo kwa makali ya upanga; [14]lakini wanawake na watoto, na wanyama wa miji, na vilivyo mjini vyote, navyo ni nyara zake zote, uvitwae viwe mateka kwako; nawe utakula nyara za adui zako alizokupa BWANA, Mungu wako.'' Kumbukumbu la Torati 20:10-14 | ya Makureyshi, mnadhani nitawafanya nini? Wakajibu utatufanyia heri, wewe ni ndugu mkarimu na ni mtoto wa ndugu mkarimu. Akawaambia, leo ninakuambieni yale aliyoyasema ndugu yangu Yusuf hapo zamani: ''Hakuna tatizo juu yenu, Allah akusameheni, na Yeye ndiye Mbora wa wenye kusamehe. Nendeni nanyi mko huru''.<br><br>Miongoni mwa usia wa Abuu Bakri Asswidiiqu, Allah amuwie radhi, kwa kamanda wa jeshi lake ni: ''Usifanye usaliti, wala usivuke mipaka, wala usicharange maiti, wala usimuue mtoto mdogo, wala mzee sana, wala msikate mtende, wala msiuunguze, wala msikate mti wa matunda, wala msiwachinje kondoo wala ng`ombe, wala ngamia ila kwa ajili ya chakula. Pia mtapita kwa kaumu waliojitenga katika mahekalu yao, basi hao waacheni kile walichojitenga nacho''.<br><br>Katika usia wa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, ndani yake kuna makatazo ya wazi juu ya kucharanga miili ya maiti au kuharibu majengo au kuangamiza kila chenye manufaa maishani. Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema akilihusia jeshi katika |

| | | |
|---|---|---|
| | ''[2]wakati BWANA, Mungu wako, atakapowatoa mbele yako, nawe utawapiga; wakati huo ndipo uwaondoe kabisa; usifanye agano nao, wala kuwahurumia; wala usioane nao; [3]binti yako usimpe mwanawe mume, wala usimtwalie mwanao mume binti yake. [4]Kwa kuwa atamkengeusha mwanao mume asinifuate, ili wapate kuabudu miungu mingine; ndipo itakapowaka hasira ya BWANA juu yenu, naye atakuangamiza upesi. [5]Lakini watendeni hivi; zivunjeni madhabahu zao zibomosheni nguzo zao, yakateni maashera yao, ziteketezeni kwa moto sanamu zao za kuchonga. [6]Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa BWANA, Mungu wako...'' Kumbukumbu la Torati 7:2-6 | vita vya muutah: (Nakuhusieni kumcha Mwenyezi Mungu, na wale walio pamoja na nyinyi miongoni mwa waislamu muwafanyie ya heri. Piganeni kwa jina la Allah, pambaneni katika njia ya Allah dhidi ya kafiri anayemkufuru Allah, msifanye usaliti wala msivuke mipaka wala msimuue mtoto wala mwanamke wala mzee kikongwe wala aliejiepusha na kujiweka katika hekalu lake wala msiukaribie mtende wala msikate mti wala msibomoe jengo). |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anasaidia uuaji wa bila ya kukusudia? | ''Basi Wayahudi wakawapiga adui zao wote mapigo ya upanga, na machinjo, na maangamizo, wakawatenda kama wapendavyo wale waliowachukia.'' Esta 9:5 ''Nao Wayahudi wengine waliokaa katika majimbo ya mfalme walikusanyika, wakazishindania maisha zao, wakajipatia raha mbele ya adui zao, wakawaua waliowachukia, watu sabini na tano elfu; walakini juu ya nyara hawakuweka mikono.'' Esta 9:16 | Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Msivuke mipaka wala msifanye usaliti wala msicharange maiti wala msimuue mtoto na muogopeni Allah kwa wakulima ambao hawashiriki kukupigeni vitani) Sunanu Said bin Mansuuri. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaamrisha kudhalilishwa umma wakati wa kusuluhisha? | ''[2]Basi Israeli akaweka nadhiri kwa BWANA akasema, Kama wewe utawatia watu hawa mikononi mwangu kweli ndipo mimi nitaiharibu miji yao kabisa. [3]BWANA akasikiza sauti ya Israeli, akawatia Wakanaani mikononi mwao; nao wakawaharibu wao na miji yao kabisa; na jina la mahali hapo likaitwa Horma.'' Hesabu 21:2-3<br><br>''[9]Tangazeni haya kati ya mataifa; takaseni vita; waamsheni mashujaa; watu wa vita na wakaribie; na wapande juu. [10]Yafueni majembe yenu yawe panga, na miundu yenu iwe mikuki; aliye dhaifu na aseme, Mimi ni hodari. [11]Fanyeni haraka, mje, enyi mataifa yote, wa pande zote, jikusanyeni | Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Tokeni kwa jina la Allah, pambaneni katika njia ya Allah dhidi ya kafiri anayemkufuru Allah, msifanye usaliti wala msicharange maiti, wala msivuke mipaka wala msiwaue watoto wala watu wa mahekaluni) Sunanu Alkubra ya Albaihaqiyi. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaitisha vita vya dunia na kuwasha moto wa vita hivyo? | pamoja; na huko watelemshe mashujaa wako wote, Ee BWANA.'' Yoeli 3:9-11<br><br>''[14]Basi BWANA akawaletea Israeli tauni; nao wakaanguka wa Israeli watu sabini elfu.'' 1 Mambo ya Nyakati 21:14 | |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu anaua watu kwa dhambi iliyofanywa na Daudi? | | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaadhibu kwa kupika na kula nyama za watoto wakiume na watoto wa kike? | ''Mikono ya wanawake wapole iliwapika watoto wao. Wakawa chakula chao…'' Maombolezo ya Yeremia 4:10<br><br>''[28]Mfalme akamwambia, Una nini? Akajibu, Mwanamke huyu aliniambia, Mtoe mtoto wako, tumle leo, na mtoto wangu tutamla kesho. [28] Basi tukamtokosa mtoto wangu, tukamla, nikamwambia siku ya pili, mtoe mtoto wako, tumle; naye amemficha mtoto wake.'' 2 Wafalme 6:28 – 29 ''[28]ndipo nami nitakwenda kwa kuwashikia ninyi kinyume katika ghadhabu yangu; nami nitawaadhibu mara saba kwa dhambi zenu. [29]Nanyi mtakula nyama ya miili ya wana wenu, na nyama ya miili ya binti zenu mtaila.'' Mambo ya | Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Msimuue mtoto, wala mwanamke, wala mzee kikongwe, wala mgonjwa, wala padri/mchungaji, wala msikate mti wa matunda, wala msiharibu palipojengwa, wala msichinje ngamia, wala ng`ombe ila kwa ajili ya kula tu, msiangamize mtende wala msiuchome moto). |

| | | |
|---|---|---|
| Je, kula nyama ya binadamu ni adhabu ya mbinguni, kwa hiyo wazazi wanawala wana na wana wanawala wazazi?<br><br><br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa kuwala watoto wakati wa kuzingirwa? | Walawi 26:28-29 ''[7]… Bwana MUNGU asema hivi; Kwa sababu ninyi mmefanya ghasia kuliko mataifa wawazungukao ninyi, wala hamkuenda katika sheria zangu, wala hamkuzishika hukumu zangu... [10]Kwa sababu hiyo baba za watu watawala wana wao kati yako, nao wana watawala baba zao...'' Ezekieli 5:7-10<br><br>''Nami nitawalazimisha kula nyama ya wana wao, na nyama ya binti zao, nao watakula kila mmoja nyama ya rafiki yake, wakati wa mazingira na dhiki, ambayo adui zao, na watu wale watafutao roho zao, watawadhiikisha.'' Yeremia 19:9<br><br>''[53]Nawe utakula uzao wa tumbo lako mwenyewe, nyama ya wana wako na binti zako aliokupa BWANA, Mungu wako; katika mazingirwa… [55] hata asitake wao mmojawapo apewe katika nyama ya wanawe atakaowala… [57]… na juu ya mchanga wake atokaye katikati ya miguu yake, na juu ya wanawe atakaowazaa; kwa kuwa atawala kwa siri...'' Kumbukumbu la Torati 28:53-57 | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ni dhalimu hadi anaua watoto kwa sababu ya dhambi ya wazazi?<br><br><br>Je, Mungu anaamrisha | ''Fanyeni tayari machinjo kwa watoto wake. Kwa sababu ya uovu wa baba zao...'' Isaya 14:21 '' [15]… kwa ajili ya hayo namtolea BWANA wote wafunguao tumbo, wakiwa waume; lakini wazaliwa wa kwanza wote wa wana wangu nawakomboa.'' Kutoka 13:15 ''Kila kifunguacho tumbo, cha wenye mwili wote watakachomsongezea BWANA cha wanadamu na cha wanyama, ni chako...'' Hesabu 18:15<br><br>'' [28] Usimtukane Mungu, wala usimlaani mkuu wa watu wako. [29]Usikawie kuleta malimbuko ya matunda yako na ya vinywaji vyako. Mzaliwa wa | (Hakika wamehasirika wale ambao wamewaua watoto wao kwa upumbavu pasipo kujua, na kuharimisha Alivyowaruzuku Mwenyezi Mungu kwa kumtungia uwongo Mwenyezi Mungu. Bila shaka wamepotea wala hawakuwa wenye kuongoka). Al-Annaam 140.<br><br>Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, alikuwa pindi |


<table>
<tr><td rowspan="2">kumchinja mtoto wa kwanza awe mbadala wa wanyama?<br>________________</td><td>kwanza katika wanao waume utanipa mimi.’’ Kutoka 22:28-29</td><td rowspan="2">anapopeleka kikosi cha kijeshi anakiambia: (Piganeni kwa jina la Allah, katika njia ya Allah pambaneni dhidi ya kafiri anayemkufuru Allah, msivuke mipaka wala msifanye usaliti wala msicharange maiti na wala msimuue mtoto) Sahihi Muslimu.</td></tr>
<tr><td>Soma tafsiri ya kitabu cha Kutoka 13 (Tazama picha ifuatayo). Kanisa linaamini kuwa kabla ya kuja kwa Yesu, watu walikuwa wakimtoa kila mtoto wa kwanza wa kiume achinjwe na kuwa sadaka kwa Mungu ili watakasike waliobakia…, akaja Yesu na kuwa ndio mtoto wa kwanza ambaye atatolewe na kuchinjwa kwa ajili ya watu wote. .. Na kwa hiyo amewakomboa watu wote. Imani hii ya kuwatoa watoto wa kwanza wachinjwe inathibitisha ubaya wa Mungu huyu asiyeridhia chochote ila kuchinja watoto wa kwanza na kuhisi utamu wa harufu ya damu na kuunguza mizoga.</td></tr>
<tr><td>Swali: Je, sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuuwa, kuchinja na ugaidi?</td><td>Picha ya tafsiri ya kitabu cha Kutoka 13 iliyoandikwa kwa Kiarabu.<br><br>http://www.arabchurch.com/commentaries/father_antonios/Exodus/13<br>ويبدأ الإصحاح بقوله قدس لي كل بكر (آية2)= وقدس أي إفرز وخصص لله. فقبل العبور لابد من التقديس وإلا سيكون العبور عبوراً من عبودية إلى عبودية أخرى. والبكر هي أثمن وأعز شئ لدى العائلة، وهذا ما يطلبه الله أن نقدم له أثمن شئ عندنا. ونلاحظ أن هذه الوصية هي أول وصية يقدمها موسى ويأمر بها الله بعد الخروج مباشرة. وهي ليست وصية بمقدار ما هي وعد وعطية، فبخروج الشعب من دائرة العبودية والإنطلاق نحو أورشليم العليا (غل26:4) يدخل المؤمن في دائرة ملكية الله، ويصير عضواً حياً في هذا الملكوت الإلهي، إذ يقول الله "إنه لي" وتقول النفس وأنا له.. أنا لحبيبي وحبيبي لي.<br>http://www.arabchurch.com/commentaries/father_antonios/Exodus/13<br>ولقد اهتم الرب بموضوع البكور، وطلب البكر من الإنسان والحيوان والنباتات. راجع (لا23:10-14، 29-26:27 + عد15:19-21 + 20-13:18 + 23:19). والمفهوم أنه بتقديم البكر يتقدس الكل وبهذا يحسب أن الكل قد للرب. وكان هذا رمزاً لما صنعه لنا المسيح بكرنا، وبكر كل خليقة ورأسها (كو18:1،15 + رو29:8). فهو تقدم نيابة عنا نحو إخوته الأصاغر مقدماً حياته للآب ذبيحة طاعة وحب بلا عيب، فإشتمه أبوه الصالح رائحة رضا</td><td></td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale ni muuaji?</td><td>‘… bali waueni, mwanamume na mwanamke, mtoto naye anyonyaye, ng’ombe na kondoo, ngamia na punda.’’ 1 Samweli 15:3 ‘’Nitawaangamiza kabisa, asema BWANA; hapana zabibu katika mizabibu, wala tini katika mitini, hata jani lake litanyauka; na vitu vile nilivyowapa vitawapotea… [17] Maana, tazama, nitatuma nyoka, naam, fira, kati yenu,</td><td></td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| | wasiweza kutumbuizwa kwa uganga; nao watawauma, asema BWANA.'' Yeremia 8:13 - 17 | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaamrisha kuwasagasaga watoto na kupasua matumbo ya wajawazito?!! | ''Samaria atachukua hatia yake; kwa maana amemwasi Mungu wake; wataanguka kwa upanga; watoto wao wachanga watavunjwa vipande vipande, na wanawake wao wenye mimba watatumbuliwa.'' Hosea 13:16 ''Ndipo Menahemu akapiga Tifsa, na wote waliokuwamo, na mipaka yake, toka Tirza; kwa sababu hawakumfungulia, kwa hiyo akaupiga; nao wanawake wote waliokuwamo wenye mimba akawapasua.'' 2 Wafalme 15:16 | Dini yetu tukufu haiamrishi kuwasagasaga watoto na kupasua matumbo ya wajawazito!!!... Isipokuwa Dini yetu inamtia hatiani afanyaye hayo. |
| | Mpendwa msomaji:<br><br>Baada ya kusoma sura ya tano katika kitabu hiki.<br><br>Je, miongoni mwa sifa za Mungu ni kuwa huyo Mungu ni muovu wa kivita na muhamasishaji wa ugaidi? | |
| Sura ya sita: Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa yeye anatoa ufunuo wa visa vya kutunga, ngano na hekaya za ajabu? | | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anapenda visa na hekaya za ajabu za nyoka Lewiathani mwenye kuzonga-zonga na **lewiathani** na yule joka lilioko baharini?<br><br>Je, Mungu wa Agano la Kale anatumia visa vinavyoaminiwa na waabudu masanamu? | Lewiathani: ni aina ya kiumbe wa mchanganyiko wa mamba au nyoka. ''Katika siku hiyo BWANA, kwa upanga wake ulio mkali, ulio mkubwa, ulio na nguvu, atamwadhibu lewiathani, nyoka yule mwepesi, na lewiathani, nyoka yule mwenye kuzonga-zonga; naye atamwua yule joka aliye baharini.'' Isaya 27:1 ''[13]Wewe umeipasua bahari kwa nguvu zako, Umevivunja vichwa vya nyangumi juu ya maji. [14]Wewe uliviseta vichwa vya lewiathani...'' Zaburi 104:25-26 ''... Ndimo zipitamo merikebu, Ndimo alimo lewiathani ...'' Zaburi 74:13-14<br><br>Picha ya kubuni ya hilo joka kiumbe cha kifikirika katika ngano za watu wa kale akiwa baharini. \| Picha ya kubuni ya nyoka lewiathani kiumbe cha kifikirika katika ngano za watu wa kale. | Makafiri wa Kikureyshi na wengineo wanadai kuwa Quran Tukufu ni katika ngano za watu wa kale. (… hata wanapokufikia wanakujadili; wale waliokufuru wanasema: Hizi si chochote ila ni hadithi tu za watu wa kale). Al-An`am 25<br><br>Lakini wao hawakuweza kuthibitisha kuwa Quran Tukufu imechuliwa kutoka katika hizi hidithi za watu wa kale. Basi ni kipi kilichowakilisha wakashindwa kuleta sura moja mfano wa sura ya Quran kama walivyopewa changamoto na na Allah kwa kauli yake: (Na ikiwa mna shaka kwa hayo Tuliyomteremshia Mtumishi wetu, basi leteni sura iliyo |


| | | |
|---|---|---|
| |   | mfano wa hii, na muwaite wasaidizi …. i). Albaqarah: 23. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale anakipenda kisa cha ndege Phoenix? | Ngano ya: (Phoenix) wakati saa ya kufa kwake inapokaribia anawasha moto mkubwa katika kiota chake ili ajiunguze. Na baada ya kupita siku tatu tangu kutokea tendo la kujiua anaamka kutoka katikati ya majivu ndege Phoenix mpya. Na huyu ndege Phoenix anaashiria kufufuka kutoka katika mauti.<br>''… Nitakufa ndani ya kiota changu, Nami nitaziongeza siku zangu'' Ayubu 29:18  | |


| | | | |
|---|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale anawapenda wahusika wa kubuni wa ngano za kale, mfano: mtupunda,<br><br>lamia, lilith, na zimwi? | **Ngano ya mtupunda (<u>Onocentauris</u>):** huyu ni kiumbe ambaye nusu yake ya chini ni mwili wa punda na nusu yake ya juu ni mwili wa mtu.<br><br><br><br>Latin: Biblia Sacra Vulgata **…<u>Onocentauris</u>** …<br><br>Isaya 34:14 | **Ngano ya Lamia: Mwa-namke joka** anayenya-kua watoto na kufyonza damu zao hadi wanaku-fa.<br><br><br><br>I | Uislamu ulipokuja, ulizikana fikra hizo za kinganongano na hekaya za hovyo.<br><br>Uislamu unapigavita mazingaombwe na uchawi. |
| Je, kuna amana ya kifasihi katika kutafsiri lilith /satyr kutoka lugha ya Kingereza kwenda Kiarabu (mbuzi/pori?!)<br><br> | Ngano ya **Lilith** ipo katika vitabu vya Wayahudi kama vile ‘’Zuhuru bin Satyr’’ na ‘’Hazina inayolindwa katika Misingi ya Talmudi’’.<br><br>Ngano: Adamu alizini na shetani aitwaye: Lilith kisha akateremka naye pamoja na Eva hadi ardhini na kubeba maradhi na kifo.<br><br><br><br>**<u>International Standard Version</u> … Liliths, (Isaias 34:14)** | Douay-Rheims Bible…<br><br>… Lamia … (Isaias 34:14)<br><br>Ngano ya **Satyr** zimwi Manywele ni: kiumbe wa hovyohovyo kwenye ngano anatajwa katika visa pendwa na wengi.<br><br>Na kiumbe huyu anasifi-ka kwa kutisha/ukatili ili kuwahofisha watoto.<br><br><br><br>**<u>King James Bible</u>** | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | (Manywele anampigia ukulele mkewe na hapo anatulia Lilith…)<br><br>Ya Kikatoliki: (Wanyapori wa maeneo ya wazi wanakutana na mbwa mwitu, mbuzi pori ...) Isaya 34:14. | **…** satyr … (Isaya 34:14)<br><br>Na mbuzi pori ataitwa<br><br>kwake; naam, zimwi<br><br>anakaa huko na kujipatia nafasi…’’ (Isaya 34:14) (Imetafsiriwa<br><br>kutoka katika Tafsiri ya pamoja ya lugha ya<br><br>Kiarabu) | | | |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale anaamini Urimu na Thumimu? | **Urimu na Thumimu**: ni kama ramli na zinazingatiwa kuwa ni vitu vya kipagani kwa kuwa vinategemea uchawi na mazingaombwe … ambapo Kuhani anamwambia Mungu na kumwomba kitu fulani kwa kumwambia Mungu kama umekubali basi nijibu kwa Urim na hapo hapo Urim inatoa mwanga, na kama umekataa nijibu kwa Thumimu na hapo hapo Thumimu inatoa mwanga <br><br>''Nawe utie hizo <u>Urimu na Thumimu</u> katika kile kifuko cha kifuani cha hukumu...'' Kutoka 28: ''… akatia hizo <u>Urimu na Thumimu</u> katika hicho kifuko cha kifuani.'' Mambo ya Walawi 8:8 ''… hata atakaposimama kuhani mwenye <u>Urimu na Thumimu</u>.'' Nehemia 7:65 | Allah Mtukufu Aliyetukuka anamwachia mtu achague na kuamua akifanyacho, pia inawezekana kwa Muislamu kumuomba Allah amsaidie katika kuchagua kwake kwa dua ya kumuomba ushauri Allah.<br><br>Ama kuhusiana na kupiga ramli, hilo limekatazwa na Uislamu. (Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu; na kutazamia kwa mishale ya kupiga ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (ni) katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu (kutengenekewa). AL-Maidah 90.<br><br>(… na (ni haramu kwenu) kugawanya kwa mishale ya kuagua. Hayo ni uasi…). Almaidah 3 |
| Je, Mungu analeta ufunuo wa kisa cha jogoo arukaye **basilisks** na kinyonga **cockatrice**<br><br>Ambaye anatoka katika yai la jogoo?<br><br>Utakatifu u wapi katika tarjuma | ''Maana, tazama, nitatuma nyoka, naam, fira … '' Yeremia 8:17<br><br> <br><br>King James Bible version<br>(…**cockatrices** …) (Jeremiah 8:17)<br>(… cockatrice'…)(Isaiah 11:8)<br><br>English Revised Version<br>(…**basilisks**, …) (Jeremiah 8:17) | Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema katika hadithi nyingi: (Atakayemwendea kuhani (mpiga ramli) na kumsadikisha yale ayasemayo basi mtu huyo ameshakufuru yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad) Imepokewa na Attwabraaniyyu. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (tafsiri) zinazotofautiana ? | (… cockatrice…) (Isaiah 14:29)<br><br>(…cockatrice' … ) (Isaiah 59:5). | (… **basilisk's** …) (Isaiah 11:8)<br><br>(… **basilisk**…) (Isaiah 14:29)<br><br>(… **basilisks'**…) (Isaiah 59:5). | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa hadithi za ngano za kale kuhusu mnyama wa kinganongano **unicorn**?<br><br>Utakatifu u wapi katika tarjuma (tafsiri) zinazotofautian? | **Unicorn (Harishi)** ni kiumbe wa kingano mwenye umbo la farasi mweupe mwenye pembe moja. Hakuna athari yeyote ya kale inayothibitisha kuwahi kuwepo kwa kiumbe aliyeumbwa na Mungu mwenye sifa hizi. Kwa hakika kuna tofauti kubwa baina ya **Unicorn** na **nyati**.<br><br>**King James 2000 Bible** And the **wild oxen** shall come down with them … (Isaiah 34:7)<br><br>Isaya 34:7<br><br>''**Na nyati** watatelemka…'' Isaya 34:7 | **King James Bible** And the **unicorns** shall come down with them... (Isaiah 34:7).<br><br>Isaya 34:7<br><br>[7]**Na harishi** watatele-mka pamoja nao…''<br><br>Isaya 34:7<br><br>Picha za kubuni za farasi wa pembe moja (**unicorn).** | |

| | | |
|---|---|---|
| |   | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa viumbe vya kinganongano kwa mfano **dragons**?<br><br>Utakatifu u wapi katika tarjuma (tafsiri) zinazotofautiana ? | (Mungu akaumba nyangumi wakubwa…) Mwanzo 1:21<br><br>**King James 2000 Bible…**<br>**jackals** … Malachi 1:3<br> Mbweha<br>Jackal<br>''Bali Esau nimemchukia na kuifanya milima yake kuwa ukiwa, na urithi wake nimewapa **mwebweha wa nyikani.''** Malaki 1:3<br> Mbwa mwitu<br><br>**King James Bible** …<br>**dragons** …Malachi 1:3<br> Picha Ya kubuni ya Dragoni | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa viumbe vya kinganongano | Picha ya kubuni ya joka la moto 1<br><br>Picha ya kubuni ya joka | |

<table>
<tr>
<td>kwa mfano mijoka ya moto?</td>
<td>
<table><tr><td></td><td>la moto 2<br></td></tr></table>
''BWANA akatuma <u>nyoka za moto</u> kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa.'' Hesabu 21:6
</td>
<td></td>
</tr>
<tr>
<td>Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa viumbe vya kinganongano kwa mfano Behemoth?</td>
<td>
<table><tr><td>Picha ya kubuni ya Behemoth<br></td><td>Picha ya kubuni ya<br>Behemoth<br>
</td></tr></table>
''[15]Mwangalie huyo <u>kiboko</u>, niliyemwumba pamoja nawe; Yeye hula nyasi kama vile ng'ombe, [16]Tazama basi, nguvu zake ni katika viuno vyake,<br><br>
Na uwezo wake u katika mishipa ya tumbo lake. [17]Yeye hutikisa <u>mkia wake</u> mfano wa <u>mwerezi</u>; Mishipa ya <u>mapaja</u> yake yanaungamana pamoja.'' Ayubu 40:15-17<br><br>
Je, Behemoth = kiboko? Je, kiboko ana mapaja? Je, tafsiri ya Kiswahili ipo sawa?
</td>
<td></td>
</tr>
<tr>
<td>Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa viumbe vya kinganongano kwa mfano makerubi?</td>
<td></td>
<td>Uislamu umekuja kuwaweka huru wanadamu na mambo yote ya hovyohovyo. Sawa sawa yawe mambo ya kiimani au ya kitabia. Na kila jambo la hovyo ni kitu kibaya kwa uhakika wake hata kama kitahesabiwa kuwa ni katika mambo ya kujifakharisha nayo.</td>
</tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu anapanda kerubi na mawingu na makerubi katika kuhamahama kwake? | **Makerubi ni nani?**<br><br>Ezekieli 1:10<br><br><br><br>''Kwa habari za mfano wa nyuso zao; walikuwa na uso wa mwanadamu; na hao wanne walikuwa na uso wa simba upande wa kuume; na hao wanne walikuwa na uso wa ng'ombe upande wa kushoto; na hao wanne walikuwa na uso wa tai pia.''<br><br><br><br>''Ee BWANA wa majeshi, Mungu wa Israeli, ukaaye juu ya makerubi...'' Isaya 37:16 '...Ee BWANA, Mungu wa Israeli, ukaaye juu ya makerubi...'' 2 Wafalme 19:15 ''...Tazama, BWANA amepanda juu ya wingu jepesi...'' Isaya 19:1 ''Akapanda juu ya kerubi akaruka, Naam, aliruka...'' Zaburi 18:10 ''Na huo utukufu wa Bwana wa Israeli ulikuwa umepanda juu kutoka kwa kerubi...'' Ezekieli 9:3 ''...nao wakalileta toka huko sanduku la agano la BWANA wa majeshi, akaaye juu ya makerubi...'' 1 Samweli 4:4 | Mtume, rehema na amani ziwe juu yake alisimama mbele ya vigogo wengi wa Kiarabu, walioabudu mambo ya hovyohovyo kwa muda mrefu, na kuyafanyia mambo hayo ibada na matambiko, hadi yakawa mambo hayo ni ya dhati kwao wao, hayaepukani nao wala hayatengani nayo. Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema, pale alipoukomboa mji wa Makkah: "Zindukeni, hakika mimi nimeyaweka mapendeleo yote na takrima zote zilizokuwa katika zama za Jahiliya (ujinga) chini ya nyayo zangu ila kuhudumia Nyumba Tukufu na Kuwanywesha mahujaji." |

<table>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa viumbe vya kinganongano kwa mfano nyoka arukaye (flying serpent)?</td><td>''Ufunuo juu ya hayawani wa Negebu. Katikati ya nchi ya taabu na dhiki, Ambayo hutoka huko simba jike na simba, Nyoka na joka la moto arukaye…'' Isaya 30:6<br><br><br>''Usifurahi, Ee Ufilisti, pia wote, Kwa sababu fimbo ile iliyokupiga imevunjika; Maana katika shina la nyoka atatoka fira, Na uzao wake ni joka la moto arukaye…'' Isaya 14:29<br></td><td></td></tr>
<tr><td>Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa mauzauza ya kitabibu?</td><td>''Malaika akamjibu, akasema utakapoweka kitu chochote katika moyo wake juu moto, moshi unafukuza kila aina ya shetani… [9] na uchungu unafaa kupangusia macho yenye utando…'' Tubia 6:8 – 9<br><br>''…ukichoma ini la nyangumi shetani anashindwa...'' Tubia 6:19</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="3">Mpendwa msomaji:<br><br>Baada ya kusoma sura ya sita katika kitabu hiki: je, ni miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale kuleta ufunuo wa visa vya kufikirika, ngano na hadithi za hekaya?</td></tr>
<tr><td colspan="3">Sura ya saba: je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa yeye ni mjinga hajui sayansi?</td></tr>
<tr><td>Je, ardhi ni ya duara au ipo kama yai? Je, Mungu wa Agano la Kale anakaa juu ya duara la ardhi?</td><td>Isaya 40:22<br><br>Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia, na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi; yeye ndiye azitandazaye mbingu kama pazia na kuzikunjua kama hema ya kukaliwa;</td><td>(Na ardhi baada ya hayo Akaitandaza). Annaziat 30.</td></tr>
</table>

Je, Mungu wa Agano la Kale analeta ufunuo wa kuwako na tarjuma/tafsiri tofauti tofauti?

Je, wakazi wa ardhini ni kama nzige (panzi)?



Tafsiri zote za Kingereza zimetaja neno circle. Na circle = duara. Na kwa Kiebrania ni "חוּג" na hutamkwa "Khuuju"

**Kuna makosa katika tafsiri za Kiarabu**

| Tafsiri ya Al-Arabiya Mushtaraka Isaya 40:22 | Tafsiri ya Vandayki Isaya 40:22 |
|---|---|
| Yeye ndiye anayeketi juu ya mpira wa dunia, na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi; yeye ndiye azitandazaye mbingu kama pazia na kuzikunjua kama hema ya kukaliwa. | Yeye ndiye anayeketi juu ya kuba la dunia, na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi; yeye ndiye azitandazaye mbingu kama pazia na kuzikunjua kama hema ya kukaliwa |


**Je, kuna tofauti baina ya Kuba, Mpira na Duara?**

22. It is He Who sits above the circle of the earth, and whose inhabitants are like grasshoppers, who stretches out the heaven like a curtain, and He spread them out like a tent to dwell.

כב הַיֹּשֵׁב עַל חוּג הָאָרֶץ וְיֹשְׁבֶיהָ כַּחֲגָבִים
הַנּוֹטֶה כַדֹּק שָׁמַיִם וַיִּמְתָּחֵם כָּאֹהֶל לָשָׁבֶת:

**the circle:** Heb. חוג, an expression similar to (infra 44:13) "And with a compass (וּבַמְּחוּגָה)," a circle (compas in O.F.).


**and whose inhabitants:** are to Him [lit. before Him] like grasshoppers.





Maaana ya neno "Dahaahaa" katika kamusi, miongoni mwayo ni kamusi ya mtandaoni ya almaani.com inaeleza: lugha ya Kiarabu cha Kisasa: dahaa Allahu Al-ardha = ameitandaza, kuikunjua na kuipanua ikiwa katika umbo la yai kwa ajili ya kuweka makazi na kuijenga.


Kamusi ya Almuhiitwu inaeleza: Na Aluduhuwatu = sehemu ya kutagia mbuni mchangani.

Asswihaahu Fii Allughati = Na Udhiyyuhaa ni eneo amabalo hutotolewa vifaranga. Neno hilo ni la uzani wa ufu~uluulu litokanalo na dahautu kwa sababu ndege anatandaza hilo eneo kwa miguu yake kisha anataga katika eneo hilo.

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale ameumba mbingu zikiwa na nguzo zinazotikisika na kutetemeka? |   | (Ameziumba mbingu pasipo nguzo mzionazo; na Ameiweka milima ardhini ili (ardhi) isisukesuke nanyi; …). Luqman 10. |
| | Waandishi wa Agano la Kale walikuwa wanataswira kuwa dunia ni eneo bapa lililobebwa na nguzo na hizo nguzo hazibebwi na chochote. Na mbingu ni za duara zinazoizunguka dunia.<br><br>''Nguzo za mbingu zatetemeka, Na kustaajabu kwa kukemea kwake.'' Ayubu 26:11 | (Mwenyezi Mungu ndiye Aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona…). Arraad 2. |
| Je, Mungu wa Agano la Kale ameumba nyoka ili ale mchanga siku zote za uhai wake na akamuumba sisimizi bila kiongozi? | ''… kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako'' Mwanzo 3:14 ''Ewe mvivu, mwendee chungu… Kwa maana yeye hana akida, Wala msimamizi, wala mkuu,'' Mithali 6:6-7 | |
| Je, pimbi na sungura ni miongoni mwa wanyama wacheuao? | ''Na wibari, kwa sababu yeye hucheua... Na sungura, kwa sababu hucheua, lakini hana kwato, <u>yeye ni najisi kwenu</u>.'' Mambo ya Walawi 11:5-6<br><br> Sungura<br><br> Pimbi | |

| | | |
|---|---|---|
| Je, kuna ndege atembeaye kwa miguu minne, kwa mujibu wa tarjama ya Kiarabu? | ‘’Tena vyote vitambaavyo vyenye mabawa viendavyo kwa miguu minne,… hivi vitambaavyo vyenye mabawa viendavyo kwa miguu minne ni halali kula… [23]Lakini vyote vitambaavyo vyenye mabawa, vilivyo na miguu minne, ni machukizo kwenu.’’ Mambo ya Walawi 11:20-23<br><br>(Zingatia nzige si miongoni mwa ndege) | (Na radi inamsabihi kwa sifa Zake na (pia) Malaika kwa kumhofu; na Hupeleka mapigo ya radi na kumpiga nayo Amtakaye, nao wanabishana juu ya Mwenyezi Mungu, hali Yeye ni Mkali wa kuadhibu). Arraad 13. |
| Je, ’Wanyama wakapata mimba mbele ya hizo fito kwa hiyo wakazaa watoto wenye mistari mistari? | ‘’Wanyama wakapata mimba mbele ya hizo fito, wakazaa wanyama walio na milia, na madoadoa, na marakaraka.’’ Mwanzo 30:39 | |
| Je, ardhi ni mraba na ina pembe nne? | ‘’… Mwisho umezijia pembe nne za nchi.’’<br><br>Ezekieli 7:2 | |
| Je, Mungu ni dhaifu kijiografia? | ‘’Dhoruba hutoka kusini; Na baridi kaskazini mwake.’’ Ayubu 37:9 | |
| Je, ardhi imetandazwa juu ya maji?! | ‘’Yeye aliyeitandaza nchi juu ya maji…’’ Zaburi 136:6 | |
| Je, kwa upande wa kitabibu, ni vizuri kwa jicho kutazama jua? | | |

| | | |
|---|---|---|
| Je, kuna maji juu ya mbingu?<br><br>Je, siku za mwanadamu ni miaka 120? | ''Kweli nuru ni tamu, tena ni jambo la kupendeza macho kutazama jua.'' Mhubiri 11:7<br><br>---<br><br>''Msifuni, enyi mbingu za mbingu, Nanyi maji mlioko juu ya mbingu.'' Zaburi 148:4<br><br>''BWANA akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini.'' Mwanzo 6:3<br><br>--- | |
| Je, uwepo wa maji katika hatua ya awali ya uumbaji ni jambo linalopingwa kisayansi?<br><br>Uko wapi mzunguko wa ardhi kulizunguka jua? | ''Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi… Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji.'' Mwanzo 1:1-2<br><br>---<br><br>''Jua lachomoza, na jua lashuka, na kufanya haraka kwenda mahali pa maawio yake.'' Mhubiri 1:5<br><br>--- | Hayo ni wapi na wapi na kauli ya Quran Tukufu:<br><br>(Na Yeye ndiye Aliyeumba usiku na mchana na jua na mwezi: vyote vinaogelea katika duara (zao). Al-Anbiyaa 33.<br><br>(Ameumba mbingu na ardhi kwa haki, Hufunika usiku juu ya mchana, na Hufunika mchana juu ya usiku, na Amevitiisha jua na mwezi, vyote huenda kwa muda uliowekwa; jueni kwamba |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kesi ya mwanasayansi Galileo mbele ya kanisa likimtuhumu kuwa ni mzandiki kisha kumtesa na kumfunga jela kwa kuwa alisema: ‘jua limetulia na dunia ndio inalizunguka jua. Pia kwa sababu ya ugunduzi wake wa kisayansi kupingana na maandiko mawili ya Agano la Kale. |  | Yeye ni Mwenye nguvu, Msamehevu). Azzumar 5. |
| | ‘’Uliiweka nchi juu ya misingi yake, Isitikisike milele.’’ Zaburi 104:5 | ‘’Aitikisaye dunia itoke mahali pake, Na nguzo zake hutetema. Aliamuruye jua, nalo halichomozi; Nazo nyota huzipiga muhuri.’’ Ayubu 9:6-7 | (Je, hawakuona wale waliokufuru ya kwamba mbingu na ardhi vilikuwa vimeambatana kisha Tukaviambua; na Tukafanya kwa maji kila kitu kilicho hai; basi je, hawaamini?) Al-Anbiyaa 30. |
| | ‘’…, na mawingu ni mavumbi ya miguu yake.’’ Nahumu 1:3 | | (Je, hawakuona ya kwamba Tunaifikia ardhi Tukiipunguza mipaka yake…). Arraad 41. |
| Je, mawingu ni vumbi la miguu ya Mungu wa Agano la Kale? | Mawingu ni zao la mvuke wa maji ya bahari na mengineyo, wala sio vumbi?! | | (Yeye ndiye ambaye Huwaonyesheni umeme kwa hofu na tamaa, na Huinua mawingu mazito). Arraad 12. |
| | “Jua halitakupiga mchana, Wala mwezi wakati wa usiku.” Zaburi 121:6 | | |
| Je, kuna kitu kinachoitwa kupigwa na mwezi?! | ‘’Tena kwamba kuhani akiingia ndani na kuangalia, na tazama, ikiwa pigo halikuenea katika hiyo nyumba, baada ya nyumba kupakwa chokaa; ndipo kuhani atasema kwamba hiyo nyumba i safi, maana, | | (Na Akawatiishieni jua na mwezi, vifanyavyo kazi mfululizo. Na Akawatiishieni usiku na machana). Ibrahim 33. |

| | | |
|---|---|---|
| Je, Mungu wa Agano la Kale ameweka sheria ya kuwa tiba ya ukoma ndani ya nyumba ni kuumwagia ukuta wa nyumba hiyo kwa damu ya ndege aliyechinjwa?! <br><br> Jambo maarufu kisayansi ni kuwa damu ni sababu ya kuwepo vijidudu. Sasa iweje usafishe nyumba kwa vijidudu? | pigo limepoa. Naye atatwaa ndege wawili, na mti wa mwerezi, na sufu nyekundu, na hisopo, kwa kuitakasa hiyo nyumba; naye atamchinja mmojawapo wa ndege hao katika chombo cha udongo kilicho juu ya maji ya mtoni; kisha atatwaa huo mti wa mwerezi, na hisopo, na sufu nyekundu, pamoja na huyo ndege aliye hai, na kuvichovya vyote katika damu ya huyo ndege aliyechinjwa, na katika hayo maji ya mtoni, na kuinyunyiza nyumba mara saba; naye ataitakasa hiyo nyumba kwa damu ya ndege, na kwa maji ya mtoni, na kwa huyo ndege aliye hai, na kwa mti wa mwerezi, na kwa hisopo, na kwa sufu nyekundu; lakini ndege aliye hai atamwacha atoke mle mjini aende nyikani; ndivyo atakavyofanya upatanisho kwa ajili ya hiyo nyumba; nayo itakuwa safi. Hiyo ndiyo sheria ya pigo la ukoma ya kila aina, na ya kipwepwe;'' Mambo ya Walawi 14:48-54 | |
| | Mpendwa msomaji: <br><br> Baada ya kusoma sura ya saba katika kitabu hiki. <br><br> Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa huyo Mungu ni mjinga kielimu (kisayansi)? | |
| **Sura ya nane: Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa huyo Mungu ni dhaifu katika hisabati na nambari?** | | |
| Je, Mungu wa Agano la Kale hajui kuwa uwiano wa mzingo wa duara ni kipenyo cha duara kwa Pai ($\pi$) na sio 3? | ''Tena akaifanya bahari ya kusubu, mikono kumi toka ukingo hata ukingo, ya mviringo, na kwenda juu kwake ilikuwa mikono mitano; na uzi wa mikono thelathini kuizunguka kabisa.'' 2 Mambo ya Nyakati 4:2 na 1 Wafalme 7:23 <br><br> Mzingo wa duara = Pai × kipenyo | Uislamu unawalingania watu watafute elimu. <br><br> Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, amesema: (Atakayepita njia, akitafuta elimu katika njia hiyo, basi |

<table>
<tr>
<td>Je, Mungu wa Agano la Kale ni dhaifu katika hisabati?</td>
<td>Kwa kugawanya mzingo wa duara (urefu wa uzi) mikono 30 kwa kipenyo mikono 10 jibu lake = 3, na jambo linalojulikana ni kuwa Pai π si namba kamili na si sawa na "3", lakini Pai π si namba inayogawanyika na kuisha, takribani Pai = 3.141592 au 22/7.
<table>
<tr><td>"[13]Basi Gadi akamwendea Daudi, akamweleza, akamwambia, Basi, miaka saba ya njaa ikujie katika nchi yako? …".</td><td>"[11]Basi Gadi akamwendea Daudi, akamwambia, BWANA asema hivi, Kubali upendavyo;<br>[12]<u>miaka mitatu ya njaa</u>…"</td></tr>
<tr><td>2 Samweli 24:13</td><td>1 Mambo ya Nyakati 21:11-12</td></tr>
</table>
</td>
<td>Mwenyezi Mungu anamfanyia wepesi mtu huyo njia ya kuingia peponi) Imepokewa na Al-Bukhariyu.</td>
</tr>
<tr>
<td>Je, Mungu wa Agano la Kale anakosea katika nambari au ni kusahau?!</td>
<td>
<table>
<tr><td>"Haya ndiyo majina ya mashujaa aliokuwa nao Daudi; Yashobeamu Mhakmoni, mkuu wa maakida; huyo aliinua shoka lake juu ya <u>watu mia nane waliouwa pamoja</u>."</td><td>[11] Na hii ndiyo hesabu ya hao mashujaa aliokuwa nao Daudi; Yashobeamu, Mhakmoni, mkuu wa maakida; huyo aliuinua mkuki wake juu ya <u>watu mia tatu, akawaua pamoja.</u></td></tr>
<tr><td>2 Samweli 23:8</td><td>1 Mambo ya Nyakati 11:11</td></tr>
<tr><td>Ahazia alikuwa na umri wa <u>miaka ishirini na miwili</u> alipoanza kutawala; akatawala mwaka mmoja huko Yerusalemu…</td><td>Ahazia alikuwa na umri wa <u>miaka arobaini na miwili</u> alipoanza kutawala; akatawala mwaka mmoja huko Yerusalemu…</td></tr>
<tr><td>2 Wafalme 8:26</td><td>2 Mambo ya Nyakati 22:2</td></tr>
</table>
</td>
<td>Kwa ajili ya umuhimu wa elimu, Allah Mtukufu amemwamrisha Mtume wake, rehema na amani ziwe juu yake aombe ziada ya elimu kutoka kwake pale aliposema: (Basi Atukuzwaye ni Mwenyezi Mungu, Mfalme wa haki. Wala usifanye haraka kwa Qur'an, kabla haujamalizika<br><br>kukufikia ufunuo wake, na uombe: Mola wangu, nizidishie elimu). Ta-ha 114.</td>
</tr>
</table>

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Wana wa Zatu, mia nane arobaini na watano. | Wana wa Zatu, mia kenda arobaini na watano. | |
| | Nehemia 7:13 | Ezra 2:8 | |
| | Wana wa Bebai, mia sita ishirini na wanane. | Wana wa Bebai, mia sita ishirini na watatu. | |
| | Nehemia 7:16 | Ezra 2:11 | |
| | Wana wa Hashumu, mia tatu ishirini na wanane. | Wana wa Hashumu, mia mbili ishirini na watatu. | |
| | Nehemia 7:22 | Ezra 2:19 | |
| | Watu wa Betheli na Ai, mia moja ishirini na watatu. | Watu wa Betheli, na Ai, mia mbili ishirini na watatu. | |
| | Nehemia 7:32 | Ezra 2:28 | |
| | … Kisha walikuwa na waimbaji waume kwa wake mia mbili arobaini na watano. | … nao walikuwa na waimbaji waume kwa wake mia mbili. | |
| | Nehemia 7:67 | Ezra 2:65 | |
| | Wana wa Delaya, wana wa Tobia, wana wa Nekoda, mia sita na arobaini na wawili. | wana wa Delaya, wana wa Tobia, wana wa Nekoda, mia sita hamsini na wawili. | |
| | Nehemia 7:62 | Ezra 2:8 | |
| | Sulemani akawa na mazizi ya farasi na magari elfu nne.... | Tena Sulemani alikuwa na mabanda ya farasi arobaini elfu… | |
| | 2 Mambo ya Nyakati 9:25 | 1 Wafalme 4:26 | |

| | |
|---|---|
| … nao wa Yuda walikuwa watu mia tano elfu. | …na wa Yuda watu mia nne na sabini elfu, wenye kufuta panga. |
| 2 Samweli 24:9 | 1 Mambo ya Nyakati 21:5 |
| Yekonia alikuwa na umri wa miaka minane alipoanza kutawala… | Yekonia alikuwa na umri wa miaka kumi na minane alipoanza kutawala… |
| 2 Mambo ya Nyakati 36:9 | 2 Wafalme 24:8 |
| Daudi akampokonya wapanda farasi elfu na mia saba na askari waliokwenda kwa miguu ishirini elfu… | Daudi akampokonya magari elfu, na wapanda farasi saba elfu, na askari waendao kwa miguu ishirini elfu… |
| 2 Samweli 8:4 | 1 Mambo ya Nyakati 18:4 |

Mpendwa msomaji:

Baada ya kusoma sura ya nane katika kitabu hiki.

Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa huyo Mungu ni dhaifu katika hisabati na nambari?

## HITIMISHO

Mpendwa msomaji, baada ya kusoma sifa zinazohusishwa na Mungu katika Agano la Kale. Je, Mungu mwenye sifa hizo anastahiki kuabudiwa? Jibu ni hapana. Je unaamini kuwa maandiko ya sasa ya Agano la Kale yenyewe ni ufunuo wa Mungu? Bila shaka jibu ni hapana. Kwa hakika matokeo haya uliyoyafikia. Kwa hakika yamefikiwa na wengi wa kabla yako waliokuwa wakisifika kuwa wana moyo wa kuibagua na kuikosoa dini ya haki. Dini ya kuwa na Mungu mmoja tu. Dini ya Manabii na mitume wote. Dini ya Kiislamu. (Bila shaka dini hasa mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu; na waliopewa Kitabu hawakuhitilafiana ila baada ya kuwajia elimu, kwa sababu ya uasi uliokuwa kati yao; na anayezikataa Aya za Mwenyezi Mungu, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhesabu). Aali-Imran 19.

Ni yepi mazuri ya dini ya Kiislamu?

1- Uislamu unawatoa wanadamu kutoka katika kiza cha ushirikina (kumfanya Mwenyezi Mungu ana washirika) na kuabudu viumbe na kuwapeleka katika nuru ya kumpwekesha (kumfanya Mwenyezi Mungu ni wa peke yake) na kuwa na Muumba mmoja wa kumwabudu.
2- Uislamu si wenye kupita katika mapito ya maisha ya wale walioufuata Uslamu kabla ya kusilimu kwao, kwani watu hao walikuwa katika kilele cha ujinga na kubaki nyuma kimaendeleo na migogoro ya kikabila.
3- Uislamu umewaokoa wanawake kutokana na yale yaliyokuwa yanawatokea kabla ya Uislamu miongoni mwa dhulma kwa mfano, kuwazika watoto wakike wakiwa hai, kuwanyima haki zao na mirathi, pamoja na kuwafanyia miamala mibaya.
4- Uislamu unamtaka mtu atakayeuingia awe msafi wa roho na mwili.
5- Uislamu unazuia kuvifanyia uadui viumbe vya Mwenyezi Mungu, sawasawa ni wanadamu au wanyama au mimea.
6- Uislamu unambebesha anayeufuata jukumu la kuwalingania (kuwaita) watu waingie katika dini ya Allah ili kuwaokoa na moto.
7- Uislamu unakataza kula/kunywa kila kinachochafua akili miongoni mwa pombe au madawa ya kulevya.
8- Uislamu unalinda heshima, utu na nasaba kwa hiyo umeharamisha uzinzi.
9- Uislamu unalinda mali na milki za watu kwa hiyo umeharamisha wizi.
10- Uislamu unalinda mali (pesa), kwa hiyo umeharamisha ulanguzi (kuficha bidhaa kwa nia ya kulangua).
11- Uislamu unataka kuwepo kutoshelezana kijamii. Kwa hiyo ukaweka zaka ya lazima na kuhamasisha sadaka.
12- Uislamu unawafanya waja (watu) wa Allah kuwa ni sawa bila ya kutazama rangi zao. Kwa hiyo hautofautishi baina ya mweupe na mweusi.
13- Uislamu umelazima swala tano kwa wenye kuufuata ili wawe na muunganiko/mawasiliano na Muumba wao nyakati zote.
14- Milango ya kupata malipo haina idadi. Kwa hiyo Muislamu anapata malipo kwa kila anachokitenda akitarajia malipo na radhi za Allah.
15- Uislamu umeuacha mlango wa kutubu uko wazi mbele ya watu wote, jambo linalofufua utulivu wa nafsi na kuitika wito wa kutubia.
16- Kila anachokifanya mwanadamu miongoni mwa mema kinamfutia baadhi ya madhambi yake.
17- Uwepezi wa Uislamu na uwezo wa matabaka yote ya wanadamu kuufahamu unaufanya Uislamu ukubaliwe na watu bila ya kutahayari.
18- Unyumbulifu wa Uislamu na uwezo wake wa kuendana na kila jipya umeufanya udumishe uasilia wake.
19- Uislamu ni dini ya haki ya Mwenyezi Mungu, iliyoridhiwa naye kwa ajili ya viumbe wake wote. Lau kungekuwa na dini za kweli nyinyi, hilo lingelazimu kuwe na Miungu mingi. Allah ameepukana na hilo.

20- Uislamu ndio dini ya pekee ambayo wafuasi wake wana kitabu cha mbinguni kilichohifadhiwa kama kilivyo tangu kilipoteremshwa na Allah kwa Nabii wake, rehema na amani ziwe juu yake.
21- Mtume wa Uislamu, rehema na amani ziwe juu yake, ni Nabii wa pekee ambaye wafuasi wake walitilia umuhimu maelezo ya kina ya maisha ya Mtume wao na kile kilichotoka kwa mtume huyo miongoni mwa kauli au matendo na mwenendo wake safi, ndicho chanzo cha pili cha sheria za Kiislamu.
22- Wakati amababapo, jumbe za Mitume ya Allah iliyotangulia zilielekezwa kwa watu maalumu kwa wakati maalum, kwa hakika Ujumbe huu umeelekezwa kwa watu wote mpaka kitakaposimama kiama.
23- Uislamu ni dini ya pekee yenye wepesi kiasi ambacho, katika Uislamu, wafuasi wake wanamwabudu Muumba wao kwa mujibu wa maelekezo yake na sio kama katika vitabu wa wengine katika kile kiitwacho ‘‘nje ya vitabu vitakatifu”.
24- Unaamrisha kuwafanyia huruma madhaifu na maskini.
25- Unasafisha historia za Manabii wa Allah na kuziepusha na dosari walizotuhumiwa nazo na wale wasiokuwa Waisalamu.
26- Unaweka usawa baina ya fukara na tajiri katika miamala, katika misikiti, katika vikao. Kwa hiyo, si haki tajiri kumnyanyua fakiri atoke katika sehemu yake ili akae huyo tajiri sehemu hiyo.
27- Uislamu umelazimisha kufunga kwa waislamu ili uwafunze kudhibiti nafsi zao na kuhisi yale wanayoyahisi mafakiri miongoni mwayo kukosa mahitaji. Na hilo linawasukuma waislamu watoe sadaka.
28- Uislamu unainyanyua nafsi ya mtu. Kwa hiyo mtu hata ona kuwa kutafuta starehe za dunia ndio jambo la muhimu zaidi kwake.
29- Uislamu hautofautishi baina ya muislamu na asiyekuwa muislamu katika kuwapa sadaka.
30- Uislamu unampa jirani haki nyingi/kubwa hata kama sio muislamu.
31- Uislamu unahimiza kumheshimu mkubwa na kumhurumia mdogo.
32- Uislamu unawapa wazazi wawili haki kubwa/nyingi hata kama si waislamu.
33- Uislamu umelazimisha haki nyingi kwa mtoto hata kabla ya kuzaliwa kwake.
34- Uislamu umelazimisha kuwaamini Manabii wote wa Allah na kuwaheshimu.
35- Uislamu umelazimisha haki nyingi hata kwa maiti.

Vipi utaingia katika Uislamu? Mpendwa msomaji usiyekuwa Muislamu: Kwa hakika, kuingia katika dini ya Kiislamu ni kwepesi sana… Inakupasa uamini kuwa Allah ni mmoja naye ndiye mwenye kuyaendesha mambo yote ya ulimwenguni. Upende yale anayoyapenda Allah na uyachukie yale anayoyachukia Yeye. Na ufanye kutegemea kwako kote kuwe kwa kumtegemea yeye peke yake. Na hofu yako yote iwe kwake yeye peke yake. Na matarajio yako yote yawe kwake yeye peke yake. Na yeye awe mwelekeo wako na makusudio yako katika kila ibada yako na dua zako, na kuomba kwako msaada. Na maisha yako yote yawe kwa Allah peke yake. Na uache yale uliyokuwa ukiyaabudu na kuyaomba kinyume na yeye hapo kabla. Na uamini ya kwamba Allah ameepukana na kila sifa ya upungufu kwa mfano kuwa na mtoto (Hakuzaa wala hakuzaliwa) (Al-ikhlas 3). Na kuamini kuwa Masihi Yesu mwana wa Maryamu, amani iwe juu yake, yeye ni mja wa Allah, Mtume wake, neno lake aliloliweka kwa Maryamu, roho itokayo kwake. Ameumbwa na Allah kwa muujiza ya kiuungu kutoka kwa mama bila ya baba. Na ya kwamba hajasulubiwa isipokuwa amenyanyuliwa na Allah kwenda kwake. Yeye ni Nabii na Mtume kama walivyo Manabii na Mitume wengine. Mfano: Nuhu, Ibrahimu, Mussa na Muhammad, rehema za Allah ziwe juu yao wote.

Ewe mpendwa msomaji, kabla ya kuingia katika Uislamu inakupasa utamke shahada mbili kwa kusema kwa ulimi wako na moyoni mwako:
**“ASH-HADU AN-LAA ILAAHA ILLA LLAHA WA-ASH-HADU ANNA MUHAMMADAN RASUULU LLAH”**

Tafsiri yake: “Ninashuhudia ya kuwa hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na ninashuhudia ya kuwa Muhammad ni mtume wa Allah”.

Napenda kukupongeza kwa maamuzi yako haya ya kishujaa, maamuzi amabayo kwa haki kabisa yanazingatiwa kuwa ni maamuzi muhimu zaidi katika maisha yako. Kipindi hiki ulichoamua kujisalimisha kwa Allah Mola wa viumbe wote ni kipindi cha kuzaliwa kwako kikwelikweli. Hiki ni kipindi ambacho umejiweka huru na kuwaabudu wale waliomzushia uongo Allah, wakapotosha dini yao na wakafuata matamanio yao ya kuacha kumwabudu Mungu wa kweli. Na wewe sasa hivi, umeshakuwa katika dini ya Muhammadi na Masihi amani ziwe juu yao. Na jua ya kuwa neema kubwa kabisa aliyokuneemesha Allah ni kule kukuwezesha wewe kuingia katika Uislamu. Kwa hiyo fanya hima kumshukuru Allah vizuri kwa neema hii. Na jua, kwa hakika neema hii haifanani na neema yeyote nyingine. Chochote kitakachokugharimu kwa ajili ya kuilinda neema hii, basi hicho ni kidogo. Na kila janga baada ya janga la dini janga hilo ni dogo.

Tunamuomba Allah avikunjue vifua vyetu kwa vile tulivyotofautiana miongoni mwa haki kwa idhini yake. Hakika yake ni mwenye kusimamia hayo, na mwenye kuweza hayo, na mwisho wa dua yetu ni kumpa Allah Mola wa viumbe vyote kila sifa njema na shukuran zote.

Rejea:

1- Quran Tukufu.
2- Taurati na Maagano mawili; (la Kale na Jipya).
3- Tovuti za Kiislamu, Kiyahudi na Kikristo mtandaoni (internet).

**www.islamic-invitation.com**

**Yaliyomo**


| | | Ukurasa |
|---|---|---|
| | Utangulizi | 1 |
| Sura | Maswali | |
| Kwanza | Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kufanya uasherati, uzinzi na kujiweka uchi na ngono zembe? | 11 |
| Pili | Je, Roho Mtakatifu (nafsi ya tatu ya Mungu) wakati anapokuwa kwa mwanadamu anafanya maovu? | 25 |
| Tatu | Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kumfanyia uadui mwanamke? | 28 |
| Nne | Je Mungu wa Agano la Kale ana vitendo, mifananisho, sifa na maamrisho maovu? | 34 |
| Tano | Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kwamba yeye ni Mwovu wa kivita na muhamasishaji Ugaidi? | 68 |
| Sita | Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa yeye anatoa ufunuo wa visa va kutunga, ngano na hekaya za ajabu? | 77 |
| Saba | Je, ni miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale kuwa yeye ni mjinga hajui sayansi? | 83 |
| Nane | Je, miongoni mwa sifa za Mungu wa Agano la Kale ni kuwa huyo Mungu ni dhaifu katika hisabati na nambari? | 87 |
| Hitimisho | Ni yepi mazuri ya dini ya Kiislamu? Vipi utaingia katika Uislamu? | 90 |
| Rejea | | |


Nataraji kutoka kwa Allah Mtukufu aikubali kazi yangu na aifanye iwe kwa ajili yake yeye tu Mtukufu: nikitarajia radhi za Allah.

www.islsmic-invitation.com

KWA JINA LA MWENEZI MUNGU

MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

# SIFA ZA MWENYEZI MUNGU MTUKUFU KATIKA AGANO LA KALE NA QURAN TUKUFU

MTAYARISHAJI: RAAJII RIDHWA LLAAH

MTAFITI KATIKA MLINGANISHO WA DINI MBALIMBALI

KIMEPITIWA NA: ABUUKARIIMI ALMARAAKISHIYYU

HAKI ZA UCHAPAJI, KUSAMBAZA, KUTAFSIRI NA KUNAKIRI ZIMEHIFADHIWA KWA KILA MTU LAKINI KWA SHARTI LA KUTOBADILI CHOCHOTE.

Kimefasiriwa na Omari J. Mangilile

Kimepitiwa na Shaibu Swalehe Saidi

www.islamic-invitation.com